

**MATUMIZI YA MSAMIATI UNAOSAWIRI MAZINGIRA YA
KIZANZIBARI KATIKA RIWAYA ZA MUHAMMED SAID
ABDULLA**

Na

Saida Abdulla Said

Tasnifu Imetolewa kwa Ajili ya Kukamilisha Mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika
Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma

Chuo Kikuu cha Dodoma

Oktoba, 2015

ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyesaini hapa chini anathibitisha kwamba ameisoma na amependekeza tasnifu hii inayoitwa *'Matumizi ya Msamiati Unaosawiri Mazingira ya Kizanzibari Katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla'* ikubaliwe kwa minajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dodoma.

Saini.....

Dkt. Athumani S. Ponera

(Msimamizi)

Tarehe.....

IKIRARI
NA
HAKIMILIKI

Mimi, Saida Abdulla Said, ninathibitisha kwamba tasnifu hii ni kazi yangu asilia, na kwamba, haijawahi kuwasilishwa na wala haitawasilishwa katika Chuo Kikuu kingine chochote kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Uzamili au Shahada nyingine yoyote.



Saini.....

Tarehe 25/6/2015.

Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya tasnifu hii kwa namna yoyote bila kibali cha maandishi kutoka kwa Chuo Kikuu cha Dodoma.

SHUKURANI

Kukamilika kwa kazi hii si kwa nguvu zangu pekee bali ni matokeo ya ushiriki wa michango ya watu mbalimbali. Kwa ujumla, ninaithamini michango yao na imenisaidia sana. Natumia fursa hii kuwataja wachache lakini kwanza kabisa nimshukuru Allah kwa kunipa afya hadi kukamilisha kazi hii nzito. Pia, rehema na amani zimwendee kipenzi chetu Muhammad (S.A.W) pamoja na ahli zake.

Pili, ninatoa shukurani kwa msimamizi wa utafiti uliozaa tasnifu hii, Dkt. A. S. Ponera, kwa kunipa ushauri, maoni, mapendekezo na dira nzima ya kazi hii hadi kukamilika kwake. Ninamshukuru kwa uvumilivu mkubwa aliouonesha; kwani, pamoja na matatizo yaliyojiri, haikuwa ni kikwazo cha kushindwa bali ikawa ni chachu ya kusonga mbele. Allah ampe umri mrefu wenye mafanikio mazuri huko tunakokwenda.

Tatu, natoa shukurani kwa uongozi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, hususani uongozi wa masomo ya Shahada za Uzamili, chini ya Prof. Ahmed Ame pamoja na uongozi wa kitengo cha fasihi, Idara ya Kiswahili kwa usimamizi ulioniongoza hadi kufikia kukamilisha tasnifu hii. Pia, Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni, chini ya Dkt. Ziddy kwa ushirikiano uliowezesha kutimiza azma ya utafiti huu. Bila kuwasahau walimu wangu walionifundisha na wanaonifundisha. Allah awalipe ujira mwema wa kazi yao.

Nne, naishukuru familia yangu, hasa mume wangu mpenzi, Bw. Said Ali Abdulla kwa moyo alionionesha, na kunipa muda wa kutosha na hata kukubali kufarikiana naye kwa pale ilipobidi katika kuikamilisha kazi hii kwa mustawa unaotakiwa.

Tano, nizifikishe shukrani zangu kwa wanafunzi wa Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili na wale wote walioshiriki katika kila hatua niliyopitia. Mungu awabariki na kuwapa afya njema. Ammin.

TABARUKU

Kwa Said Ali Abdulla;

Ni peke anayefaa, kupewa hii ridhaa
Sikuwa ninajikwaa, pamoja na kushangaa
Kwa nguvu zilonijaa, namtunuku kifaa
Hii ni kama hidaa, niliyohisi yafaa.

Nguvuze nazithamini, kuzilipa siamini
Abadani asilani, hazilipiki jamani
Huyu ni wangu mwandani, musingie tafrani
Uwezowe siukhini, ajuwaye Rahmani.

IKISIRI

Tasnifu hii inahusu **Matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla**. Msamiati ni jumla ya maneno yaliyomo katika lugha. Hivyo, kwa mujibu wa utafiti huu maneno yenyewe yalichunguzwa kupitia riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale, Duniani Kuna Watu na Kosa la Bwana Msa*. Uchunguzi huu ulilenga kuchunguza na kubainisha msamiati huo na etimolojia yake pamoja na athari yake kwa wasomaji.

Sababu ya kuchunguza suala hilo lilitokana na mtafiti kuvutika na lugha ya utunzi wa riwaya hizo. Shabaha ni kupunguza au kuondoa tatizo la kutofahamika maana iliyokusudiwa kwa baadhi ya msamiati, hasa kwa wale ambao si weledi wa kucheza na lugha hiyo.

Mbinu ambazo zilitumika kupata data ni udurusu wa maandiko, udodosaji na mahojiano. Jamii tafitiwa katika uchunguzi huu ilikuwa ni ya Wazanzibari kwa kuwa ndiyo jamii ya mtunzi wa riwaya hizo. Data za uwandani zilizopatikana kwao zilichanganywa na zile za maktabani kupitia maandiko mbalimbali. Data hizi zilihusishwa na nadharia ya uhalisia kuhusu upatikanaji wa etimolojia sahihi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari na matukio ambayo yamo katika riwaya za mtunzi huyo ambayo yamekithiri msamiati huo.

Matukio ya uchunguzi huo yalibaini kuwa usawiri wa msamiati na mazingira ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla upo kwa kiwango kikubwa. Usawiri huo ulibainika zaidi kupitia miktadha ya maisha ya Wazanzibari kijiografia, kilugha, kisanaa na kiutamaduni. Aidha, msamiati uliobainika ulijikita katika vipengele vya kihistoria (kupitia lugha ya Kiarabu na Kiingereza), kiutamaduni (kupitia utamaduni wa dini ya Kiislamu), na kilahaja (kupitia vijilugha vya wakazi wa Zanzibar). Hali hiyo imetoa athari kwa wasomaji ya kuvutika na uandishi wa mtunzi huyo, kubaini historia na silika yake, kubaini umahiri wake wa matumizi ya visawe, kubaini historia na athari ya Wakoloni, kutambulisha lahaja na utofauti wake kimatumizi, kushajiisha matumizi ya msamiati uliopo hatarini kupotea, na kuathiri watunzi wengine wa Zanzibar waliomfuatia. Pia matokeo ya uchunguzi huo yametoa mchango mpya kwa kuorodhesha msamiati na asili zake katika riwaya hizo.

YALIYOMO

Uk.

ITHIBATI YA MSIMAMIZI	i
IKIRARI NA HAKIMILIKI	ii
SHUKURANI	iii
TABARUKU	v
IKISIRI	vi
YALIYOMO	vii
ORODHA YA MAJEDWALI	x
VIFUPISHO	xi

SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

1

1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti.....	1
1.1.1 Etimolojia	1
1.1.2 Msamiati.....	1
1.1.3 Riwaya.....	1
1.1.4 Lahaja	2
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti	2
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti	6
1.4 Malengo ya Utafiti	7
1.4.1 Lengo la Jumla	7
1.4.2 Malengo Mahususi	7
1.5 Maswali ya Utafiti	7
1.6 Umuhimu wa Utafiti.....	8
1.7 Maelezo Mafupi Kuhusu Muhammed Said Abdulla.....	8
1.8 Nadharia ya Uchanganuzi wa Data	11
1.9 Mipaka ya Utafiti	14
1.10 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake	14
1.11 Muhtasari wa Sura ya Kwanza	14

SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO

15

2.1 Utangulizi	15
2.2 Maandiko Kuhusu Matumizi ya Lugha kwa Ujumla	15

2.3 Maandiko Kuhusu Kazi za Muhammed Said Abdulla.....	17
2.4 Mapengo Yanayopaswa Kuzibwa.....	23
2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili	24
SURA YA TATU: USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI.....	25
3.1 Utangulizi	25
3.2 Mpango wa Utafiti	25
3.3 Eneo la Utafiti	25
3.4 Walengwa wa Utafiti.....	26
3.4.1 Jamii Tafitiwa.....	26
3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa	26
3.5 Ukusanyaji wa Data	27
3.5.1 Njia na Zana za Ukusanyaji wa Data	27
3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data.....	27
3.6 Uchanganuzi wa Data.....	28
3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti	29
3.8 Itikeli za Utafiti	29
3.9 Muhtasari wa Sura ya Tatu.....	29
SURA YA NNE: UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA	
UTAFITI.....	30
4.1 Utangulizi	30
4.2 Miktadha ya Maisha ya Wazanzibari	30
4.2.1 Muktadha wa Kijiografia	31
4.2.2 Muktadha wa Kiuchumi	32
4.2.3 Muktadha wa Kiutamaduni	33
4.2.4 Muktadha wa Kiisimu	35
4.2.5 Muktadha wa Kisanaa	37
4.3 Muhtasari wa Riwaya Teule.....	38
4.3.1 Muhtasari wa Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale	38
4.3.2 Muhtasari wa Riwaya ya Duniani Kuna Watu.....	39
4.3.3 Muhtasari wa Riwaya ya Kosa la Bwana Msa	40

4.4 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Miktadha ya Kizanzibari katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla na Etimolojia Yake	42
4.4.1 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Miktadha ya Kizanzibari na Etimolojia Yake katika Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale.....	46
4.4.2 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Miktadha ya Kizanzibari na Etimolojia Yake katika Riwaya ya Duniani Kuna Watu.....	56
4.4.3 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Miktadha ya Kizanzibari na Etimolojia Yake katika Riwaya ya Kosa la Bwana Msa.....	77
4.5 Athari za Msamiati Unaoakisi Miktadha ya Kizanzibari Katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla kwa Wasomaji.....	97
4.5.1 Tija Zilizopatikana	101
4.5.1.1 Kuvutika na Uandishi Wake	101
4.5.1.2 Kubainisha Historia na Athari ya Wakoloni kwa Wenyeji wa Zanzibar .	103
4.5.1.3 Kubainishwa kwa Historia na Silika ya Mtunzi.....	104
4.5.1.4 Kutambulisha Lahaja Mbalimbali na Kuzitofautisha Kimatumizi	106
4.5.1.5 Kurahisisha Kueleweka kwa Maudhui.....	106
4.5.1.6 Kushajiisha Matumizi ya Msamiati Uliopo Hatarini Kupotea.....	107
4.5.1.7 Kubainisha Umahiri wa Mtunzi Katika Matumizi ya Visawe	107
4.5.1.8 Kuathiri Watunzi Wengine wa Zanzibar Waliomfuatia.....	108
4.5.2 Madhara Yaliyopatikana	110
4.6 Muhtasari wa Sura ya Nne	111
SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO	112
5.1 Utangulizi	112
5.2 Muhtasari wa Tasnifu.....	112
5.3 Hitimisho	113
5.4 Utoshelevu wa Nadharia	114
5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo.....	115
5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano.....	116
MAREJELEO	117
VIAMBATISHO	122

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Muhtasari wa Msamiati Kutoka katika Mzimu wa Watu wa Kale na Etimolojia Yake	52
Jedwali 2: Muhtasari wa Msamiati Kutoka Katika Duniani Kuna Watu na Etimolojia Yake	67
Jedwali 3: Muhtasari wa Msamiati Kutoka katika Kosa la Bwana Msa na Etimolojia Yake	86

VIFUPISHO

ASP - *Afro Shirazi Party*

BAKIZA - Baraza la Kiswahili Zanzibar

Bw. - Bwana

Dkt. - Daktari

http - *Hyper Text Transfer Protocol*

Kur. - Kurasa

Na. - Nambari

Prof. - Profesa

SAW - *Swallallahu Alayhi Wasallam*

SUZA - *The State University of Zanzibar*

UDOM - *The University of Dodoma*

Uk. - Ukurasa

www - *World Wide Web*

ZEB - *Zanzibar Economic Bulletin*

ZIP - *Zanzibar Investment Policy*

SURA YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Ufafanuzi wa Istilahi Muhimu Zilizotumika katika Utafiti

1.1.1 Etimolojia

Ni elimu ya asili ya maneno na njia ambazo maana zilivyobadilika kulingana na wakati (*Kamusi ya Oxford Advanced Learners*, 2009). Dhana hii huchunguza maendeleo ya maneno katika lugha ambayo hupatikana kwa njia mbalimbali kama vile njia ya utohoaji kutoka lugha moja kwenda lugha nyingine, uambishaji na uvunjaji wa neno. Katika utafiti huu dhana hii imetumika kubainisha asili ya neno lilipotokea na maana yake ilivyo na ilivyotumika katika riwaya teule za Muhammed Said Abdulla.

1.1.2 Msamiati

Ni maneno yote yanayotumika katika lugha (*Kamusi ya Oxford Advanced Learners*, 2009: na *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, 2010). Kwa mujibu wa utafiti huu, neno msamiati halijatumika si kwa maneno yote yaliyotumika katika vitabu teule isipokuwa, kwa baadhi tu ya maneno yaliyosawiri mazingira ya Kizanzibari.

1.1.3 Riwaya

Ni kisa ambacho urefu wake unakiruhusu kitambe na kutambaa mahali pengi na kuambaa vizingiti vingi vya maisha kama apendavyo mwandishi wake. Ni hadithi ndefu ya kubuni, yenye visa vingi, wahusika zaidi ya mmoja na yenye mazungumzo na maelezo yanayozingatia kwa undani na upana maisha ya jamii (Senkoro, 1982:73 - 74). Riwaya hueleza kadhia nyingi sana ambazo mara nyingi huisawiri jamii ilivyo. Hivyo, hubaki kuwa ni kielelezo cha jamii ambacho mwandishi ameamua kukiweka

katika hali ya maandishi kitabuni. Sio ndoto ambazo mwandishi huota katika usingizi, anachokiandika hutokana na uhalisi wa jamii husika.

1.1.4 Lahaja

Ni aina fulani ya lugha ambayo ni pekee kwa kanda maalumu au kundi la kijamii (*Kamusi ya Oxford Advanced Learners, 2009*). Lahaja hujitokeza katika lugha moja. Hii ina maana kuwa kila lugha ina lahaja zake. Kwa mfano, Kiswahili kina lahaja nyingi kama vile Kimakunduchi, Kimrima, Kimtang'ata, Kitumbatu, Kipemba na Kingazija. Mipaka yake ni midogo sana na mara nyingine huweza kuathiriana kwa namna moja au nyingine. Kwa mfano, unaweza kukuta neno moja linatumika katika lahaja mbili au tatu kwa maana moja. Mara nyingine huweza kubadilika matamshi au kutobadilika. Kwa mfano, neno 'bezo' hutumika katika lahaja kuu zote za Zanzibar, Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba bila kubadilika maana wala matamshi.

1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

Dhana za msamiati na maneno ni kitu kimoja. Hata hivyo, neno msamiati huweza kutafsiriwa kama ni maneno magumu. Maneno hayo hutumika katika ufahamu au kifungu cha habari fulani na kawaida hufafanuliwa kabla ya kusoma. Pia huweza kutafsiriwa kama ni maneno ambayo hayawezi kupatiwa maana moja. Kwa mfano, neno tabasamu linaweza kutumika kwa maana tofauti. Hivyo, tunapozungumzia matumizi ya msamiati tuna maana tunaizungumzia lugha, ingawa lugha ni kitu kikubwa sana katika maisha ya binadamu.

Wallek na Warren (1984) wanaeleza kuwa uhusiano kati ya lugha na fasihi ni wa lazima. Kazi ya sanaa inayotumia maneno, kwa kiwango kikubwa, huathiri ukuaji wa lugha na maendeleo yake. Kifaransa na Kiingereza cha leo zisingefikia hali zilivyo bila ya fasihi ya kale. Vivyo hivyo, lugha ya Kijerumani isingekuwa kama

ilivyo bila ya kuathiriwa na Martin Luther Schriften, Johann Wolfgang von Goethe pamoja na wasanii waliofuatia. Hili linatubainishia kuwa hata Kiswahili kinaweza kupata mchango wa maneno kupitia fasihi ama kwa kusawiri maneno na pahala fulani au vinginevyo.

Katika fasihi, kipengele cha lugha hutumika kwa upana kwa sababu ndiyo muhimili wake. Hutumika kama tamathali za semi (kama vile tash-biha, tash-hisi, sitiari, na tauria), hutumika kama mbinu nyingine za kisanaa (kama vile jazanda na taswira) na pia hutumika kama semi (kama vile methali, misemo, nahau, mafumbo, na vitendawili). Vipengele hivyo, mara nyingi, watunzi huvitumia katika kazi zao kulingana na mazingira yao wanamoishi. Ni nadra kuikuta fasihi iliyotungwa Ukerewe ikiwa na msemu wa Kipemba au kinyume chake. Lakini, unaweza kukuta msemu wa Kiswahili kwa kuwa Kiswahili kina uwanja mpana. Utafiti huu ulijikita katika kipengele cha msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari kwa kutalii kipengele cha lugha katika riwaya za Muhammed Said Abdulla.

Zanzibar ni nchi yenye visiwa vikuu viwili, Unguja na Pemba. Visiwa hivyo vipo umbali wa kilomita 40 kutoka mwambao wa Afrika Mashariki. Katika bahari ya Hindi vipo baina ya nyuzi 5 mpaka 6 za Latitudo kwa upande wa Kusini na nyuzi 39.5 mpaka 40 za Longitudo kwa upande wa Mashariki. Jumla ya eneo la kilomita za mraba kwa visiwa hivi ni 2,654; ikiwa Unguja ni 1,666 na Pemba ni 988 (ZIP, 2006:4). Jamii na utamaduni wa Zanzibar ni wa mchanganyiko ambao unaonekana moja kwa moja kupitia majengo, mfumo wa maisha, lugha na watu wenye makabila mchanganyiko. Kiswahili ndiyo lugha kuu ya nchi ingawa lugha nyingine hutumika kama vile Kiingereza, Kiarabu, Kifaransa na Kitaliano. Zanzibar imekuwa ikiitwa kwa majina mbalimbali. Majina hayo ni kama vile ardhi ya viungo asilia, visiwa vya

wapendanao, ardhi yenye kila aina ya wafanya biashara na wavumbuzi, mji mama wa Afrika ya Mashariki, pepo ya Afrika, visiwa vya amani na upendo, na kitovu cha Kiswahili sanifu (ZEB, 2004:27).

Sensa ya watu na makazi ya mwaka 1988 ilibainisha jumla ya watu 640,685; ambapo mwaka 2002 idadi hiyo ilikua hadi kufikia 984,531 sawa na ongezeko la asilimia 3.1 (ZIP, 2006:4). Mwaka 2011 ilibainika kuwa Zanzibar ina jumla ya watu 1,200,000; ambapo asilimia 40 ya watu wake wanaishi mjini na asilimia 60 wanaishi vijijini. Ongezeko la watu wake linatokana zaidi na kiwango cha juu cha uzazi ambacho ni 5.3 (Suleiman na Onkolo, 2011). Wenyeji wa Zanzibar ni Wapemba ambao wanaishi katika kisiwa cha Pemba, wenye asili ya sehemu tofauti kama vile Lamu - Kenya, Uajemi, na wengi kutoka Uarabuni. Wengine ni Watumbatu wanaoishi kisiwani Tumbatu, kisiwa kidogo kilichopo Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja kiasi cha kilomita 48 kutoka mjini Zanzibar. Ni kisiwa chenye jumla ya kilomita 15.5 kwa urefu na 2.5 kwa upana. Na wengine ni Wahadimu (Wamakunduchi) wanaoishi katika wilaya ya Kusini Unguja. Wilaya hiyo ina miji kama vile Pete, Jozani, Kitogani, Paje, Jambiani, Muungoni, Muyuni, Kizimkazi, Kibuteni, Mtende na Makunduchi yenyewe ambayo ndio makao makuu ya lahaja ya Kihadimu (Kimakunduchi). Asili yao ni kutoka Windi na mwaka 1870 walitokea Uajemi (BAKIZA, 2012; Haji 2006; na Werner 1916).

Kabla ya kuwapo kwa lugha moja inayotumika kwa wakazi wote wa Zanzibar, historia inaeleza kuwa kulikuwa na lahaja ambazo wenyeji wa Zanzibar - Wapemba, Watumbatu na Wamakunduchi - wakizitumia katika mawasiliano yao. Lahaja hizo zilikuwa zikitofautiana kimsamiati na kilafudhi baina ya watu wa sehemu moja na

nyingine. Hali hiyo ipo mpaka sasa kwani lahaja hizo zipo lakini zimepata athari nyingi kitendo ambacho kimeweza kupunguza kasi na uimara wake.

Khatib (1983) anaeleza lahaja kuu za Zanzibar kuwa ni Kiunguja mjini, Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba. Pia anaendelea kueleza kuwa, msingi wa Kiswahili sanifu unatokana na Kiunguja mjini. Msingi huo ulitokea pale kamati ya elimu ya Kikoloni iliyoitwa *Phelps Stoke Cummission* ilipofika Afrika Mashariki mwaka 1925. Lengo lao lilikuwa ni kupendekeza kuhusu haja ya kuwapo lugha moja sanifu itakayotumika katika nchi nne za Afrika Mashariki. Nchi hizo ni Zanzibar, Tanganyika, Uganda na Kenya. Hatimaye, mwaka 1930 Kiunguja mjini kilitumika katika shughuli zote za kielimu na za kiserikali.

Kiunguja mjini ni lahaja iliyokuwa ikizungumzwa mjini Unguja. Lahaja hii ndiyo msingi wa Kiswahili sanifu. Haina maana kwamba baada ya kupatikana kwa lugha sanifu, zile lahaja zilipotea. Bado zipo na zinatumiwa kila siku. Ushahidi wa hayo ni kuwa lahaja hizo zimeshatafitiwa na wataalamu wengi kama vile Ingrams (1924), Maganga (1991), Whitely (1960), Temu (1980), Juma (2011), Haji (2006), Idd (2010) na Khamis (2012). Wataalamu hao wamezichunguza lahaja hizo kupitia kipengele cha lugha; matamshi, muundo, maumbo, maana, kufanana na kutofautiana kimatamshi na kimaana. Pia, BAKIZA (2012) imeandaa kamusi za lahaja hizo.

Muhammed Said Abdulla alizaliwa kabla ya kupatikana lugha moja iliyotumika kwa wakazi wote wa Zanzibar, Tanganyika, Kenya na Uganda. Hii inatokana na ukweli tuliodokezwa hapo awali kuwa Zanzibar kabla ya kupatikana lugha moja kulikuwapo vijilugha ambavyo wakazi wake walivitumia. Hakuna ithibati kamili inayoonesha kuwa Muhammed Said Abdulla alikuwa ni mtumiaji wa kijilugha fulani. Hata hivyo, bila shaka, hakuna binadamu anayeishi bila ya mawasiliano. Na

kwa kuwa mtunzi huyu alikuwa ni mpekuzi wa mambo hakuna shaka na ujuaji wa lahaja nyingine zilizokuwapo Zanzibar kwa sababu lahaja zenyewe zinalingana kupitia msamiati na maana.

Lugha aliyoitumia katika utunzi wake ni Kiswahili ambacho msingi wake ni lahaja ya Kiunguja mjini. Katika utunzi wake kumejitokeza shida ya baadhi ya maneno ambayo maana zake ni fiche. Mfano wa maneno hayo ni kumzaini, kwasi, mwande, kimeme, kumuanisi, mbwanda, soli, alimbibidia, nikidinda, machugachuga, kukoroweza, kite, fetwa, kuntajili, kinyangaa, maarubu, kubeua, zuhali, kihunzi, uharara, ghera na bera. Maneno hayo, mengi ni Kiswahili fasaha kwa sasa, yenye asili ya Kiarabu na lahaja zilizopo Zanzibar; Kiunguja mjini, Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba. Mfano, maneno kama (bera, kuntajili, pumbao) - Kitumbatu, (kite, machugachuga, mwande) - Kimakunduchi, (uharara, kusowera, kujishaua) - Kiunguja mjini na; (kukoroweza, kunisusuika, sodawi) - Kipemba. Matumizi ya msamiati huo yamezua changamoto ya ugumu wa kufahamika kwa wasomaji na wahakiki. Changamoto hiyo inaweza kumalizika kutokana na shabaha ya utafiti huu ya kuchunguza matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari kupitia riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* (1958), *Duniani Kuna Watu* (1976) na *Kosa la Bwana Msa* (1984).

1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti

Lugha ndiyo muhimili na uti wa mgongo wa kazi yoyote ya fasihi. Inafahamika kuwa riwaya za Muhammed Said Abdulla ni riwaya zilizotumia Kiswahili sanifu lakini mara nyingine riwaya hizo huleta ugumu kwa wanafunzi na wahakiki wakati wa kuzisoma. Ugumu huo hutokana na kutumika kwa msamiati wenye maana fiche. Yumkini, tatizo hilo linatokana na ukweli kuwa kuna baadhi ya msamiati umesawiri mazingira ambayo riwaya hizo zimetungwa. Muhammed Said Abdulla ni mzaliwa

wa Zanzibar, tangu kabla ya kupatikana kwa lugha moja iliyotumika kwa wakazi wote. Inawezekana kwamba ugumu unaotokea kwenye baadhi ya msamiati katika riwaya zake unatokana na usawiri wake wa lugha na mazingira alimoishi. Hivyo basi, katika kutatua tatizo hilo, mtafiti ameamua kuchunguza msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya zake.

1.4 Malengo ya Utafiti

1.4.1 Lengo la Jumla

Kuchunguza matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla.

1.4.2 Malengo Mahususi

Malengo mahususi ya utafiti huu ni:

- a) Kubainisha miktadha ya maisha ya Wazanzibari,
- b) Kubainisha matukio yenye msamiati unaoakisi miktadha ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla na kuchambua etimolojia yake, na;
- c) Kutathmini jinsi msamiati unaoakisi miktadha ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla unavyowaathiri wasomaji.

1.5 Maswali ya Utafiti

Maswali ambayo yaliuongoza utafiti huu kuyafikia malengo yake ni:

- a) Miktadha ya maisha ya Wazanzibari ni ipi?
- b) Matukio yenye msamiati unaoakisi miktadha ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla ni yepi na etimolojia yake ni ipi?
- c) Kwa jinsi gani msamiati unaoakisi miktadha ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla huwaathiri wasomaji?

1.6 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti uliofanywa yanategemea kuleta manufaa yafuatayo: Mosi, kusaidia kuondoa kikwazo cha matumizi ya msamiati kwa wasomaji wa riwaya za Muhammed Said Abdulla. Pili, kuongeza juhudi za kuyachambua maandishi ya Muhammed Said Abdulla kwa kupata usawiri wa maandishi yake na Wazanzibari. Tatu, kusaidia kutoa historia ya Zanzibar kwa upande wa lugha waliyokuwa wakitumia wenyeji wake. Na nne, kusaidia kuweka wazi asili ya maneno na namna ambavyo mtunzi ameyatumia na kuyabadili.

1.7 Maelezo Mafupi Kuhusu Muhammed Said Abdulla

Mjawiri (2011) anaeleza kuwa, Muhammed Said Abdulla amezaliwa mwaka 1918 katika mtaa wa Malindi, Mji Mkongwe Zanzibar. Alikuwa ni mtoto wa pekee katika familia ya mzee Said mwenye asili ya Yemen. Mama yake ni Anoi binti Mselem mwenye asili ya Maskati kutoka ukoo wa Al-Khalas. Muhammed Said Abdulla alifariki mwaka 1992 akiwa na miaka 72 na kuzikwa Mwanakwerekwe Zanzibar. Mke wake ni Bi Thneyuu Muhammed Juma ambaye alitambulika kwa jina maarufu la Bi Mtumwa. Alizaa naye watoto wanne ambao ni Said, Abdul-Rahman, Khadija, pamoja na Fatma. Mohamed (2011) anaeleza ya kwamba, Abdulrahman alikuwa mtundu wa kuchokora redio na aliwahi kuwa fundi mitambo katika sauti ya Zanzibar. Pia, amewahi kuwa mwimbaji wa nyimbo za Kiarabu za Abdulhalim Hafidh katika kikundi cha Akhwan Safah. Mabinti wawili (Khadija na Fatma) walikuwa mahodari sana skuli na waliwahi kushiriki katika mitihani ya *Cambridge School Certificate*. Katika mitihani hiyo walifaulu lakini walifariki pamoja na mama yao wakati wa mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 kabla ya matokeo kutangazwa.

Kulingana na utafiti uliofanywa, inaonekana kuwa kuna madai matatu yenye kueleza asili ya lugha yake kadri alivyotumia katika bunilizi zake. Madai hayo ni:

- (a) Kuna wanaodai kuwa alikuwa akitumia lahaja ya Kiunguja mjini kwa kuwa alizaliwa na kukulia mjini;
- (b) Wengine wanadai kwamba, mjini watu huhamia tu, asili yao hasa ni kutoka shamba (vijijini). Hivyo, mtunzi huyu asili yake ni Kusini Unguja. Dai hili linatilia mkazo lahaja ya Kiunguja mjini lakini lahaja nyingine kama Kimakunduchi kwa vile ni mtu wa Kusini alikuwa anajua. Na kwa kuwa alikuwa ni mtukutu wa kuchunguza mambo, hata Kitumbatu na Kipemba akizifahamu, na;
- (c) Wengine wanadai kuwa mtunzi huyu ni Mngazija lakini amezaliwa na kukulia Zanzibar. Hivyo, Kiunguja mjini ni lahaja yake; na Kingazija ni lugha yake mama.

Madai yote yana ukweli ndani yake kwani hakuna linalopinga kuwa Muhammed Said Abdulla ni mzaliwa wa mjini Unguja ingawa asili yake hasa bado ina mushkeli. Pia, lugha yake wote wameikubali lahaja ya Kiunguja mjini.

Mjawiri (ameshatajwa) anaeleza kuhusu elimu na kazi za mtunzi huyu. Anasema kwamba, alianza elimu ya msingi mwaka 1928 baada ya kuanza kusoma Qur'an katika madrasa ya mwalimu Saleh bin Ali. Mwaka 1938 aliendelea na elimu ya sekondari na alipomaliza alikuwa ofisa wa afya mpaka mwaka 1958. Baada ya kuachishwa kazi hiyo alifanya kazi katika gazeti la *Mkulima* kama mhariri. Ilipofika mwaka 1968 aliachishwa tena kazi lakini hakukata tamaa. Aliendelea kutafuta tena kazi na alibahatika kuwa mtayarishaji wa kipindi cha "Sadiki Ukipenda" katika redio ya "Sauti ya Unguja". Pamoja na majukumu mengi aliyokuwa nayo, pia alikuwa ni mwanafasihi anayetambulika. Alikuwa ni maarufu katika uga wa riwaya za kipelelezi. Kazi zake zilizohibitika ni *Mzimu wa Watu wa Kale* (1958), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani Kuna Watu* (1973), *Siri ya Sifuri* (1974), *Mke Mmoja*

Waume Watatu (1975), *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976), *Kosa la Bwana Msa* (1984) na hadithi fupi, "Mke Wangu". Muhammed Said Abdulla alijiegemeza katika uga huo wa upelelezi kutokana na sababu tano alizozieleza Mjawiri kupitia *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdulla (Bwana MSA)* katika kurasa 112 - 113. Nazo ni:

- a) Ameingia katika uandishi huo kutokana na athari ya kazi za Sherlock Holmes. Kwa kuwa alikuwa msomaji na mshabiki wa kazi hizo basi alipotaka kuandika alishitukia ameingia katika uga huo.
- b) Ameingia katika dhamira hiyo na mtindo huo kwa sababu hakupenda kugusia mambo nyeti ambayo yangeudhi tabaka tawala na kuhatarisha usalama wake. Alitaka aishi maisha ya kutokwaruzana na utawala.
- c) Hakupenda kugusia jambo jengine lolote kwa kuhofia kupata kiwewe kwa yaliyopita wakati wa Mapinduzi. Hivyo njia pekee ya kujidhibiti na kujikinga na kujiliwaza aliona ni kuogelea katika bahari ya riwaya za upelelezi ambazo yeye mwenyewe alipenda kuziita hadithi za kadhia.
- d) Inawezekana kwamba uzoefu wake na hata elimu yake juu ya masuala mengine ya jamii haikuwa ya kiwango cha juu. Hivyo asingeweza kuogelea kwa mapana na marefu katika masuala kama vile uchumi, ukombozi, haki za binadamu na demokrasia. Kwa kweli msanii mahiri huandika mambo anayoyafahamu kwa undani kuliko kuchupia mambo kijuujuu na hatimaye kufedhehesha sanaa yake.
- e) Ameandika katika utanzu huu kwa sababu amehisi na kugundua kuwa fani ya upelelezi katika jamii iko katika kiwango cha chini na kupelekea kutiwa hatiani watu wasiokuwa na hatia. Kwa mujibu wa maelezo yake, upelelezi unahitajia zaidi kipaji ambacho hujaaliwa nacho wateule wachache katika jamii. Iwapo upelelezi utaendeshwa na watu walio na kiwango cha chini cha kipaji huwa ndiyo chanzo cha fitina.

Mohamed (ameshatajwa) anaeleza kuwa, uandishi wake uliathiriwa na mazingira aliyokuwa akiishi. Athari hiyo imebainisha sifa ya mabadiliko ya utamaduni uliovukuta vuguvugu la upeo wa dini na dunia inayoturejesha nyuma tulikotoka. Hali hii ilimjenga sana mtunzi huyu kuwa gwiji wa uandishi. Vitabu vilivyompatia tunzo ni *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Kisima cha Giningi*. Riwaya zake ni riwaya pendwa za kihalifu na kipelelezi zenye mtindo wa sanjari, ambapo wahusika

muhimu walikuwa watatu; polisi (Inspekta Seif), mpelelezi wa kujitegemea (Bwana Msa) na rafiki wa mpelelezi (Najum).

Katika uumbaji wa wahusika; hali ya Inspekta Seif na Najum kuwa mbumbumbu mbele ya Bwana Musa imewekwa bayana na Madumulla (2009). Madumulla anaeleza kuwa, mtunzi huyu ameathiriwa na mtunzi wa Kiingereza, Arthur Conan Doyle¹ ambaye alikuwa gwiji wa vitabu vya uhalifu na upelelezi. Mtunzi huyu alikuwa akiwatumia wahusika wakuu watatu: Polisi, Sherlock Holmes na Watson. Naye Sumary (2013), katika kuchunguza maandishi mengine ya mtunzi huyu, anaeleza kuwa mwandishi huyu alikufa akiwa kaacha insha tatu. Insha hizo ni *Bwawani Hoteli, Utukufu wa Funguni na Mchuchu si Mchumba*.

1.8 Nadharia ya Uchanganuzi wa Data

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya Uhalisia. Kwa mujibu wa Njogu na Wafula (2007), dhana ya uhalisia imehusishwa na miktadha miwili. Kwanza, uhalisia kama njia ya kutathmini hali au halia (uhalisia wa maisha). Pili, uhalisia wa kifasihi unaoashiria uwezo wa kusawiri au kuelezea hali kwa kuzingatia uyakinifu au uhakiki wa maisha. Maana hii ndiyo iliyotumiwa huko Ufaransa na waandishi kama vile Flaubert² (1850) kwa kuelezea kazi ya sanaa inayoonesha maisha ya binadamu jinsi yalivyo. Uhalisia unahusu uigaji wa mazingira anamopatikana mwanadamu. Katika

¹ Arthur Conan Doyle (1859 - 1930) alikuwa ni mwandishi na mtabibu wa Kiskochi (*Scottish*) ambaye alijulikana sana kwa hadithi za kubuni zinazozungumzia uhalifu kupitia mpelelezi wa kubuni Sherlock Holmes. Kazi zake nyingine zilihusu masuala kadhaa kama hadithi za kubuni za Kisayansi, tamthilia, ushairi, mapenzi, historia na kazi nyingine ambazo si za kubuni (*Wikipedia The Free Encyclopedia*).

² Gustave Flaubert (1821 - 1880) alikuwa mwanafasihi mashuhuri wa Ufaransa aliyetoa athari kutokana na umahiri wa kutumia sana uhalisia wa nchi yake. Riwaya yake ya mwanzo na iliyompatia umashuhuri mkubwa ni *Madame Bovary* (1857) ambayo ilijikita katika mfumo wa uhalisia na ujumi (*Wikipedia The Free Encyclopedia*).

kitabu chake kiitwacho *Aesthetics*, mwanafalsafa Hegel³ alilitumia neno uhalisia kumaanisha kazi ya sanaa iliyo na wahusika ambao matendo yao yanachochea na hali ya kisaikolojia iliyowazunguka.

Nadharia hii ilianza karne ya 19 barani Ulaya kama njia ya kuonesha hisia za kisiasa na kiuchumi iliyochangiwa sana na fikra za Karl Marx⁴. Kimsingi, nadharia hii inaichukulia kwa undani kazi ya fasihi na somo la fasihi kama matokezo ya kijamii na kiuchumi. Kazi ya fasihi ni mfano ambao unaonesha hali halisi iliyomo katika jamii na kuleta mabadiliko pale panapohitajika. Wanauhalisia wanaichukulia fasihi kama historia. Kwao, riwaya, ushairi na tamthiliya zinaweza kuhakikiwa vizuri iwapo zitahusishwa na matokeo yanayojitokeza katika jamii ambayo ni ya kisiasa, kiuchumi pamoja na mfumo wao wa maisha. Wanaiita nadharia hii Uyakinifu pembuzi unaotokana na lugha (Mushengyezi, 2003).

Kwa mujibu wa Njogu na Wafula (2007:63), nadharia ya uhalisia imediriki kuhusishwa na mikondo mitatu ambayo ni:

(i) Ni mwelekeo:

- a) Unaozingatia njia ya Kisayansi ya kutekeleza jambo.
- b) Unaosisitiza upinzani dhidi ya mtazamo wa kinjozi juu ya maisha.
- c) Unaopingana na ulimbwende.

(ii) Ni mbinu ya kisanii:

- a) Ambayo ni ya kujaribia
- b) Iliyo na mashiko katika hali ya maisha ya watu.
- c) Yenye kuonesha hali ya kisaikolojia ya wahusika ambao msomaji anakumbana nao.

³ Georg Wilhelm Friedrich Hegel (1770 - 1831) alikuwa ni mwanafalsafa wa Kijarumani. Aliendeleza na kuelezea mtindo wa kutumia vijilugha ambao ndani yake hupatikana muendelezo wa matukio ya kihistoria (*Encyclopedia Britannica*).

⁴ Karl Marx (1818 - 1883) alikuwa ni mwananadharia muhimu wa nadharia inayohusu masuala ya kijamii. Hakuwa mtaalamu wa falsafa ingawa alihitimu Shahada ya Udaktari wa Filosofia. Maisha yake yalijikita katika shughuli za kisiasa, uanahabari, uhistoria na uchumi. Uanasiasa wake uliangukia katika bunilizi za kimapenzi na kazi zake za mwanzo zilijengeka katika dhana ya uhalisia kutokana na mwamko wa mabadiliko wa binadamu ambao walipigania kuwa huru. Hayo yalionekana kupitia fikra za Hegel ambazo zimemfanya Marx kujifanisha na vijana wa Kihegel (Michael Rosen, Harvard University 1998 through *Encyclopedia of Philosophy*).

(iii) Ni mbinu ya kuhakiki inayozingatia:

- a) Muundo na muwala katika kazi ya fasihi.
- b) Uchambuzi wa kazi ya sanaa kama zao linalojitosheleza.
- c) Hali halisi ya wahusika na lugha wanayoitumia.
- d) Inayoainisha vielelezo vya kihistoria vinavyosababisha mabadiliko makubwa ya kijamii kama anavyosema Lukacs⁵.

Wahusika na wahakiki waliotumia nadharia hii waliamini ya kwamba, dhima ya mwandishi ni kuonesha ukweli jinsi ulivyo. Mhakiki naye alimtathmini mwandishi kwa namna ambavyo alijibidiisha kuonesha ukweli katika jamii. Haja kuu ya utunzi ni kuonesha picha ya mazingira ambamo, jamii inapatikana na ndiyo maana dhana ya fasihi 'ni kioo cha jamii' ilitokana na nadharia hii.

Mkondo wa mwisho kati ya ile mikondo mitatu iliyobainishwa na Njogu na Wafula (2007) ndiyo uliyotumiwa. Mkondo wenyewe ni mbinu ya kuhakiki inayozingatia: muundo na muwala wa kazi ya fasihi, hali halisi ya wahusika na lugha wanayotumia, na vielelezo vya kihistoria vinavyosababisha mabadiliko makubwa ya kijamii kama vile lugha. Utafiti ulitumia misingi hiyo kwa kuchunguza lugha waliyobebeshwa wahusika katika riwaya teule na hali halisi ya mabadiliko ya lugha hiyo kulingana na nyakati ambazo riwaya hizo zilitungwa. Lengo na matarajio ya uchunguzi huo ni kupata msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari na etimolojia ya msamiati huo katika riwaya teule za Muhammed Said Abdulla. Uchunguzi huo ulihusisha wadau wa fasihi na wazee waliomo katika jamii pamoja na mawazo ya mtafiti kupitia maandishi mbalimbali ili kupata kitu kizuri kinachofaa.

⁵ Georg Lukacs (1885 - 1971) alikuwa ni mwananadharia na mmoja wa waanzilishi wa nadharia ya Umarx wa Kimagharibi. Alijulikana kupitia maandishi yake yaliyohusu nadharia za fasihi zinazozungumzia ujumi na Umarx. Kitabu chake cha *'The Theory of the Novel'* cha 1916 na cha *'History and Class Consciousness'* cha 1923 ni miongoni mwa kazi zake zilizosomwa sana na kumpatia umaarufu mkubwa mpaka zama hizi (*Stanford Encyclopedia of Philosophy*, 2013).

1.9 Mipaka ya Utafiti

Utafiti huu ulihusu lugha. Kwa kuwa lugha ina uwanja mpana, uchunguzi ulijikita katika kipengele cha matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla.

1.10 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Kikwazo kikubwa cha utafiti huu ni gharama zilizotumika katika kuifanya kazi hii hadi kukamilika kwake. Katika kutatua kikwazo hicho, ilimbidi mtafiti kuomba mkopo ambao angalau ulisaidia kusogeza mbele gurudumu hili.

1.11 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura hii imeeleza mambo ya msingi kuhusu mchakato wa utafiti. Hii ni sura iliyotoa mwanga kuhusu utendekaji wa mchakato mzima wa kazi na kutengeneza njia ya kupita ili kufikia kilele. Imeweka bayana dhana za msingi zilizojitokeza katika utafiti huu, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la utafiti, malengo ya utafiti, maswali na umuhimu wa utafiti. Aidha, imeeleza historia ya mwandishi teule, Muhammed Said Abdulla kwa kugusia kipengele cha asili na uzao wake, familia yake, na kazi zake nje na ndani ya fasihi. Nadharia ya utafiti ni kipengele kingine kilichojadiliwa katika sura hii ili kuweka bayana mweka mkuu wa mchakato huu. Nadharia iliyoelezwa ni Nadharia ya Uhalisia. Baada ya hapo, kulifuata kipengele cha mipaka ya utafiti na kumalizia kwa vikwazo vya utafiti na utatuzi wake ili kuonesha changamoto zilizomkabili mtafiti na namna ambayo alizitatua changamoto hizo. Sura inayofuata inajadili mapitio ya maandiko mbalimbali yahasuyo mada hii ili kubaini mapengo ambayo yanapaswa kuzibwa na uchunguzi huu.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO

2.1 Utangulizi

Sura hii inabainisha maandiko mbalimbali yanayohusiana na mada hii kwa namna moja au nyingine. Inajumuisha mapitio ya maandiko kuhusu matumizi ya lugha kwa ujumla na mapitio ya maandiko kuhusu kazi za Muhammed Said Abdulla. Baada ya kuonesha maandiko hayo, sura hii imekamilishwa na sehemu inayoeleza mapengo yanayopaswa kuzibwa na muhtasari wa sura.

2.2 Maandiko Kuhusu Matumizi ya Lugha kwa Ujumla

BBC SWAHILI (2012) wanaeleza kwamba, katika sehemu nyingi duniani wanahabari wanaaminika kwa yale wanayosema hewani ama katika makala wanazoandika. Wananchi pia huamini kuwa maneno wanayotumia wanahabari ni sanifu. Lakini je, matumizi ya msamiati usiofahamika kwa watu wengi yana manufaa gani katika jamii? Ni dhahiri kuwa mojawapo ya sifa kuu ya lugha ni kukua na kubadilika; lakini makuzi na mabadiliko hayo hayatakiwi kutatiza mawasiliano baina ya wahusika. Hii ina maana ya kwamba, haitoshi watu kuelewa visawe vya maneno mengine ya Kiswahili pasi na kujua jinsi ya kuvitumia. Kwa mfano, yatumikapo maneno kama 'shangazi', 'heshima' na 'mzee' yataeleweka kwa urahisi kuliko 'mbiomba', 'mbeko' na 'shaibu'. Aidha, nchini Kenya watangazaji wengi wamekuwa wakitumia neno 'ghushi' badala ya 'bandia'. Ni dhana zinazokaribiana ila kwa maoni yaliyotolewa katika makala hiyo, 'bandia' litaeleweka kwa urahisi. Kwa hivyo, huu msamiati unaotumiwa katika lugha ya Kiswahili unaweza kuwa ni hatari kwa usalama wa lugha yenyewe. Makala hii ilitoa mwanga juu ya uteuzi wa msamiati unaoeleweka kwa hadhira, ukuaji na ubadilikaji wa lugha, na wakati huo huo,

ilituachia swali la kujiuliza. Kwamba, je, msamiati alioutumia Muhammed Said Abdulla katika riwaya zake umebadilika? Na je, mahali ambamo ameutumia mnafaa?

Kantangayo (2011) anaeleza kuwa lugha na sanaa ni vipengele muhimu vya utamaduni wa jamii yoyote. Mtu anaweza kutambulika popote kwa kuzungumza au kwa sanaa yake kama vile ngoma, nyimbo na kadhalika. Mathalani, sanaa za majukwaani haziwezi kuvutia, kufikisha ujumbe, kuburudisha wala kuonya kama matumizi ya nyenzo kuu (lugha) haikutumika vizuri. Ili sanaa iweze kukidhi haja ya hadhira, lazima wawasilishaji wawe mahiri katika kuitumia lugha. Umahiri huo hujitokeza katika matumizi ya lugha fasaha yenye kujumuisha sarufi, muundo na vionjo muhimu. Mfano wa vionjo hivyo ni kama tamathali za semi, nahau, methali na misemo. Vionjo hivyo vina uwezo mkubwa wa kuisitiza, kushawishi na kueleza kwa usahihi kile kilichokusudiwa pasipo kuwa na mlolongo wa maneno mengi. Kazi hii imeweka wazi utambulisho wa mtu kupitia sanaa yake, hivyo ilisaidia katika utafiti huu kwa kuonesha njia za kumtambua Muhammed Said Abdulla kupitia matumizi ya msamiati katika riwaya zake.

Kiango (2004) ametoa ufafanuzi juu ya uundaji wa msamiati katika kukidhi azma ya lugha ya Kiswahili. Ameeleza kuwa msingi mkubwa ni mabadiliko ya sera ya lugha Kitaifa kama yalivyojitokeza wakati wa mkoloni na baada ya uhuru. Anasisitiza kuwa kasi imepanda wakati huu wa utandawazi ambapo mawasiliano hasa ya kompyuta yamekuwa ndio mweka mkuu. Hadhi hii imesababisha kukikuta Kiswahili kimetupwa mkono na maendeleo. Pia, ni muhimu kujitosheleza katika kukidhi haja za mawasiliano kwa lahaja zote za taifa. Hii ina maana kwamba lahaja zote nchini ni muhimu zitajike kwa Kiswahili sanifu. Kwani, si jambo la ajabu kukuta lahaja fulani

haina msamiati wa Kiswahili au kuchanganya Kiswahili na maneno ya kilahaja wakati wa mazungumzo. Kazi hii iliiweka wazi dhana ya etimolojia ya msamiati kulingana na mfumo wa lugha kiwakati. Hivyo, ilitoa changamoto ya kuchunguza etimolojia ya msamiati katika riwaya za Muhammed Said Abdulla kwa kuhusisha na wakati ambapo riwaya hizo zilitungwa.

Ntarangwi (2004) na Gibbe (1990) wanasisitiza kuwa lugha ndicho kiungo kinachowaunganisha mhakiki na mtunzi. Ni kupitia lugha aitumiayo mtunzi ndipo mhakiki hufahamu anamlenga nani, kwa lengo gani, na kwa kuzingatia nini. Bila ya lugha hakuna maudhui yatakayopatikana na wala uchambuzi utakaofanyika. Kazi hizi zilisaidia katika utafiti huu kwa kuibua shabaha ya Muhammed Said Abdulla juu ya kutumia msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya zake.

2.3 Maandiko Kuhusu Kazi za Muhammed Said Abdulla

Sumary (2013), Mkawe (2011), Ahrenberg (1984) na Mgeni (1983) wamechunguza suala la upelelezi katika riwaya za Muhammed Said Abdulla. Wanaeleza ya kwamba, mwandishi huyu amejadili suala hilo kupitia vipengele mbalimbali katika jamii kama vile urithi, dhulma, mapenzi, ndoa, elimu na kifo. Mambo hayo yametuzunguka katika maisha yetu ya kila siku. Hivyo, watafiti hawa wameona kuwa upo umuhimu wa kutosha wa kuyachunguza na kuyabainisha matukio hayo kama ambavyo riwaya hizo zilivyoonesha. Pia, kuyasawiri kwa dhati na mfumo halisi wa maisha ya watu ya kila siku. Wakilitolea mfano suala hilo kupitia riwaya tofauti za Muhammed Said Abdulla, wanamuelezea mhusika Bwana Msa aliyekuwa akifanya kazi ya upelelezi kuliko askari wenyewe. Wanasema ya kwamba, mhusika huyo alikuwa akitumia elimu ya saikolojia na mbinu za kisayansi kuagua tatizo lilivyokuwa, jambo ambalo askari na watu wengine kupigwa na butwaa. Kwa mfano katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, wakati Bwana Msa anachunguza muuaji

wa Bwana Ali. Alibaini kuwa Baniani si muuaji kwa elimu yake aliyoitumia. Aliangalia hali ya uzee na afya aliyonayo Baniani na kulinganisha na jinsi kifo chenyewe kilivyotokezea. Muhammed Said Abdulla amemtumia mhusika huyo si tu kumpa elimu ya kizungu lakini hata busara ya Waswahili. Alimuandalia kitabu alichokuwa anatumia kiitwacho 'Kinyume cha Mambo'. Kitabu hicho hudaiwa kuwa mambo yote yamegeuzwa juu chini, chini juu. Lakini Bwana Msa alikuwa anakisoma mara kwa mara bila ya wahusika wengine kubaini anachokisoma. Tafiti hizi zimeweka bayana busara na hekima walizonazo Waswahili kupitia mhusika wake Bwana Msa. Lakini zilituachia swali la kujiuliza, je, lugha iliyotumika nayo ni bayana kwa Waswahili?

Sanga (2012) ametafiti ujumi katika riwaya pendwa ya Kiswahili kwa kutumia mifano kutoka riwaya za Muhammed Said Abdulla na Aristabulus Elvis Musiba. Kazi hii inaeleza ujumi kupitia vipengele mbalimbali kama ujumi katika mguso au hisi, idili za jamii na makusudio ya kitu. Alieleza ujumi katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* unavyohusiana na idili za jamii ya Watanzania kupitia matukio mbalimbali yanayoakisi maisha yao miaka ya 1980. Alitoa mfano wa tukio la kuuu kupitia mhusika Joka na Shoka kuwa haliendani na idili za jamii hasa kwa upande wa Tanzania visiwani; mijini na vijijini. Pia, kitendo cha kubadili jina Seyyid Ahmed katika ndoa kati yake na Jamila. Ni ujumi unaohusiana na watu wa Unguja miaka ya 1980. Hii ni kwa sababu ya ubaguzi wa rangi na kabila unaotokana na koo za kifalme zilizotawala Zanzibar kabla ya Mapinduzi. Ama kwa upande wa riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, ameeleza uhusiano wa kiujumi na idili za jamii kwa miaka ya 1940. Amegusia kionjo cha utamaduni na mazingira ya jamii ya Kizanzibari juu ya wenyeji kwa Waarabu. Desturi ya wenyeji wa Zanzibar ni

kukubali chochote ambacho kinatokana na Waarabu. Ametoa mfano wa Inspekta Sefu wa kukiiga Kiswahili kibovu cha Baniani na kujionea fahari anapozungumza wakati ni makosa. Pia, masuala ya itikadi yalithaminiwa sana miaka hiyo. Hii inaonekana kupitia mama Kipwerere alipokuwa akimpeleka binti yake kwa mganga kwa sababu ya kusibikwa na shetani.

Naye Issa (2011) katika kuchunguza taswira ya mwanamke kupitia riwaya hizo anaeleza kwamba, masuala ya mila na itikadi yapo sana kwa wanawake. Sambamba na tendo la mama Kipwerere, pia Kipwerere mwenyewe alipopanda shetani na kuagua kupotea kwa mumewe; Bwana Ali. Aidha, ametoa mfano katika *Kisima cha Giningi* kupitia mhusika Mwana wa Ginigi. Anaeleza kuwa mama huyu alimtuhumu mumewe, Vuai kuwa katumia uramali ili amnyang'anye mali yake. Hatimaye, kachukuwa hatua ya kumfukuza mumewe kwa dhana ambayo haina ithibati. Kazi hizi zimetoa dira ya kuwapo kwa wazo la utafiti huu. Zimeonesha usawiri wa kiujumi na taswira ya mwanamke katika riwaya za Muhammed Said Abdulla kwa jamii ya Wazanzibari kupitia kipengele cha idili za jamii lakini zilishindwa kugusia kipengele cha lugha. Mwanaya huo umezibwa na utafiti huu kwa kujadili matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari kupitia riwaya hizo.

Mdowe (2011) anaelezea falsafa ya Muhammed Said Abdulla jinsi ilivyozama katika utamaduni wa Kizanzibari na utamaduni wa jamii ya Waswahili kwa ujumla. Anaeleza kwamba, katika kazi zake tunakuta kuwa yamejitokeza mawazo makuu ya kifalsafa ambayo moja kwa moja yamefungamana na utamaduni wa Kizanzibari. Mawazo yenyewe ni mapenzi na ndoa, malezi na makuzi, uaminifu, urafiki, siasa, uwezo, imani na itikadi za kijadi, dini, uongozi, maisha na kifo, lugha, kukosea na uzalendo. Mawazo hayo ameyajadili kwa kuiangalia jamii yake katika falsafa ya

tambo aliloliita kinyume cha mambo lenye kusimamia mambo sivyo yalivyo. Katika kuchambua falsafa hiyo kupitia kipengele cha lugha alisema, mtunzi huyu ameibua misemo inayoendana na hali ya utamaduni wa Mzanzibari juu ya kutawaliwa. Pia, kutetea matumizi mazuri ya lugha na kulaani matumizi mabaya yanayofanywa na Waswahili wenyewe. Akitoa mfano wa hilo, alimtumia mhusika wake Bwana Musa, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* aliposema:

Nitatumia Kiswahili changu mwenyewe, sitaiga Kiswahili cha Kibaniyani. Ajabu kubwa hii iliyomo humu mwetu. Mtu maadam atakuwa anasema na Baniyani kwa Kiswahili, atajilazimisha na yeye aseme Kiswahili kwa namna anavyosema Baniyani, ingawa anajua kuwa vile anavyosema yule Baniyani si Kiswahili safi, na vile kumuiga anaharibu lugha yake (uk. 63).

Nukuu hiyo inaonesha tabia ya Waswahili iliyokuwepo miaka ya nyuma. Mwandishi alimtumia mhusika Inspekta Sefu kuonesha tabia ya kuwaiga Mabaniani na Wamanga kisha Bwana Musa kutoa dosari ya wigo huo, kama ambavyo jamii ya leo watu hawaridhiki kama hawajachanganya Kiswahili na Kiingereza. Hii ilitokana na kuitaka jamii ielewe hatari ya jambo hilo. Ingawa kazi hii ilitoa mwanga juu ya utafiti huu, bado ilitupa changamoto ya kutaka kujua hicho Kiswahili chake mwenyewe alichokitumia ni kipi? na je, kinasawiri mazingira ya Mzanzibari kwa ujumla?

Sengo (2011) alichunguza kipengele cha mandhari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla. Alihusisha riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, *Duniani Kuna Watu* na *Kosa la Bwana Msa*. Alitoa mfano kipengele cha lugha waliyobebeshwa wahusika kama ni usawiri wa mandhari halisi ya jamii ya Wazanzibari. Anaeleza kuwa, Muhammed Said Abdulla ni upande wa pili wa Shaaban bin Ufukwe katika fasihi ya Uswahilini-Upwa wa Afrika Mashariki. Kama wangepambanishwa, kusimama pamoja kuanzia pamoja katika jambo moja, mbio hizo za kukiandikia kitu

hicho zingewapa taabu majaji juu ya yupi wamtangulize. Kazi zake zina utajiri wa maneno ya hekima yenye kueleza kitu kikaonekana machoni. Kwa mfano, 'Ukitaka kujua asili ya mwangaza ingia kizani', 'Shibe kamwamini njaa, njaa alikiangamiza chakula chote tumboni mwake', 'Kuzinduwa ni kuzingua', yaani raha ya msomi, taabu ya asiyesoma. Kazi hii imedokeza tu kwamba Muhammed Said Abdulla ni mwanafasihi wa Uswahilini bila ya kubainisha vipengele vinavyomtambulisha. Hivyo, katika kumtambulisha mtunzi huyo, utafiti huu ulichunguza kuhusu matumizi ya msamiati katika riwaya zake na namna yalivyowaathiri wasomaji.

Rashid (2011) alichunguza kipengele cha wahusika kupitia lugha ambayo wamebebishwa wahusika hao katika riwaya za Muhammed Said Abdulla. Anaeleza kuwa, mwandishi amewavisha wahusika lugha na majina yanayoweza kuleta picha ya utabaka katika jamii kabla ya Mapinduzi (1964). Mfano wa wahusika hao ni kama vile Sikudhani na Twajuana wa *Mwana wa Yungi Hulewa*, Masanja na Kurwa wa *Mzimu wa watu wa Kale*, pamoja na Safinia na Siajabu wa *Kosa la Bwana Msa*. Wahusika hao wanabainisha majina na lugha ya watu wa tabaka la chini (tabaka la wanyonge) ambao ni vijakazi na watwana. Hawa aliwajenga kuwa wanamilikiwa na akina Seyyid Ahmed bin Soud wa *Kosa la Bwana Msa*, Hakimu Marjani wa *Duniani Kuna Watu*, Bishali na Soarez wa *Mwana wa Yungi Hulewa* na Bwana Ali Bin Bomani wa *Mzimu wa Watu wa Kale* ambao ni tabaka la juu. Ijapokuwa maelezo haya yaliishia kudokeza kuwa dhana ya lugha na majina ya wahusika yalitumika kiutabaka kabla ya (1964), ilisaidia wakati wa kuchambua msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya hizo.

Salim (2011) alichunguza mafunzo na ujumbe unaopatikana katika riwaya za Muhammed Said Abdulla. Anaeleza kuwa, mwandishi huyu ametoa mwelekeo

wenye kufunza tabia njema, hususani katika mambo ya kijamii na kiutamaduni. Kwa kuwa jamii hulelewa ndani ya utamaduni fulani, basi mwandishi huyu ametoa ujumbe na mafunzo kupitia mambo yanayofungamana na silka za kijamii na utamaduni. Ujumbe huo ulitokana na vipengele vya mapenzi na ndoa, elimu, umuhimu wa kujifunza historia, malezi, hadhari katika maisha, ubahili na ubaya wake katika jamii, tamaa, umuhimu wa kutunza kumbukumbu, na umuhimu wa uchunguzi na upelelezi. Pamoja na kuwa kazi hii imeweka bayana mafunzo na ujumbe unaokwenda sambamba na jamii ya watu wa visiwani, lakini je, lugha iliyotumika inashabihiana na utolewaji wa mafunzo hayo? Pengo hilo limewekwa bayana na utafiti huu ili kuziweka kazi za Muhammed Said Abdulla katika mustakbali mzuri na jamii andikiwa.

Hamad (2011) alichunguza matumizi ya lugha kupitia riwaya za Muhammed Said Abdulla. Anaeleza ya kuwa, mwandishi ameifinyanga na kuisanifu lugha apendavyo. Ametumia visawe vinavyofanana na kukaribiana kimaana, mafumbo, Kiswahili cha kikabila, lugha katika shughuli maalumu, uteuzi wa maneno na usambamba pamoja na matumizi ya lugha kwa misingi ya kimuktadha. Alidondoa matukio mbalimbali kupitia riwaya za mtunzi huyo kwa ajili ya kutoa ushahidi. Kwa mfano, Kiswahili cha kikabila kupitia mhusika Mmanga na Baniani ambao wakizungumza kwa athari ya lugha zao za awali katika *Mzimu wa Watu wa Kale*. Pia, lugha katika shughuli maalumu kwenye mchezo wa karata katika *Duniani Kuna Watu*. Aidha, lugha ya mfumo wa Kimwinyi kati ya Bi Shinuna na mjakazi wake, Tunu, katika *Kosa la Bwana Msa*. Vilevile, katika kuchunguza maneno na usambamba wake, alitumia mhusika Bwana Hakim alipokuwa akimueleza mwanawe Kasim katika *Duniani Kuna Watu*. Maneno yenye kutolewa kinyume chake katika sentensi moja na ya

mafumbo yenye mzunguko kiasi ambacho inakuwa vigumu kufahamu, ametumia mfano katika *Mzimu wa Watu wa Kale* na *Mwana wa Yungi Hulewa*. Hata hivyo, amebainisha visawe vinavyofanana na kukaribiana kimaana katika *Duniani Kuna Watu* ukurasa wa 3, pale Bwana Hakim alipokuwa akijitoharisha. Anaeleza "...anarudi msalani ambako kulikuwa na faragha ya mambo yote yanayohusu kujikosha, kujisafisha, kujinadhifisha, kujitoharisha na kusali".

Sambamba na hilo, Rweyemamu (2013) katika kulinganisha ufundi wa Muhammed Said Abdulla na Katalambula aligusia kipengele cha mtindo. Mtindo huo aliujadili kupitia matumizi ya lugha (kama vile tashbiha, tashhisi, tauria, tasfida, methali, mafumbo na misemo), matumizi ya lugha ya picha na matumizi ya lugha ya ishara. Tafiti hizo zimetubainishia matumizi ya lugha kwa namna mtunzi alivyoweza. Lakini lugha hizo zilishindwa kufafanuliwa vipi zilisawiri mazingira ya Kizanzibari kama ndio mandhari halisi ya riwaya hizo.

2.4 Mapengo Yanayopaswa Kuzibwa

Jitihada kubwa iliyofanywa na wataalamu hao katika vipengele mbalimbali ni toshelevu kwa malengo yao waliyoyakusudia. Licha ya hayo, bado kuna mapengo yanayojitokeza. Mosi, kutochunguzwa usawiri wa kipengele cha lugha (msamiati) na jamii andikiwa. Pili, kutofafanuliwa athari ambazo wasomaji huzipata kutokana na usawiri huo wa lugha na jamii hiyo. Muhammed Said Abdulla ameweza kuifinyanga lugha kwa namna ambayo mara nyingine inaweza kuwa fiche kwa baadhi ya wasomaji. Hii hutokana na baadhi ya msamiati katika riwaya zake ukiwa na historia na asili ya lahaja zilizokuwa zikitumika Zanzibar kabla ya kuwapo kwa lugha moja inayotumika kwa watu wote. Kutokana na sababu hiyo, utafiti huu ulikusudia kuziba mianya hiyo kwa kujiegemeza katika nadharia ya uhalisia. Lengo ni kuchunguza matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari. Utafiti umetumia

riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale, Duniani Kuna Watu na Kosa la Bwana Msa* katika kubainisha etimolojia ya msamiati huo na kueleza athari yake kwa wasomaji.

2.5 Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura hii imebainisha maandiko mbalimbali yanayoendana na mada. Lengo ni kuweka bayana dhana zilizomo katika mada inayochunguzwa. Aidha, kuonesha maandiko hayo yalivyosaidia katika uchunguzi huu pamoja na kubainisha mapengo yaliyoachwa. Kazi hiyo ilifanyika kwa minajili ya kuonesha namna kazi hii ilivyoweza kuyaziba mapengo hayo ili kuondoa changamoto kwa wasomaji, watafiti na wahakiki wa riwaya hizo. Baada ya kubainisha hayo, sasa tuingie katika sura ya tatu ambayo inajadili usanifu na mbinu za utafiti huu.

SURA YA TATU

USANIFU NA MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Sura hii inaweka wazi kuhusu usanifu na mbinu ambazo zilitumika katika mchakato mzima wa utafiti huu. Ni sura inayoweka wazi vipengele kama vile mpango wa utafiti, eneo la utafiti, walengwa wa utafiti ikiwa ni jamii tafitiwa na sampuli yao, ukusanyaji wa data zikiwemo njia na zana pamoja na mchakato wa ukusanyaji, uchanganuzi wa data, uhalali na uthabiti wa matokeo ya utafiti, itikeli za utafiti pamoja na muhtasari wa sura.

3.2 Mpango wa Utafiti

Utafiti huu ulikusanya data maktabani na uwandani. Data zilizopatikana maktabani zilihusu maana na asili za msamiati kupitia makamusi mbalimbali, riwaya teule za Muhammed Said Abdulla, tasnifu, makala na vitabu mbalimbali vilivyoelezwa kuhusu mtunzi huyo. Aidha, data za uwandani ziliwashirikisha wenyeji wa Zanzibar, wakiwemo wahadhiri wa vyuo, wanafunzi na wakazi wengine. Zilihusu matukio yenye msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari kupitia riwaya hizo pamoja na athari inayopatikana kwa wasomaji wake. Mwelekeo wa utafiti huu ni wa kiufafanuzi ambao haukujihusisha na taarifa zozote za kitakwimu. Hivyo, ukusanyaji, uchanganuzi na uwasilishaji wa data ulikuwa ni wa kitaamuli ambao ulitumia mbinu ya maelezo.

3.3 Eneo la Utafiti

Utafiti huu ulifanyika Zanzibar, Mkoa wa Mjini Magharibi kwa kuhusisha maeneo ya maktaba iliyopo Baraza la Kiswahili Zanzibar na Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Mkoa wa Mjini Magharibi ni eneo lililochaguliwa kufanyia uchunguzi

kwa sababu ndiyo sehemu aliyozaliwa na kuishi mwandishi teule na ni sehemu rahisi ya kupata huduma za kimaktaba. Aidha, utafiti huu ulifanyika Chuo Kikuu cha Dodoma kwa matumizi ya maktaba.

3.4 Walengwa wa Utafiti

3.4.1 Jamii Tafitiwa

Utafiti huu ulitumia jamii ya Wazanzibari kuhusiana na riwaya za Muhammed Said Abdulla. Makundi ambayo yalishughulikiwa kwa jamii ya Wazanzibari ni:

- a) Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza na walimu wa fasihi ya Kiswahili wafundishao Vyuvo vya Zanzibar kwa sababu ndio wanaozisoma kazi za mwandishi huyu. Hawa walitoka katika jamii ya Wapemba, Watumbatu na Wamakunduchi.
- b) Jamaa wa mwandishi ambao wanajua historia yake.
- c) Wakazi wa Zanzibar wenye umri kuanzia miaka 45 na kuendelea, wenye kuzielewa lahaja za Zanzibar.

3.4.2 Sampuli ya Watafitiwa

Utafiti huu ulitumia mbinu ya sampuli lengwa kwa kuchagua taarifa zinazohusiana na riwaya za Muhammed Said Abdulla. Mugenda na Mugenda (2003:50) wanasema kuwa katika kuitumia njia ya sampuli lengwa, mtafiti huchukua data ambazo zinahusu taarifa na malengo ya utafiti wake. Hivyo, sampuli ya utafiti huu imebainika kama ifuatavyo:

- a) Riwaya 3 ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale, Duniani Kuna Watu na Kosa la Bwana Msa.*
- b) Wanafunzi 20 wa Shahada ya Kwanza wasomao masomo ya fasihi ya Kiswahili kutoka SUZA (wanaume 13 na wanawake 10).

- c) Wahadhiri 5 wafundishao masomo ya fasihi ya Kiswahili kutoka SUZA (wanaume 3 na wanawake 2).
- d) Jamaa 2 wa mwandishi (mwanamme 1 na mwanamke 1).
- e) Wakazi 5 wa Zanzibar (wanaume 3 na wanawake 2).

3.5 Ukusanyaji wa Data

3.5.1 Njia na Zana za Ukusanyaji wa Data

Njia kuu zilizotumika kukusanyia data katika utafiti huu ni udurusu wa kimaktaba, usaili, na udodosaji. Zana zilizotumika ni mwongozo wa udurusu, mwongozo wa usaili na dodoso. Pia kulitumika kamusi za lahaja ya Kipemba, Kitumbatu na Kimakunduchi, kamusi ya Kiswahili Fasaha, kamusi ya Kiswahili - Kiingereza, Kiingereza - Kiswahili, Kiarabu - Kiingereza, na Kiingereza - Kiarabu. Zana nyingine ni riwaya tatu teule za Muhammed Said Abdulla, kompyuta, kinyonyeo, modemu, kalamu, wino wa kufutia, karatasi za A4, vijidaftari vya kuhifadhia data na vocha.

3.5.2 Mchakato wa Ukusanyaji wa Data

Ukusanyaji wa data ulishaelezwa katika mpango wa utafiti kuwa ni wa maktabani na uwandani. Ukusanyaji huo uliongozwa na misingi ya nadharia ya uhalisia ili kuondoa mkanganyo wa data katika ukusanyaji huo. Data za maktabani zilikusanywa kwa njia ya udurusu, ambapo mwongozo wa udurusu ulitumiwa. Mwongozo huo uliongoza kusoma maandiko mbalimbali kama vile tasnifu, majarida, vitabu na makala yahusianayo na utafiti huu. Pia, kusoma riwaya teule za Muhammed Said Abdulla ili kuibua msamiati, pamoja na makamusi kutolea etimolojia ya msamiati huo. Njia hii ya udurusu humwezesha mtafiti kukusanya, kuhakiki na kutoa maoni yenye nguvu na yenye kuleta maana kupitia ubora na wingi wa taarifa zenye ukweli (Amin, 2005:74).

Data za uwandani zilikusanywa kwa njia ya usaili na udodosaji. Mwongozo wa usaili ulitumika kuwasaili wahadhiri wa SUZA, jamaa wa mwandishi, na wakazi wa Zanzibar. Njia hii ilitumika, kama aelezavyo Kothari (2004), humpa fursa mtafiti kubadilisha swali iwapo hakutakiwa kuuliza maswali maalumu, hurahisisha upataji wa data kutoka kwa watu hata kama hawawezi kusoma na kuandika na humruhusu mtafiti kusaili vipengele vya nyongeza. Dodoso lilitumika kuwadodosa wanafunzi wa SUZA. Kompyuta, kinyonyeo, modemu na vocha vilitumika katika mchakato mzima wa uchapaji, uhifadhi na utafutaji wa data mitandaoni na kwa watafitiwa. Daftari na kalamu vilitumika kunukuu data zilizopatikana katika usaili na wakati wa udurusu.

3.6 Uchanganuzi wa Data

Uchanganuzi wa data ulizingatia misingi ya nadharia ya uhalisia na malengo ya utafiti. Data zote zilizokusanywa uwandani zilijumuishwa na zile za udurusu wa kimaktaba kisha kupimwa na kutathminiwa. Changamoto iliyojitokeza ni kupatikana etimolojia ya sehemu zaidi ya moja kwa baadhi ya maneno. Hali hiyo ilitokana na uhalisia wa mazingira ya Wazanzibari na matumizi yao ya lugha yalivyofanana na kuingiliana. Hivyo, ilibidi kurejelea makamusi kwa maneno yote ili kuondoa sintofahamu zilizojitokeza. Baada ya uchanganuzi huo, data zilizopatikana ziliwasilishwa katika mtindo wa malengo ya utafiti. Hivyo, kila lengo liliwasilishwa kwa maelezo na kuungiwa sehemu ya mjadala wenye maudhui yanayoenda sambamba na lengo hilo. Uchanganuzi wa namna hiyo unaunga mkono maelezo asemayo Kothari (2004:111 - 112) kwamba, data zinazopatikana zinachujwa kwa kiwango kikubwa kwa sababu data hizo zinatumika iwapo tu ni za uhakika, zinakidhi na zinafaa kwa kazi yenyewe.

3.7 Uhalali na Uthabiti wa Matokeo ya Utafiti

Uthabiti wa data ulizingatiwa kwa kiwango kikubwa. Uthabiti huo umeoneshwa kupitia vipengele vifuatavyo: Mosi, kutumia njia tatu katika ukusanyaji wa data ambazo ni udurusu, usaili na udodosaji. Pili, kuhoji na kuchunguza data kulingana na maelekezo ya nadharia iliyotumika. Tatu, kujikita katika kusudio la utafiti na kuweka mipaka madhubuti ili kuepuka mkanganyiko wa data hizo.

3.8 Itikeli za Utafiti

Mchakato wa utafiti huu ulifanyika kwa kufuata hatua, kanuni na sheria za utafiti vilivyo. Baada ya kupata ridhaa ya ukusanyaji wa data kutoka UDOM, mtafiti alihitaji tena ridhaa za watafitiwa ili kuendelea na mchakato huo. Kwa vile washiriki wengi katika utoaji wa data walihitaji kuwepo kwa usiri baina yao na mtafiti, mtafiti alitunza siri hiyo bila ya kumuathiri yoyote pamoja na kutotaja majina yao ili kwenda sambamba na matakwa ya wengi.

3.9 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura hii imejadili kipengele cha usanifu na mbinu za utafiti zilizotumika. Usanifu wa uchunguzi huu uliambatana na kuweka wazi mpango wa kazi, eneo lililotumika kufanyia uchunguzi huo pamoja na watafitiwa. Pia, imejadili uchanganuzi wa data zilizopatikana ambazo zilizingatia uhalali na uthabiti pamoja na itikeli za utafiti. Mchakato wote huo, haukuacha kuorodhesha mbinu na vifaa mbalimbali vilivyotumika pamoja na kujadili namna ya utumikaji wake katika mchakato wa ukusanyaji wa data. Sura inayofuata inajadili matokeo ya utafiti kulingana na malengo mahususi yaliyobainishwa katika sura ya kwanza.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI NA MJADALA WA MATOKEO YA UTAFITI

4.1 Utangulizi

Sura hii inajadili matokeo yaliyopatikana katika ukusanyaji wa data kwa kujiegemeza katika nadharia ya uhalisia. Mjadala huo umejikita zaidi kuchunguza lugha waliyobebeshwa wahusika katika riwaya teule, vielelezo vya kihistoria katika jamii na hali halisi ya mabadiliko ya lugha kulingana na nyakati ambazo riwaya hizo zilitungwa. Katika kufikia malengo ya utafiti huu, sura hii imegawika katika sehemu tano. Sehemu hizo ni miktadha ya maisha ya Wazanzibari, kijiografia, kiuchumi, kiutamaduni, kiisimu na kisanaa. Sehemu nyingine ni mihutasari ya riwaya teule za Muhammed Said Abdulla, matukio yenye msamiati unaoakisi miktadha ya Kizanzibari katika riwaya za mtunzi huyo na etimolojia yake. Nyingine ni athari za msamiati unaoakisi miktadha ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla kwa wasomaji na muhtasari wa sura.

4.2 Miktadha ya Maisha ya Wazanzibari

Wazanzibari ni wakazi wa visiwa viwili yaani Pemba na Unguja. Wakazi hawa walitawaliwa hasa na koloni mbili, Waarabu⁶ na Waingereza⁷. Khamis (2012) anaeleza kuwa kabla ya kuja mkoloni wa Kiingereza Zanzibar, Wazanzibari walikuwa wakiishi kwa mapenzi makubwa bila ya chuki za ukabila na urangi. Muingereza alipoingia aliwaundia Wazanzibari vyama vya kikabila na urangi. Vyama hivyo vilikuwa kama jumuiya za kikabila. Mfano wa jumuiya hizo ni *Arab Association, Shirazi Association, African Association na Indian Association*. Wazanzibari walivishabikia sana vyama hivyo na badala ya mtu kupigania maslahi

⁶ Walitawala kuanzia kipindi cha 1832 - 1889 kwa utawala wa Seyyid Said hadi Seyyid Baraghash.

⁷ Kuanzia 1890 Zanzibar ilikuwa chini ya Himaya ya Muingereza na Sultani hakuwa na nguvu yoyote (Utafiti, 2015).

ya Wazanzibari ikawa anapigania maslahi ya kabila lake. Na hayo yakawa ni mafanikio makubwa ya Muingereza kwani ni sera yake muhimu ya ukoloni ya wagawe uwatawale (*divide and rule*). Kuanzia harakati za kutafuta uhuru, chama cha *Afro Shirazi Party* (ASP) chini ya kiongozi wake mkuu Karume, walijaribu kuyatenga makundi yote ya Kizanzibari yaliyo na asili kutoka nje ya bara la Afrika kama vile Waarabu, Wahindi, Magoa na kadhalika. Pia hata Waafrika wenye ngozi nyeupe waliwakataa na kuwakejeli. Hivyo, waliunadi, kuutukuza na kuupigia kelele Uafrika pamoja na ngozi nyeusi na kuzidharau jamii zote za Kizanzibari zilizobaki.

Ilipofika mwaka 1964 chama cha ASP kiliongoza kufanya Mapinduzi na Wazanzibari walianza kujitawala wenyewe mpaka hivi leo. Lakini asili ya wakazi wake imebaki kuwa mchanganyiko hadi leo. Maisha yao ni kama zilivyo jamii nyingine kwa mazuri na mabaya. Wanaishi kiuujamaa kwa kuoneana huruma, kupendana na kusaidiana katika furaha na misiba.

4.2.1 Mukadha wa Kijiografia

Wazanzibari ni watu wa visiwa ambavyo hutambulika kwa jina moja la Zanzibar. Mipaka ya visiwa hivyo imeoneshwa na Krain (1998) pale aliposema kuwa, visiwa hivyo vimezungukwa na bahari ya Hindi Kusini mwa dunia. Vipo Kusini mwa Ikweta kutoka nyuzi 450° - 630° kwa mwelekeo wa Magharibi na Mashariki vimepakana na GM7 kutoka nyuzi 3910 - 3950. Vina jumla ya eneo la kilomita za mraba 2332. Vipo baina ya kilomita 30 hadi 50 nje ya ufukwe wa Tanzania.

Wazanzibari wamegawika katika maeneo makubwa mawili. Kuna Wapemba na Waunguja. Wapemba hutambulika kwa jina moja tu la Wapemba, nao huishi kisiwani Pemba. Ama Waunguja wamegawika kutokana na maeneo yao waliyotoka, Kusini au Kaskazini mwa kisiwa hicho. Kwa mfano, Wamakunduchi ni wale wote

wanaotoka Makunduchi, Watumbatu wanaotoka kisiwa cha Tumbatu, Wapaje wanaotoka kijiji cha Paje na Wajambiani wanaotoka kijiji cha Jambiani.

Ardhi ya visiwa hivyo ni milima, mabonde na tambarare. Ardhi hiyo hutumika kwa kilimo na ufugaji. Na kwa kuwa visiwa hivyo vimezungukwa na bahari, uvuvi ni shughuli nyingine ya wenyeji hao. Kilimo chao ambacho mara nyingi ni kwa ajili ya chakula ni kama muhogo, viazi vikuu, viazi vitamu, ndizi na mpunga. Pia, hufuga ng'ombe, mbuzi, kuku, bata, ndege na kasuku kwa ajili ya chakula na kwa biashara. Shughuli zao za uvuvi hufanyika katika bahari ya Hindi. Hutumia vyombo kama mashua, vidau, mitumbwi na boti za mashine kwa samaki wakubwa, wadogo na dagaa. Katika kutilia mkazo juu ya ardhi ya Wazanzibari, Ingrams (1931) anaeleza kuwa, kisheria ardhi ya Zanzibar ni ya serikali ingawa watu huiuza kwa kufanya makazi na kwa kilimo kienyejiyenyeji. Ni ardhi yenye aina zote za udongo. Katika suala la kilimo watu hutumia majembe ya mkono. Na ufugaji ni wa kienyeji ambao ni kwa ajili ya matumizi ya nyumbani. Ardhi ya Wazanzibari humea mazao ya nafaka, mboga mboga na miti mikubwa kwa ajili ya ujenzi. Kilimo chao mara nyingi si cha umwagiliaji, hufuatia mihula minne ya hali ya hewa. Kwa mfano, mazao ya nafaka ambayo hulimwa ni mbaazi, choroko, kunde, maharage, mtama na mihindi. Mboga mboga ni kama vile mchicha, figili, tungule, tikiti, nyanya chungu na bilinganya. Miti ya matunda humea sana Zanzibar; na hii ni moja ya chanzo cha mapato kwa familia nyingi za vijijini. Mfano embe, shokishoki, ndimu, parachichi, doriani, nanasi, papai, chungwa, miwa, limau, ndizi, stafeli na pera.

4.2.2 Mukadha wa Kiuchumi

Uchumi wa Wazanzibari unatokana na shughuli za uvuvi, kilimo na ufugaji. Pia, wanawake hutanda dagaa, hushona kofia, mikoba, makawa, vikapu na mikeka. Shughuli hizo wengi huzifanya kwa ajili ya mahitaji yao ya kila siku na kidogo kwa

biashara, hasa kilimo cha karafuu na nazi. Kihistoria, Wazanzibari ni wafanyabiashara wakubwa kwa sababu Zanzibar ilikuwa ni kituo cha biashara tangu zamani. Shughuli hiyo ilikuwa na nguvu tangu kipindi cha uongozi wa Kisultani kwa kuwa Waarabu wenyewe ndio wafanyabiashara wakuu. Hili linatiliwa mkazo na Mohamed (1994) anayeeleza hali hiyo kwa kusema kuwa, Zanzibar ni kituo cha biashara kwa nchi nyingi. Mbali ya karafuu, viwanda, pembe za ndovu na viungo, pia ilikuwa ni kituo kikubwa cha watumwa. Inasemekana kuwa tokea karne ya 15 wakati wa uongozi wa Kisultani, Zanzibar ilikuwa na pesa iliyojitengenezea yenyewe.

4.2.3 Muktadha wa Kiutamaduni

Utamaduni wa Wazanzibari unakwenda sambamba na dini ya Kiislamu. Takribani asilimia 97 za Wazanzibari ni Waislamu⁸. Utamaduni huu ni wa zamani sana tangu kuhamia kwa Waarabu kutoka Yemen na kufanya makazi yao kabla ya miaka 1498. Wahamiaji hawa walikuja na hati na imani za dini ya Kiislamu. Hivyo, mwaka 1498 walipoingia Wareno Zanzibar, Wazanzibari walikuwa tayari wanasifika kwa utamaduni wa dini hiyo. Dini hii ilisomwa sana na Wazanzibari hadi ikasababisha kutajika kwa Mashekhe maarufu wa dini kama vile Abdulla Saleh Al-farsy. Baadaye, walipoingia Waarabu kutoka Oman na kutawala Zanzibar, utawala wao ulikuwa ni wa Kisultani uliokuwa ukiendeshwa kwa misingi ya dini hiyo katika nyanja zote kama vile mavazi, hukumu na sheria. Hili limetiliwa mkazo na Makuthuria (2013) alipoeleza haya:

Waarabu walipofika Pwani ya Afrika Mashariki walianza kuingiliana na wenyeji wa upwa huo (Waswahili). Maingiliano ya kiutamaduni baina ya makundi haya mawili yalipelekea kuathiriana kiimani na vitu vingine vya kiutamaduni mfano, masuala ya ndoa, mavazi, vyakula, urithi na uchukuaji wa leksimu katika lugha. Waswahili wengi walijiunga na dini

⁸ Majadiliano kuhusu Uislamu Nchini Tanzania (http://sw.wikipedia.org/wiki/Dini_nchini_Tanzania).

hiyo ya Kiislamu, na kwa njia hii Waswahili wasingeweza kuepuka kujifunza lugha ya Kiarabu ili waweze kuielewa Kurani. Pamoja na hayo utamaduni wa Waarabu ulikuwa na vitu vingi zaidi kuliko utamaduni wa Waswahili na hii ilipelekea Waswahili wengi kuukubali utamaduni wa Waarabu kwa haraka. Matokeo yake utamaduni wa Waswahili uliiga mambo mengi kutoka katika utamaduni wa Waarabu, kama vile; katika leksimu maneno ya Kiarabu ni kama *Allah, mola, subhana, maulana, karama, kurani, tawadha, ramadhani, swala, msikiti, kaaba, kibla*, na *bismilahi*. Kiutamaduni, Waswahili walivutiwa na namna ya uvaaji kwa mfano wanawake kuvaa *hijabu* na *ushungi* na kwa upande wa wanaume huvaa magauuni marefu yaitwayo *kanzu*. Pia sheria zao za ndoa ziliongozwa na kanuni za dini ya Kiislamu ziiitwazo *sharia*.

Ujio wa wageni ulivyozidi kuongezeka katika maeneo mbalimbali ya Afrika Mashariki, ulisababisha kuharibu utamaduni wa Kiislamu uliokuwepo Zanzibar. Utafiti huu umegundua kuwa, mchakato wa kudai uhuru na kusababisha kufanyika kwa Mapinduzi ya mwaka 1964 zilitajwa kama ni sababu za kuharibika kwa utamaduni wa Kiislamu. Hii ilitokana na Ukoministi kutawala wenyeji hao. Hali ya mavazi kulingana na utamaduni wa Kiislamu ikaanza kupotea. Wanawake walikuwa wakitembea vichwa wazi huku wakiwa na vinguo mpaka magotini. Na wengine walikata nywele zao mkato wa *afro*⁹ wakawa wamefanana na wanaume. Ghafila, miaka ya 1980 hali ilipungua, watu wakarudi katika utamaduni wao wa asili. Kwa wanawake, utembeaji wa kichwa wazi ukatoweka na baibui na hijabu vikarejea tena miilini mwao. Hali hii inaendelea hadi sasa lakini utandawazi umeshaanza kuuathiri utamaduni huo. Hii leo wapo wanawake ambao wanavaa suruali na shati na kutembea kichwa wazi bila ya kujali asili wala dini yao. Hili linatiliwa mkazo na Suleiman (2015) wakati akifanya mahojiano na wakazi wa Zanzibar kuhusu changamoto za utalii katika visiwa hivyo. Anaeleza kuwa, sekta ya utalii Zanzibar, imechangia kuporomoka kwa maadili kwa kujikuta Wazanzibari wanaiga tamaduni

⁹ Ni mtindo wa kukata nywele zikawa kubwa kiasi cha kuweza kusukika lakini kwa kuwa Waafrika wana nywele ngumu basi nywele hizo huwa hazisukwi na badala yake huchanwa zikawa zimesimama (Utafiti, 2015).

za wageni ambazo haziendani na maadili yao. Vijana wa kiume husuka nywele na kuvaa mapambo ya kike na wasichana huvaa vivazi vinavyofanana na watalii wafikao hapo. Kwao wao jambo hilo limekuwa ni la kawaida ingawa ni kinyume na tamaduni zao. Hapo awali ilikuwa si rahisi kumuona mtu amelewa hadharani, lakini sasa jambo hilo ni la kawaida na nyakati za usiku ndio hali hubadilika zaidi kwani kila kona muziki wa kila aina hurindima.

4.2.4 Mukadha wa Kiisimu

Kimsingi, hakuna jamii isiyo na lugha kwa sababu lugha ni chombo cha mawasiliano. Kama ambavyo huko nyuma tulieleza kuwa Zanzibar ina wakazi mchanganyiko, hata lugha zao zimetofautiana. Hapo awali, hakukuwa na lugha moja iliyokuwa inawaunganisha watu wote. Lugha zao zilitegemea asili ya mtu anapotoka na kwa hivyo, kujikuta wana vijilugha kadhaa. Wakazi wa Pemba walikuwa wakitumia lahaja ya Kipemba. Hii haikuwa na mgawanyiko lakini ina tofauti za kimatamshi baina ya sehemu moja na nyingine. Whitely (1960) anaeleza kuwa lahaja hii imepata athari ya mjini na kupitia wageni. Wakati alipokuwa akifanya kazi Kusini Mashariki mwa Pemba mwaka huo aligundua kuwa lahaja safi ya Kipemba iko sehemu za vijijini.

Wakazi wa Unguja huzungumza lahaja tatu kuu. Mosi, lahaja ya Kitumbatu ambayo hutumika kwa wakazi wa Kaskazini mwa kisiwa cha Unguja. Lahaja hii huzungumzwa kisiwani Tumbatu na maeneo ya jirani ya kisiwa hicho kama vile Nungwi, Potoa, Mkwajuni, Matemwe, Pwani Mchangani, Chaani na Donge. Wazungumzaji wakubwa ni wenyewe wanaoishi kisiwani na kasi ya usemaji hupungua kadiri mtu anavyokuwa mbali na kisiwa chenye (BAKIZA, 2012). Pili, lahaja ya Kimakunduchi ambayo hutumiwa na wakazi wa Kusini mwa kisiwa cha Unguja. Lahaja hii huzungumzwa katika vijiji vingi vya Kusini mwa kisiwa hicho.

Kwa mfano, kijiji cha Makunduchi ambacho ndio makao makuu ya lahaja hiyo, Pete, Jozani, Kitogani, Paje, Jambiani, Muungoni, Muyuni, Kizimkazi, Kibuteni na Mtende. Wazungumzaji wake hutofautiana katika kiimbo, sauti, mkazo na msamiati. (BAKIZA, 2012). Tatu, lahaja ya Kiunguja mjini ambayo huzungumzwa maeneo ya mjini Unguja. Lahaja hii ikitumiwa na watu wa aina na namna tofauti. Kwa kuwa ni kawaida ya mjini kuwa na watu wengi wa kutoka maeneo tofauti, hivyo lahaja hii ilikuwa na nguvu sana kuliko lahaja nyingine. Wakazi wote waliokuwa wanaishi mkoa wa Mjini Magharibi mwa kisiwa cha Unguja wakiizungumza lahaja hiyo. Baadaye, miaka ya 1930 lahaja hii ilikuwa inatumika katika mawasiliano na shughuli zote za kiserikali; na hatimaye, kusanifiwa na kuwa Kiswahili sanifu.

Pamoja na lahaja zao, wenyeji wa Zanzibar hawakuacha kuathiriwa na wakoloni pamoja na utamaduni wa dini ya Kiislamu. Walitumia msamiati ya lugha za Kigeni kwa njia ya kutohoa maneno na kuyatamka wanavyojua wao. Kwa mfano maneno kama vile girikacha, katuni, marikiti, kortini, kalamu, mstari, daftari na kitabu. Pia, hata katika maandishi yao, wazee wengi wakiandika kwa hati za Kiarabu. Hii ilitokana na athari za Waarabu na dini ya Kiislamu kwa wenyeji hao kwa sababu walikuwa ndio walimu wa Waswahili katika kujifunza dini hiyo. Makuthuria (2013) akilitilia mkazo suala hilo, anaeleza ya kuwa:

Katika vituo vya biashara walijenga shule za Kiislamu karibu na misikiti yao, madarasa yalijengwa kwa ajili ya kuwafundishia wenyeji namna ya kusoma, kuandika na misingi ya dini ya Kiislamu. Lugha ya kufundishia ilikuwa ni Kiswahili. Kwa upande mwingine katika misikiti lugha ya Kiswahili na Kiarabu vilitumika kama lugha za mawasiliano.

Kwa wakati huu, Wazanzibari huzungumza Kiswahili fasaha kwa sababu yale maneno ambayo yalikuwa ni athari kutoka kwa wakoloni na dini ya Kiislamu,

yameshasanifiwa. Pamoja na lugha hiyo kuwa fasaha kwa wenyeji hao, haina maana kuwa lahaja zimepotea. Zipo na zinazungumzwa maeneo mengi ya shamba.

4.2.5 Muktaba wa Kisanaa

Katika mustawa huu, Wazanzibari walikuwa wana sanaa za aina zote kama vile upakasaji, ususi, ufumaji, utarizi, ushonaji, muziki, ufinyanzi, na fasihi. Kwa upande wa sanaa ya fasihi, Wazanzibari walikuwa na fasihi nenwa tu kwa sababu hapo awali hawakuwa na maandishi. Wazanzibari waliitumia fasihi nenwa kutambua hadithi ambazo zilikuwa zinatolewa wakati wa usiku kupitia bibi au babu kwa wajukuu zake. Pia, kuimba nyimbo ambazo zilikuwa zikiendana na tukio kama kuchombezea watoto, harusi, kushajiishana katika kufanyakazi za kilimo na uvuvi.

Kama ilivyo kwa jamii nyingine nyingi, sanaa ya ushairi ndiyo iliyokuwa ya mwanzo ukilinganisha na sanaa nyinginezo. Sanaa hii ilipata athari sana kutokana na ujio wa wageni. Iianza kuandikwa kwa hati za Kiarabu mara tu baada ya wageni kutoka Yemen kufika Zanzibar, huku maudhui yake yakibeba imani za kidini. Tamthilia zilichipuka kutokana na michezo ya baba na mama kwa watoto na maigizo ya wenyeji katika kushajiishana kufanyakazi.

Pamoja na fasihi andishi kuanza, fasihi simulizi ilikuwa ipo na inaendelea kukua. Katika kipindi chake cha ufalme Seyyid Barghash (1870 - 1888), alichukua kikundi cha waimbaji wa taarabu kutoka Misri kuja Zanzibar kwa lengo la kufanya maonesho katika Jumba la Ajabu - Zanzibar (*Bait-Al-Ajab*). Baadaye alimpeleka Bwana Mohamed Ibrahim nchini Misri kwa ajili ya kujifunza sanaa hiyo na kupiga ala zake. Aliporudi bwana Mohamed ndipo kulipoanzishwa kikundi cha taarabu Zanzibar mwaka 1905 na mwimbaji wa kwanza maarufu katika sanaa hiyo alikuwa ni Siti binti Saad. Mnamo mwaka 1958 vilianzishwa vikundi vyengine vya taarabu

ambavyo ni *Ikhwan Safaa Musical Club* (Ndugu Wapendanao) kisha *Culture Musical club (The History of Taarab in Zanzibar)*. Sanaa hiyo haikuishia hapo, ilizaa sanaa nyingine ambayo ni kidumbaki. Hii ilitokana na sanaa ya taarabu kuwasilishwa kwa kukaa kitako bila ya kucheza. Hivyo, kidumbaki kilifuata mtindo wa kucheza na waimbaji wake kusimama. Sanaa nyingine kama vile mchezo wa ngombe kwa wakazi wa Pemba na sherehe za Mwakakogwa kwa wakazi wa Makunduchi zilianza. Aidha, ngoma kama vile msewe, umeta na boso zilitamba kwa wenyeji hao.

Mnamo miaka ya 1920 -1930 wenyeji walianzisha vichekesho na vikaanza kutolewa redioni. Mfano wa vichekesho hivyo ni vichekesho vya Bakari Abeid. Baada ya hapo, uandishi wa fasihi ukaanza kufumuka kwa wakazi wa Zanzibar. Wasanii wa mwanzo waliyoibuka ni kama vile Muhammed Said Abdulla ambaye alikuwa maarufu kwa riwaya za kipelelezi, Shafi Adam Shafi, Abdulla Al-farsy na wengineo. Kazi zao walizoandika zilisawiri miktadha ya Wazanzibari kiutamaduni, kisiasa na kijamii. Hivyo, athari zilizomo katika jamii ya Wazanzibari hazikukosekana na utunzi wao.

4.3 Muhtasari wa Riwaya Teule

Sehemu hii imejadili kwa ufupi riwaya teule za Muhammed Said Abdulla ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale, Duniani Kuna Watu na Kosa la Bwana Msa.*

4.3.1 Muhtasari wa Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale

Mzimu wa Watu wa Kale ni riwaya ya mwanzo ya Muhammed Said Abdulla. Riwaya hii ilitungwa mwaka 1958 na kupata ushindi katika mashindano ya kutunga hadithi za kubuni ya mwaka huo yaliyotayarishwa na Idara ya *East African Literature Bureau*. Ingawa riwaya hii ni ya mwanzo kwa Muhammed Said Abdulla lakini kuna ustadi mwingi ndani yake. Ni riwaya yenye kueleza uhalisi zaidi ingawa

imo katika ubunifu. Inaeleza wahusika wenye uwiano sawa na wakazi wa Zanzibar. Mhusika kama vile Seti B. Sumatra, Mmanga Muuza Duka, Kurwa na Masanja wamejengwa kiuhalisia zaidi katika wasifu wa kazi zao. Lugha iliyotumika ni Kiswahili chenye usanii mkubwa wa maneno, mafumbo, na chenye ukweli wa kibunifu katika vipengele kama wahusika na uhusika wao.

Kisa chake kinaeleza kadhia ya mauaji ya kikatili kwa Bwana Ali Bin Bomani. Mhusika ambaye alikuwa akiwakilisha Umwinyi kwa watu wa Zanzibar. Mhusika huyu alikuwa ni tajiri lakini ni bahili wa kutosha. Bahili kwa familia yake na hata roho yake mwenyewe. Alikuwa na mashamba na mifugo. Kurwa na Masanja ni miongoni mwa wafanyakazi wake aliowakodi kwa ajili ya mifugo yake. Hatimaye, kifo cha Bwana Ali kilikutana na Bwana Msa ambaye ni mchunguzi maarufu wa kujitegemea. Bwana Msa alichunguza kifo cha tajiri huyo na kubaini mambo mengi ambayo yalimtatiza Inspekta Sefu na askari wenziwe. Pia, Najum, rafiki mkubwa wa Bwana Msa, alishangazwa na majibu ya uchunguzi huo. Walishangazwa sana kwani wote walidhani kifo cha Bwana Ali kilitokea mzimuni. Hata riwaya yenyewe ikapewa jina la 'Mzimu wa Watu wa Kale'.

Ubunifu huu ni wenye kila sifa ya kupewa tunzo. Usawiri wake wa lugha kwa wahusika na kadhia yenyewe ni sawa na mazingira ya riwaya husika. Mtu anapoisoma riwaya hii ataona ile dhana halisi ya fasihi ni kioo cha jamii. Muhammed Said Abdulla aliimulika jamii na kubaini mengi yaliyomo ndani yake hadi kutoa riwaya hii ya *Mzimu wa Watu wa Kale*.

4.3.2 Muhtasari wa Riwaya ya Duniani Kuna Watu

Duniani Kuna Watu ni riwaya nyingine ya Muhammed Said Abdulla iliyotungwa na kuchapishwa mwaka 1973. Ni miongoni mwa riwaya pendwa ya kipelelezi

iliyosanwa katika mandhari watu wa Zanzibar. Vipengele kama lugha, mandhari wahusika na maudhui vinaakisi mila, desturi, dini na ustaarabu kwa ujumla juu ya Wazanzibari.

Riwaya hii ilianza na kadhia ya mhusika Hakimu Marjani, mfanyabiashara, mkarimu na tajiri mkubwa mjini Unguja. Hakimu Marjani alikuwa na watoto wawili, Selume ambaye ni wa kike na mwingine wa kiume, Kasim. Watoto hao aliwalea kitajiri. Hakuwa mbahili wa mali aliyonayo katika matumizi yake, kwa wanawe na majirani. Alikuwa ni mtu wa watu bila ya ubaguzi wa sura, rangi wala kabila. Ghafla Hakimu Marjani alifariki na mali zake zote alizokuwa nazo zilitokomea zisijulikane zilipokwenda. Nini alikiwacha kwa warithi wake?

Ni kadhia pana na ndefu iliyowatanza maaskari wote na kushindwa wapi waanzie. Lakini kama ilivyo tabia ya wazee wengi kuandika kumbukumbu za matukio katika vitabu vyao vya kumbukumbu, Hakimu Marjani alikuwa akiandika katika msahafu. Baada ya kifo chake msahafu wake ulimfikia Bwana Msa, yule yule wa *Mzimu wa Watu wa Kale*. Alipambana na msahafu huo kuusoma mpaka kujua yote utandu hadi ukoko. Aligundua yote, ilipokwenda mali, mrithi wa mali na nani hahusiki katika mali hiyo kufuatia vidokezo katika msahafu ulioachwa na hayati huyo. Msahafu kweli unaweza kugundua vitu kama hivyo? Ni uchawi au ufundi? Ni kisa chenye mkasa mzito ambao, hatimaye, unatatuliwa na Bwana Msa aliyevishwa elimu ya Saikolojia katika kutatua kadhia ngumu kama hizo.

4.3.3 Muhtasari wa Riwaya ya Kosa la Bwana Msa

Riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* ilitungwa na kuchapishwa mwaka 1984. Ni riwaya ya mwisho kutungwa na Muhammed Said Abdulla kwa kipindi chote cha uhai wake. Ni riwaya ya kipelelezi kama zilizotungwa hapo awali. Mhusika mkuu ni yule yule

Bwana Msa aliyejitokeza katika riwaya zake zote. Pia, uhusika wake ni ule ule uliojengwa katika kuchunguza mambo na kutatua yaliyoshindikana. Lakini, kwa mara hii baada ya uchunguzi, utatuzi wake aliutoa ulikuwa ni wa makosa. Hiyo ndiyo sababu iliyoifanya riwaya hii kupewa jina la 'Kosa la Bwana Msa'.

Hili ni kosa ambalo Muhammed Said Abdulla alitaka kuielimisha jamii. Kosa alilolitenda Bwana Msa ni la kudiriki kutoa fat-wa ya kuoreshwa mume mwingine Bi Jamila wakati bado alikuwa ni mke wa Seyyid Ahmed. Bwana Msa alidiriki kutoa fat-wa hiyo eti kwa sababu ya kubadili jina Seyyid Ahmed wakati wa ndoa yake na Bi Jamila. Jambo hili huweza kutokea pale ambapo mhusika atahisi kulitumia jina lake sahihi kunaweza kuleta migogoro ama katika familia au jamii kama ambavyo alihofia Seyyid Ahmed. Mhusika huyu alibadili jina kwa sababu yeye alitoka katika ukoo wa kifalme na Jamila ni mwanamke wa Kiswahili. Hivyo, kwao ni aibu na fedheha kutekeleza jambo kama hilo. Hii ilitokana na ubaguzi uliokuwepo Zanzibar kwa baadhi ya wakazi wake kabla ya Mapinduzi 1964, baada na mpaka sasa urithi huu unaendelezwa kwa baadhi ya koo.

Ni jukumu kubwa kidini alilojibebesha Bwana Msa kwani, alitoa hukumu kwa jambo la kusikia tu pasi na ushahidi. Muhammed Said Abdulla hakuwa na shabaha ya kumuadhiri mhusika huyo, bali, yupo katika kuifunza jamii juu ya kuhukumu masuala kama hayo pasi na uthabiti wa hukumu yenyewe. Ni kweli makosa kama hayo hujitokeza katika jamii na mashekhe kuingia matatizoni kwa kufuata akili yake kinyume na elimu inavyoelekeza juu ya jambo hilo. Kimsingi, Muhammed Said Abdulla ni mpekuzi, mpelelezi na mvumbuzi wa kadhia mbalimbali zilizomo ndani ya jamii yake kwa lengo la kuburudisha, kuelimisha na kulinda historia ya jamii.

4.4 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Miktadha ya Kizanzibari katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla na Etimolojia Yake

Utafiti huu uliegemea nadharia ya uhalisia. Uegemezi huo umebaini kuwa dhana ya fasihi ni kioo cha jamii imefasiriwa vyema katika riwaya za Muhammed Said Abdulla. Ukweli huo unatokana na usawiri wa wahusika, lugha waliyobebeshwa na ujumbe wanaoufikisha. Kwa kuwa utafiti huu umekichunguza kipengele cha lugha kwa ajili ya kupata msamiati unaoakisi mazingira ya Kizanzibari na etimolojia ya msamiati huo, umeegemea muktadha wa Wazanzibari wa lugha zao, utamaduni wao pamoja na mazingira yao wanayoishi.

Katika muktadha wa lugha wa Wazanzibari, utafiti huu umegundua kuwa, wakazi hao wana tofauti ndogo ya vijilugha vyao baina ya sehemu moja na nyingine. Katika kulitilia mkazo suala hilo, Ingrams (1924) wakati anachunguza lahaja za Zanzibar alisema kuwa, lahaja ya Kimakunduchi na Kitumbatu zimefanana miundo yake na kadiri siku zinavyosonga mbele na watu kuenea kutoka sehemu mbalimbali, lahaja hizo zinaendelea kubadilika sauti na baadhi ya vitamkwa vyake tofauti na asili zilivyokuwa. Hali hiyo huzisababisha lahaja hizo kufifia au kuzichanganya na Kiunguja mjini ambacho ndicho kilichotawala zaidi Zanzibar. Naye Maganga (1991) akionesha msisitizo huo anaeleza kuwa, lahaja za Zanzibar zimefanana na zimekaribiana kifonolojia, mofolojia na msamiati. Wakati akieleza mofolojia kati ya lahaja ya Kimakunduchi, Kitumbatu na Kiunguja mjini alisema kuwa, kuna kanuni zilikwisha kupangwa kufuatwa katika mfuatano wa irabu katika vitenzi vya wakati uliopo (timilifu). Katika vitenzi hivyo, mzizi hufanana na irabu ya mwisho ya kitenzi. Katika ukurasa wa 36 alitoa mifano ya vitenzi kupitia Kiswahili na Kimakunduchi kama vile zimeenea, mmeuza, umeuza na zimeoza (Kiswahili) ambavyo vinasomeka zenee, muzu, kuzu na ziozo kwa Kimakunduchi.

Kutokana na tofauti ndogo iliyopo baina ya lahaja moja na nyingine, kusanifishwa kwa Kiunguja mjini kuwa Kiswahili sanifu, na hivyo kujalizwa msamiati kutoka lahaja nyingine za Zanzibar, kumesababisha wasomaji wengi wa riwaya za Muhammed Said Abdulla kutogundua matumizi ya lahaja katika riwaya hizo. Hii inaambatana na kutobaguliwa msamiati wa lahaja moja na nyingine katika riwaya za mtunzi huyo. Mfano wa msamiati uliojaziwa kutoka lahaja isiyokuwa Kiunguja mjini katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* ni hoshi (uk. 20), mafamba (uk. 26), dumaa (uk. 47), bera (uk. 82), mwande (uk. 121) na zuzu (uk. 122). Riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kuna maneno kama muwele (uk. 11), alidakiza na magugu (uk. 17), wambaje (uk. 43), bilashi na twana (uk. 59). Na riwaya ya *Duniani Kuna Watu* kuna maneno kama machugachuga (uk. 3), mtu mume (uk. 9), zuhali (uk. 15), wivi (uk. 73), kimeme (uk. 94), pumbao (uk. 97) na kiraru (uk. 115). Pia, katika riwaya hizo kuna maneno mengi ambayo ni Kiswahili sanifu kwa sasa yenye asili ya Kiunguja mjini. Maneno yenyewe ni riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* mbuya (uk. 8), mafamba na kufu (uk. 26), mbeja (uk. 50), mang'amung'amu (uk. 72), kikaka (uk. 75), ikatifikika (uk. 79), kwasi na kutwaza (uk. 121), kusowera (uk. 124), kutanza (uk. 127) na fununu (uk. 130). Riwaya ya *Duniani Kuna watu* maneno kama mpumbavu (uk. 5), magolegole (uk. 11), siungami (uk. 13), kumuanisi (uk. 21), kunisuta (uk. 66), zuti (uk. 88), nikidinda (uk. 96) na kigeugeu (uk. 114). Na katika *Mzimu wa Watu wa Kale* maneno kama imeseteka (uk. 4), rubaa (uk. 8), kuukuu (uk. 11), akichagawa (uk. 13), mazonge (uk. 35) na ametafarika (uk. 36).

Muktadha wa utamaduni kwa Wazanzibari umetawaliwa na itikadi za dini ya Kiislamu. Hivyo, katika kuitumia lugha, Muhammed Said Abdulla hakuwa nyuma kuisawiri lugha hiyo na utamaduni wa dini ya Kiislamu kama walivyo watu wake.

Pia, ametumia msamiati wenye asili ya lugha ya Kiarabu kutokana na ukweli kuwa Zanzibar ilitawaliwa na Waarabu. Mfano wa msamiati huo kutoka riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ni yahe (uk. 4), siyahi (uk. 12), heba (uk. 25), buhuri (uk. 33) na mintaarafu (uk. 54). Katika *Duniani Kuna Watu* ni masalheri, kujinadhifisha, kujitoharisha na sini (uk. 3), alisafidi (uk. 20), kumuanisi (uk. 21), nakama (uk. 39), kunishutumu (uk. 66), nisubu (uk. 71), jiha (uk. 73), ghabeni (uk. 80) na natija (uk. 84). Na katika *Kosa la Bwana Msa* maneno kama ajinabi (uk. 8), alimlaki (uk. 37), jiriwani (uk. 46), kustaladhi (uk. 68), maarubu (uk. 75), sikujibari (uk. 77), kifu (uk. 82), ewala (uk. 84), rakadha (uk. 109), duba (uk. 122) na anighufirie (uk. 129).

Katika muktadha wa mazingira ya Wazanzibari, Muhammed Said Abdulla amesawiri msamiati wake kimaeneo kama ilivyo kwa wakazi hao. Wazanzibari wanaoishi mkoa wa Kusini Unguja hutumia lahaja ya Kimakunduchi, Kaskazini Unguja hutumia lahaja ya Kitumbatu na Mjini Magharibi hutumia lahaja ya Kiunguja mjini. Mtunzi huyu alisawiri msamiati katika muktadha wa kimaeneo kwa kumchunguza mhusika ama pale anapoishi au asili yake. Kwa mfano, wahusika kama vile Sheha Haji Isa; Sheha wa Kazole, Bi Mwajuma wa Mbaleni, Kasim Hakimu aliyekuwa anaishi mjini katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*. Pia, Shekhe Judi wa Chwaka na Jamila mwenye asili ya Makunduchi katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*. Aidha, utafiti huu uligundua msamiati wenye hekima na busara kama walivyo wazee wa Kizanzibari. Hii inatokana na uhalisia wa mtunzi huyo ambaye alikuwa anapenda kukaa kwenye majlisi maalumu ya wazee maeneo ya Malindi, Mji Mkongwe na Darajani hasa wakati wa jioni kwa ajili ya mazungumzo.

Kulingana na mwongozo wa nadharia ya uhalisia ya kuonesha hali halisi ya wahusika na lugha wanayoitumia ili kuonesha mazingira ambamo jamii hiyo

inapatikana, tabia hiyo inaweka wazi kwamba, kusudi la Muhammed Said Abdulla ni kuweka bayana uhalisi wa kazi zake na jamii aliyoitungia kazi hizo kwa kujenga picha halisi ya mazingira ya Zanzibar kupitia wahusika, lugha, na maeneo ambamo wahusika hao wametokea.

Baada ya maelezo hayo mafupi, sasa tuingie katika kubainisha matukio na etimolojia ya msamiati unaoakisi mazingira ya Kizanzibari uliomo ndani ya riwaya tatu teule za Muhammed Said Abdulla. Msamiati wenyewe ni ule wenye asili ya lahaja za Zanzibar na lugha za Kigeni. Kipengele cha lahaja za Zanzibar kimebainisha msamiati ulio na chimbuko la lahaja zilizopo na zizungumzwazo Zanzibar. Msamiati huu umekubaliana na ule wenye ukasi na muktadha wa mazingira kwa sababu lahaja ambazo zipo Zanzibar zinategemea eneo ambalo mwenyeji wake anaishi au kutokea. Na kipengele cha lugha za Kigeni kimebainisha msamiati wenye chimbuko la lugha za Kiarabu na Kiingereza. Msamiati huo unaakisi mazingira ya Kizanzibari kwa kuwa Waarabu na Waingereza walitawala visiwa hivyo. Pia, unaakisi utamaduni wa Wazanzibari katika kipengele cha dini kwa kuwa wenyewe wake ni waislamu.

Aidha, katika uelekezaji wa etimolojia juu ya msamiati huo kuna mambo kadhaa ya kuzingatia ambayo ni:

- a) Maneno ambayo yana asili ya lugha za Kigeni, tayari yameshasanifiwa na kuwa Kiswahili sanifu. Na baadhi ya maneno hayo hutumika hata katika lahaja.
- b) Neno moja linaweza kuwa na maana zaidi ya moja, hivyo maana za maneno katika majedwali yanayofuata zimetolewa kulingana na lilivyotumika katika kitabu.

- c) Neno moja linaweza kutumika katika lahaja zote kwa sababu ya mchanganyiko wa msamiati na utamaduni wa wenyeji wa Zanzibar. Kwa mantiki hiyo, inaweza kutokea neno moja kutumika katika lahaja zote lakini katika utafiti huu, asili ya neno imetolewa kulingana na chimbuko lake.

4.4.1 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Mikdadha ya Kizanzibari na Etimolojia Yake katika Riwaya ya Mzimu wa Watu wa Kale

Ufuatao ni mjadala wa matukio yanayosawiri mikdadha ya Kizanzibari kutoka katika riwaya tatu teule za Muhammed Said Abdulla. Mjadala huu, hata hivyo, haukugusia matukio yote, bali uliteua yale yenye msamiati ambao, kwa maoni ya mtafiti yana kiasi kikubwa cha ugeni kwa hadhira. Hivyo, matukio hayo mateule ndiyo yaliyojadiliwa. Orodha kamili ya matukio yote yenye msamiati unaoakisi mikdadha ya Kizanzibari imewekwa katika majedwali mwishoni mwa mjadala wa kila kitabu.

Tukio la kwanza ni hili ambalo mwandishi anaeleza wasifu wa Bwana Musa kwa kutaja alama kuu zinazobainisha mwili mwake. Anasema:

Bwana Musa alikuwa kijana Mwafrika ambaye alikuwa mweusi tititi na mtu akiulizwa, "Bwana Musa gani?" hujibu "Si yule mweusi, yahe!". Alikuwa na uso mpana mwenye mashavu manene, na alivyokuwa pua yake imeseteka, midomo yake minene ilipata nafasi ya kujitoa, ikawa inaonyesha kama mdomo upo mbele na pua ipo nyuma (uk. 4).

Hapa mwandishi amekisi mikdadha wa Kizanzibari kupitia msamiati 'yahe na imeseteka'. Neno 'yahe' linatokana na neno '*yaa akhii*' lenye chimbuko la lugha ya Kiarabu kwa maana ya ewe ndugu yangu. Na neno 'imeseteka' linatokana na asili ya neno 'seteka' lenye chimbuko la Kiunguja mjini kwa maana ya kutonyanyuka. Maneno haya hayajabadilika maana zake wala matamshi. Aidha ukurasa huo huo mwandishi amebainisha tena msamiati unaoakisi mikdadha wa Kizanzibari kupitia mhusika wake Bwana Musa pale anaposema:

"Ahlan, Najum! Nimekustua au nimekuzingua? Ikiwa nimekustua, itakuwa nimekuroga; lakini, ikiwa nimekuzindua, itakuwa nimekuzingua. Bali ilivyokuwa hapo ulipochutama pana zinduko langu, na litayari kumzuga mtu yeyote atakayejitia umbeya, hapana shaka kwamba kutokea kwangu hivi sasa nikasimama mbele yako namna hii, kumekuzingua."

Hapa mwandishi ametumia maneno 'nimekustua, nimekuzingua, na nimekuzindua' ambayo maana zake zinakaribiana sana. Hiki ni kipaji cha mtunzi huyu anachokitumia sana katika riwaya zake. Maneno haya yanatumika sana kupitia wakazi wa Zanzibar na yana chimbuko la vijilugha vyao. Maneno 'nimekustua na nimekuzingua' yana chimbuko la Kiunguja mjini yakiwa na maana ya kumzindua mtu katika jambo na kumtoa mtu wahaka au tafrani zilizomo ndani ya kichwa chake. Na neno 'nimekuzindua' lina chimbuko la lahaja ya Kimakunduchi lakini maana yake na neno 'nimekustua' haitofautiani. Maana ya 'kuzindua' ni kumshitua mtu katika jambo. Aidha neno 'ahlan' linaakisi muktadha wa wakazi hao kupitia lugha ya Kiarabu. Neno hilo lina mantiki ya kumkaribisha mtu katika hali ya bashasha na pengine haikufikiriwa kuwa atatokea muda ule. Mtunzi amelitumia neno hilo kwa mkato lakini ukamilifu wake ni '*ahlan wasahlan*' na mara nyingine humalizikia kwa neno '*wamarhaba*'.

Tukio jingine ni hili ambalo mwandishi anamuonesha Mama Kipwerere anamuugua mwanawe Kipwerere katika ugonjwa alioupata wa kukumbwa na shetani. Mwandishi ameeleza hivi:

Kipwerere alijizoaoza pale kitandani alipolala akatangulia uani; mama mtu alifungua sanduku akatoa kanga mbili za kwenda kumfunikia muwele. Alimkuta muwele amekwisha kaa juu ya msala na miguu yake amenyosha upande wa kibla. Mama - Kipwerere alimfunika mwanawe kanga zote mbili gubigubi, tangu kichwani mpaka nyayoni, naye akarudi na kazi yake ya kutengeneza moto na manukato ya kumfukizia (uk. 11).

Msamiati 'muwele, msala, kibla na gubigubi' ndiyo ambayo imeakisi miktadha ya Kizanzibari katika tukio hilo. Tukianza na 'muwele na gubigubi' tunaona kuwa

mtunzi amejikita upande wa lahaja za Zanzibar; Kimakunduchi, Kipemba na Kiunguja mjini. Neno 'muwele' hutumia sana Wapemba na Wamakunduchi likiwa na maana ya mtu mwenye kutibiwa mashetani. Ama 'gubigubi' lina chimbuko la Kiunguja mjini kwa maana ya kujifunika nguo mwili mzima. Mwandishi ameyatumia maneno haya bila ya kubadilisha silabi wala maana. Aidha, maneno kama 'msala na kibla' yameakisi muktadha wa Wazanzibari kupitia kipengele cha utamaduni wao. Kama tunavyofahamu kuwa Wazanzibari wanafuata utamaduni unaoendana na silka ya dini ya Kiislamu, maneno hayo hutumika katika ibada ya sala, na kwa hivyo yana chimbuko la Kiarabu. Neno 'msala' lina maana ya kikatio maalumu kinachotumika wakati wa kutekeleza ibada ya sala. Inawezekana ikawa ni mkeka, busati au zulia. Neno hili chimbuko lake ni neno la Kiarabu '*muswallaa*' yaani mahali pa kuswalia (pa kufanyia maombi). Na neno 'kibla' lina maana ya upande maalumu ambao muislamu huelekea wakati anapofanya ibada ya sala. Ni neno linalotokana na neno la Kiarabu '*qiblat*'.

Katika uuguzi wa mama Kipwerere kwa mwanawe imeendelea tena ukurasa wa 12 ambapo uakisi wa msamiati na mazingira ya Kizanzibari imejitokeza tena. Mtunzi anaendelea kusema:

... alisogea akapenyeza mkono wa kulia chini ya kanga mpaka sikioni mwa mwanawe, mkono wa pili akapenyeza kile kitezo kinachotoa biwi la moshi linalonuka na kunukia pamoja, akimzungushia mwanawe kichwani huku akiomboleza kwa maneno yenye lafudhi au matamko kama Kiswahili cha Pemba cha ndani au Kiswahili cha asili cha Makunduchi; lakini, la mimi wala wewe hatukifahamu. Baada ya muda kitambo, muwele alianza kuharakisha kichwa chake kidogo kidogo... kichwa chake kikafikia juu ya ncha au ukingo wa baraza, akapiga siyahi ya nguvu sana...

Hapa utafiti ulibaini kuwa uakisi wa riwaya hii na muktadha wa Kizanzibari unaweza kutokea kupitia lugha iliyotumika dhahiri au si dhahiri. Mwandishi

alipodokeza tu kuwa "*akiomboleza kwa maneno yenye lafudhi au matamko kama Kiswahili cha Pemba cha ndani au Kiswahili cha asili cha Makunduchi*" tayari amebainisha mandhari ya riwaya hiyo. Lakini hakuridhika na udokezaji huo, alitumia maneno kama 'biwi, lafudhi na siyahi' kushadidia maneno yake. Neno 'biwi' linatumiwa na Wazanzibari wote, lakini kulingana na maana iliyokusudiwa katika utunzi huu, neno hilo lina chimbuko la Kimakunduchi na Kitumbatu kupitia maana ya mkusanyiko wa moshi. Ama 'lafudhi na siyahi' yameakisi muktadha wa Kizanzibari kupitia lugha ya Kiarabu. Ni maneno yenye chimbuko la lugha hiyo yanayotokana na maneno '*lafdhu na swiyaahu*' kwa maana ya tamko na kelele.

Mwandishi anatumia tena msamiati unaoakisi muktadha wa Kizanzibari wakati anawaelezea wachunga ng'ombe wa Bwana Ali walipokuwa wakimtafuta bwana wao baada ya kushindwa kurudi kwake. Anasema:

Kurwa na Masanja, Wanyamwezi wawili, masaisi wa ng'ombe wake Bwana Ali, wenye vibanda vyao uwanja mmoja na yeye, kwa nguvu walikubali kubanduka kunako marimba yao, wakawasha mienge yao, wakaelemea Baraste kuuliza habari za Bwana Ali na kukawia kwake kurudi nyumbani (uk. 14).

Tukio hili lina wahusika wenye asili ya Tanzania Bara. Lakini kwa kuwa mwandishi ameisawiri kazi hii katika jamii ya Wazanzibari, hakuwaelezea Kurwa na Masanja kwa lugha zao, bali, aliakisi muktadha wa Wazanzibari kama ndio jamii halisi ya kazi hiyo. Msamiati kama 'marimba, mienge, wakaelemea na baraste' ndiyo inayosawiri jamii hiyo kupitia kipengele cha lahaja za wakazi hao. 'Marimba, mienge na wakaelemea' yanaakisi muktadha wa Wazanzibari kupitia lahaja ya Kiunguja mjini. Maneno hayo ameyatumia bila ya kubadilisha maana wala silabi. Maana zake ni ala ya muziki ya mbao inayopigwa kwa kugongwa kwa kirungu, makuti yaliyofungwa pamoja, na kuwashwa na kwenda kusikojuilikana. Ama neno

'baraste' amelitumia kwa ama kupunguza silabi 'i' baina ya 's' na 't' kumaanisha chimbuko lake ni Kipemba au kubadili silabi 'r' badala ya 'l' kumaanisha chimbuko lake Kimakunduchi, yote yakiwa na maana moja ya njia pana. Hali hii inaweza kutokezea kwa maneno mengi kama tulivyokwisha kusema huko nyuma ya kwamba, lahaja za Zanzibar zinafanana msamiati, maana na matamshi.

Katika ukurasa wa 17, wakati Najum na Bwana Musa wakijadiliana kuhusu kutorudi kwa Bwana Ali nyumbani, mwandishi anaeleza haya:

Najum ndio kwanza aone kuwa Bwana Musa ameshika kitabu chake mkononi na huku anakwenda, akasema, "Nasemaje? Ulisema kuwa Bwana Ali ameuawa?" "Sikusema", Bwana Musa alidakiza, "nimefasiri maneno ya yule bibi tu, au shetani wake kwa ufupi." Bwana Musa huwachi kunyerereka namna hiyo? Mtu hajui ashike lipi?

Hapa mwandishi ametumia msamiati 'alidakiza na kunyerereka' kuiakisi kazi yake na jamii husika. Etimolojia ya msamiati huo unatokana na lahaja ya Kipemba kwa neno 'alidakiza' na Kiunguja mjini kwa neno 'kunyerereka'. Neno 'alidakiza' linatokana na asili ya neno 'dakiza' lenye maana ya kuingilia kati mazungumzo. Na neno 'kunyerereka' linatokana na asili ya neno 'nyerereka' lenye maana ya kuondoka bila ya kutoa taarifa. Kupitia nadharia ya uhalisia, usawiri wa maneno hayo unapatikana kupitia vijilugha vya jamii hiyo.

Mwandishi akiendelea kuisawiri kazi yake na jamii ya Wazanzibari kupitia mjadala wa Bwana Musa na Najum kuhusu kutorudi kwa Bwana Ali, anasema:

... Bwana Ali aliwaonyesha wale watu ngombe wote, takriban mmoja mmoja. Nini unadhania, Najum? Bwana Musa alikata maneno yake na huku akizunguka nyuma kumtazama Najum. Najum hakujibu neno bali alinyamaza tu... Njia waliyokuwa wakiipita ilianza kuwa nyembamba, tena imeota magugu, katikati yake au ya huku na huku yamekutana katikati. Umande wa Alfajiri ulioganda katika hayo magugu ulilowesha suruali zao kwa chini. Kwa hakika, walikuwa wakikaribia kile kichaka kinachoendelea mpaka kwa Baniani, kiitwacho, 'Mzimu wa Watu wa Kale' (kur. 17-18).

Katika tukio hili, utafiti umegundua msamiati 'takriban na magugu' kuwa ndiyo yaliyosawiri muktadha wa Kizanzibari kupitia nadharia ya uhalisia. Maneno hayo yaliakisi jamii hiyo kupitia lugha ya Kiarabu na lahaja ya Kimakunduchi. Neno 'takriban' lina maana ya kitendo cha kukisia kitu kiidadi lenye chimbuko la neno la Kiarabu '*taqriibaa*'. Na neno 'magugu' lina maana ya majani yaliyoota yenyewe na kufanya msitu mdogo. Maana hiyo imepatikana kutoka katika lahaja ya Kimakunduchi. Inawezekana ukapata maana nyingine zaidi ya hiyo lakini kwa jinsi lilivyotumika neno hilo katika muktadha huo, maana yake ni hiyo.

Pia katika ukurasa wa 35, mtunzi anaeleza hali ya Najum alipokuwa haelewi ufafanuzi wa Bwana Musa walipokuwa wakimtafuta Bwana Ali, kwa kusema:

Najum hakuelewa maneno ya Bwana Musa hata kidogo; aliona mazonge tu, yaani neno hili linatiwa huku na kutolewa kule mumo kwa mumo; kwa hiyo, alinyamaza kimya kama aliyepigwa na kibuhuti.

Hapa kalamu ya mwandishi iliangukia kuiakisi jamii yake kupitia lugha ya Kiarabu na lahaja ya Kiunguja mjini. Neno 'kibuhuti' lina maana ya huzuni ambalo linatokana na neno la Kiarabu '*huznu*'. Aidha, neno 'mazonge' lina maana ya matatizo, ambalo lina chimbuko la lahaja ya Kiunguja mjini. Maneno hayo, mwandishi ameyatumia si kwa kuonesha ustadi wake tu, bali, hata kuiakisi jamii yake kama ndiyo jamii andikiwa.

Msamiati mwingine uko katika ukurasa wa 59 katika tukio la kutafutwa kwa wauaji wa Bwana Ali baada ya kugundulika kuwa bwana huyo ameshafariki. Inspekta Sefu alisema yafuatayo:

Kweli, Mwarabu mgeni alikuwa na upanga na tumesikia kuwa ni mtu mwenye nguvu nyingi, lakini sidhani kwamba ana wazimu hata achukue upanga apite akiuwa watu tu bure bilashi. Kwani yeye ana kisasi gani na Bwana Ali hata atake kumwua... mgeni wa Mungu pale alipo? Na Hamisi, yule Boi?... Twana jabari, jenda wazimu, vutaji bangi neno lolote aweza kulifanya.

Kuwapo kwa uakisi wa msamiati wa Kizanzibari katika ukurasa huu kunatokana na mwandishi kutumia msamiati 'bilashi' wenye chimbuko la lahaja ya Kitumbatu 'bileshi' au Kipemba 'bilashi' kwa maana ya bila ya ulazima wa kufanya. Aidha, msamiati 'twana' una chimbuko la Kipemba kwa kumaanisha neno 'ntwana' lenye maana ya mtumishi wa kiume. Mwandishi ametumia neno 'twana' kuonesha ulinganifu wa kimwili wa mtu huyo na kumsifia kwa neno 'jabari' kwa maana ya kuwa ni mwenye kiburi. Neno 'jabari' lina asili ya Kiarabu kupitia neno '*jabbaar*'. Aidha 'jendawazimu' ni sifa nyingine ya 'twana' kufuatia upatanisho wa neno hilo. Neno hilo lina maana ya upungufu wa akili lenye chimbuko la Kiunguja mjini 'mwendawazimu'.

Jedwali 1: Muhtasari wa Msamiati Kutoka katika *Mzimu wa Watu wa Kale* na Etimolojia Yake

Uk.	Neno	Asili Yake	Maana Yake	Chimbuko Lake	Maelezo
1	Mbacha	Mbacha	Mkeka mkongwe	Kimakunduchi	Halijabadilika
2	Liliwaka nganya	Kangananya	Kuchanganya nafsi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
4	Nimeku-zindua	Zindua	Kumshitua mtu katika jambo	Kimakunduchi	Halijabadilika
4	Yahe	Yakhe	Ewe ndugu yangu	Kiarabu	Yaa akhii يأخي
4	Imeseteka	Seteka	Kukaa kwa kitu kikajitawanya hali ya kuwa kina uwezo wa kusimama	Kiunguja mjini	Halijabadilika
6	Saa eda	Saa ihda	Saa kumi na	Kiarabu	Ihdaa

	shara	ashara	moja		ghashara saa احدي عشرة ساعة
8	Rubaa	Rubaa	Watu ambao wanashirikiana katika safari yao	Kiunguja mjini	Halijabadilika
8	Walipota nabahi	Tanabahi	Walipojua	Kiarabu	Tanbih تنبيه
10	Anaye-kwamba	Kumbwa	Kupatwa na shetani	Kiunguja mjini	Amebadili nafasi kwa silabi 'w' na kuondoa silabi 'u'
11	Gubigu-bi	Gubigubi	Kujifunika mwili mzima kuanzia unyayo mpaka kichwa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
11	Kuukuu	Kuukuu	Kongwe lenye kuchakaa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
11	Msala	Msala	Kikalio ambacho hutumika wakati wa kutekeleza ibada ya sala	Kiarabu	Muswallaa مصلى
11	Kibla	Kibla	Upande maalumu wa kuelekea wakati mtu anaposali	Kiarabu	Qiblat قبلة
11	Muwele	Muwele	Mtu mwenye kutibiwa mashetani	Kimakunduchi Kipemba	Halijabadilika
12	Biwi	Biwi	Mkusanyiko wa vitu	Kimakunduchi Kitumbatu	Halijabadilika
12	Siyahi	Siyahi	Kelele	Kiarabu	Swiyaah صياح

12	Lafidhi	Lafudhi	Maneno au tamko	Kiarabu	Lafdhu لفظ
13	Alidu-waa	Duwaa	Kupigwa na mshangao	Kimakunduchi	Halijabadilika
13	Akicha-gawa	Chagawa	Kupandwa na shetani	Kiunguja mjini	Halijabadilika
14	Marimba	Rimba	Ala ya muziki ya mbao inayopigwa kwa kugongwa kwa kirungu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
14	Mienge	Mwenge	Makuti yaliyofungwa pamoja na kuwashwa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
14	Waka-elemea	Elemea	Kwenda kusikojulikana	Kiunguja mjini	Halijabadilika
14	Baraste	Balaste au barasite	Njia kubwa ya lami	Kimakunduchi Kipemba	Ampunguza au amebadili silabi
16	Kartuni	Katuni	Michoro inayofananishwa na binadamu	Kiingereza	Cartoon
17	Magugu	Magugu	Majani yaliyoota wenyewe na kufanya msitu mdogo	Kimakunduchi	Halijabadilika
17	Kunye-rereka	Nyererereka	Kuondoka bila ya kutoa taarifa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
17	Alidaki-za	Dakiza	Kuingilia kati mazungumzo	Kipemba	Halijabadilika
17	Takriban	Takriba-	Kitendo cha	Kiarabu	Takriibaa

		ni	kukisia kitu kiidadi		تقريباً
22	Kortini	Korti	Mahakama	Kiingereza	Court
28	Upeto	Upeto	Mkunjo kwenye nguo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
29	Nimesta- kabadhi	Stakaba- dhi	Kukabidhi	Kiarabu	Istakbadhwa استقبض
33	Buhuri	Buhuri	Punje ndogo ya ubani	Kiarabu	Bakhuur بخور
35	Mazonge	Mazonge	Matatizo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
35	Kibuhuti	Kibuhu- ti	Huzuni	Kiarabu	Huznu حزن
36	Ametafa- rika	Tafrani- ka	Kuzongwa na mambo	Kiunguja mjini	Ampunguza silabi 'n' na kuongeza 'a'
42	Imere- mbware- mbwa	Rembwa rembwa	Imechimbuliwa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
42	Fikara	Fikra	Mawazo	Kiarabu	Fikrat فكرة
43	Wambaje	Wamba- je	Maamkizi yanayotumika mara nyingi asubuhi	Kipemba	Halijabadilika
50	Ambala- nzi	Ambale- si	Gari ya kuchukulia wagonjwa	Kiingereza	Ambulance
54	Mintaara- fu	maarifa	Kwa kulingana na hayo	Kiarabu	Maghrifat معرفة
59	Jenda wazimu	Mwenda wazimu	Mtu aliyeugua ugonjwa wa akili	Kiunguja mjini	Amebadili silabi 'mw - j'
59	Bilashi	Bileshi au	Bila ya ulazima wa kufanya	Kitumbatu, Kipemba	Kitumbatu- amebadili

		bilashi			silabi 'e-a'
59	Twana	Ntwana	Mtumishi wa kiume	Kipemba	Ampunguza silabi 'n'
59	Jabari	Jabari	Mwenye kiburi	Kiarabu	Jabbar جبار

4.4.2 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Mikdadha ya Kizanzibari na

Etimolojia Yake katika Riwaya ya Duniani Kuna Watu

Tukio la kwanza tunalipata pale mwandishi anapomueleza Kasim wakati anaelekea darini kwa baba yake, Hakimu Marjani ambaye alikuwa anajitayarisha kutekeleza ibada ya sala. Mwandishi anaeleza hivi:

Kwa kitambo alichosita pale, uso wake ulionyesha machugachuga, lakini mara alijikuta akisema kichinichini, "potelea mbali, nitakwenda." Alipofika darini alikutana na baba yake soli anarudi msalani ambako kulikuwa ni faragha ya mambo yote yanayohusu kujikosha, kujisafisha, kujinadhifisha, kujitoharisha na kusali. "Masalheri, bwana," ilimtoka Kasim (uk. 3).

Katika tukio hilo, mwandishi ameonesha msamiati unaoakisi mazingira ya Kizanzibari kama vile 'machugachuga, kujikosha, kujinadhifisha, kujitoharisha, kusali, na masalheri'. Maneno kama 'machugachuga na kujikosha' yana chimbuko la lahaja za Zanzibar, Kimakunduchi na Kiunguja mjini. Maana ya maneno hayo ni hofu ya kufanya jambo na kujiweka safi kwa kutumia maji. Ni maneno yenye asili ya Kimakunduchi 'machugwachugwa' ambapo mtunzi amepunguza silabi 'w' na Kiunguja mjini 'kujiosha' ambapo mtunzi ameongeza silabi 'k' ili kusawiri lahaja hiyo. Ama maneno 'kujisafisha, kujinadhifisha, kujitoharisha, kusali, na masalheri' yana usawiri na dini ya Kiislamu. Chimbuko lake ni Kiarabu kwa maana ya kuondoa uchafu '*swaafi*', kujiweka safi '*nadhwiif*' na kuepukana na hadathi zote kubwa na ndogo '*twahaarat*' ili kutekeleza ibada ya sala (kufanya maombi) '*swalaat*'. Ni maneno yanayosisitiza kuhusu suala zima la usafi kwani ni sehemu pekee ambayo mtu huwepo karibu na muumba wake. Neno 'masalheri' lina maana ya habari za jioni

'*masaul khair*' kama ilivyo kawaida ya lugha ya Kiarabu kuwa inazingatia nyakati katika kuulizana hali kama ni asubuhi au jioni.

Katika matumizi ya lugha juu ya mwandishi huyu kuna kiwango kikubwa cha matumizi ya msamiati wenye ukaribu wa maana zake. Katika ukurasa wa 36 ametumia tena msamiati wa namna kama hiyo wakati alipokuwa akionesha tukio la majibu ya hasira aliyotoa Selume kumjibu kaka yake, Kasim alipokuja kudai pesa kwa baba yake. Tukio linapambanua hivi:

Haya Selume, mtoto kipenzi cha baba, nipe hizo shilingi mia tatu n'ende zangu. Miadi yangu, lakini usisahau; akifa baba... "Akifa baba!" alijibu Selume kwa bezo na sodawi. Shika ma-i yako haya, utuondokee hapa. Alimnyoshea mkono kumpa pesa alizotaka huku akimtupia jicho la dharau, izara na twezo.

Hapa mwandishi alikuwa anaonesha msamiati unaoonesha dhana nzima ya kutothaminika kwa kitu au mtu. Maneno kama 'bezo, dharau, izara na twezo' yote yanafikisha taarifa moja ya kupoteza thamani. Maneno haya yana akisi muktadha wa Wazanzibari kupitia lahaja zao. Neno 'bezo' hutumika sana kwa Wapemba na Watumbatu likiwa na maana ya dharau ya hali ya juu. Aidha, 'sodawi' lina chimbuko la lahaja ya Kipemba kwa maana ya kuringa kutokana na kipato au maumbile. Ama maneno kama 'dharau, izara na twezo' hutumika kwa wakazi wengi wa Zanzibar lakini chimbuko lake hasa ni Kiunguja mjini. Maneno haya yana maana ya 'dharau' kuondosha sifa ya kukijali kitu, 'izara' fedheha na 'twezo' kutothamini.

Tukio jingine ambalo lina msamiati wa namna kama hiyo ni lile ambalo mwandishi anatuonesha fikra za tamaa alizokuwa akiziwaza Kasim kwa Selume juu ya mali aliyoiacha baba yao lakini mambo yote yakawa kinyume chake. Mwandishi anasema yafuatayo:

Kifo cha baba yake kilikuwa nakama au sukumizo lenye nafuu na faida kwa mwanawe, Kasim. Yeye aliona kuwa yule baba kamfadhili pakubwa

kwa kutajamali kwake kufa kwa haraka... Atatengeneza mipango na wagawaji urithi kwa "kuzunguka nyuma ya mbuyu," Selume arushwe hapa, anyang'anywe pale, adokolewe hiki, afifilishwe kile; hata kama atabakiwa na kitu hakitakuwa kitu cha kukiita "kitu" ila ni kitu kidogo, cha uzembe tu (uk. 39).

Katika tukio hili mtunzi amechanganya msamiati wenye chimbuko la Kiarabu, Kipemba na Kiunguja mjini. Msamiati huo unatumika kwa wakazi wote wa Zanzibar bila kubadilishika maana baina ya sehemu moja na nyengine. Hii ni kutokana na uhalisia wa wakazi hao kutotofautiana sana katika lugha zao. Msamiati kama 'nakama, kamfadhili na kutajamali' yana chimbuko la Kiarabu. Maana za maneno hayo ni 'nakama' maangamizo, 'kamfadhili' wema au hisani anayofanyiwa mtu, na 'kutajamali' kujipamba. Ni maneno yaliyochimbukia kutokana na maneno ya Kiarabu '*naqamat, fadhwal, na jamiil*'. Pia, maneno kama 'anyang'anywe na adokolewe' yana chimbuko la lahaja ya Kipemba. Maana zake ni kuchukua kitu kwa kutumia nguvu bila ya hiari ya mwenyewe na kupunguziwa (kupewa kitu kidogo). Ama maneno kama 'sukumizo na afifilishwe' yana chimbuko la Kiunguja mjini. Maana zake ni laana na kufanyiwa kitu kuwa hakipo (kuondolewa). Maneno kama 'kunyang'anya, kufifilisha na kudokowa' yana dhana moja ya kufanya kitu kwa dhulma. Mwandishi ameyatumia maneno hayo kuonesha msisitizo wa dhana hiyo na pia kuonesha umahiri wake juu ya kucheza na lugha. Ni maneno ambayo ameyatumia bila ya kubadilisha maana wala silabi.

Msamiati mwingine inayoakisi miktadha ya Kizanzibari imejitokeza katika tukio la majibu ya Bwana Msa juu ya sifa alizopewa na Spekta Seif. Bwana Msa anaeleza kuwa:

"Spekta Seif! Sijui kama hivyo ndiyo katika jumla ya kunisifu au ndiyo namna yako ya kunisusiika, kunishutumumu na kunisuta. Lakini, tuk'enda nikakuonyesha mali hiyo ilipo, halafu nikikueleza na kukukamatisha mwivi wako mkononi, basi hutanibeua tena kama hivo" (uk. 66).

Kama ilivyo kawaida ya Muhammed Said Abdulla kuchanganya msamiati wenye chimbuko tofauti huku yakiwa na msisitizo katika jambo moja, ameonesha tena katika tukio hili kwa maneno kama 'kunisusuika, kunishutumu, kunisuta na hutanibeua' kwa msisitizo wa dhana mzima ya kuonesha dharau. Msamiati 'kunisuta na hutanibeua' yana chimbuko la Kiunguja mjini, 'kunisusuika' Kimakunduchi, 'kunishutumu' Kiarabu na 'mwivi' Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba. Maana za maneno hayo ni 'kunisusuika' kutokubaliana na jambo, 'kunishutumu' kunitukana kwa chimbuko la neno la Kiarabu '*shutmat*', 'kunisuta' kumkadhibisha mtu mbele za watu, 'hutanibeua' kutomtizama mtu kwa dharau na 'mwivi' mtu anayechukua kitu bila ya idhini ya mwenyewe. Kulingana na uchunguzi uliofanyika juu ya mwega wa nadharia ya uhalisia, utafiti huu umegundua kuwa ni hekma kwa Wazanzibari kutumia msamiati ambao haupo wazi sana kiasi ambacho huhitaji ufafanuzi. Kwa hivyo, ithibati ya matumizi ya msamiati ya namna kama hiyo inajidhirisha kupitia lugha ya mwandishi wa vitabu hivyo kama tulivyokwishaona katika matukio yaliyopita.

Aidha, tukio la ukurasa wa 71 hali hiyo inajirejea tena wakati mwandishi anauonesha msisitizo wa Bwana Msa kwa Spekta Seif juu ya ukutaji wa mali katika pango.

Bwana Msa anaeleza hivi:

"Sikiliza, Seif," aliteta Bwana Msa, "wewe umekuja kwangu kutaka msaada kwa kujua kuwa mimi naweza kukusaidia. Nimekukubalia. Mbona wewe sasa, baada ya juhudi niliyoichukua katika kukusaidia, unakataa kunikubalia yangu? Wewe ingia katika pango na utoke hukupata kitu, halafu nilaumu, nisubu, unitukane utakavyo - bali nenda kwanza.

Maneno yaliyopigiwa mstari chini yake ni maneno ambayo hayana maana nzuri lakini Bwana Msa kaweza kuyatumia kwa makusudi ya kumhakikishia Spekta Seif

kuwa anachokifanya ana uhakika nacho. Na kwa hivyo, uhuru aliyoutoa kwa Speкта Seif hautotendeka. Maneno hayo yana chimbuko la Kiunguja mjini 'unitukane' na Kiarabu 'nilaumu na nisubu'. Maana zake ni 'unitukane' kusema neno linaloudhi, 'nilaumu' kumsuta mtu juu ya jambo fulani kwa msingi wa neno la Kiarabu '*lawwaamat*' na 'nisubu' kusuwa au kulaumu kwa msingi wa neno la Kiarabu '*sabiikat*'.

Tukio jingine ni hili ambalo mwandishi anaonesha mjadala wa mali ya marehemu Hakimu Marjani juu ya warithi halali wa Marehemu. Mwandishi anasema:

"Sikiliza, Kasim," alimwita kwa ukali, "sikukuleta mimi hapa uje ufanye ghasia. Nimekwiteni hapa nyote mje kumsikiliza Bwana Msa maneno yake atakayotuzungumzia sio kumtolea ufidhuli au kumtukana namna hiyo... mimi bado nakutuhumu wewe ndiye mwivi aliyeiba mali ya baba'ako... "Kanitoa kusudi nje anionyeshe namna anavyoniibia yeye mali yangu, urithi wangu wa baba'angu kimachomacho amhonge huyu nani huyu - ghabeni asiyekuwa na kwao!"... Basi nakuombeni jamaa, bora sote tustahamili, tufyate hamaki na fadhaa zetu, tumwache Bwana Msa aendelee. Endelea bwana..." "Basi, bibi, basi Sheha, nendeni mkakae," aliwapa ruhusa Bwana Msa. "Sasa njoo Speкта Seif na uje hapa Bw. Kasim." Kasim aliikalifisha nafsi yake yenye kiburi, ufidhuli, deko, unyarafu na usodawi kwenda pale mbele ya Bwana Msa pamoja na Speкта Seif... Kasim alipasuka kwa kicheko, akarudi kitini kwake kwa mwendo wa mikogo na kujinyeta (kur. 79 - 81).

Hapa mwandishi amerejea tena kutumia msamiati wenye kuonesha hekma za wazee wa Kizanzibari. Maneno aliyoyatumia mtunzi ni maneno yenye maana fiche ambayo si rahisi kwa mtu yoyote kuyafafanulia maana zake. Maneno hayo ni 'mwivi, nakutuhumu, ufidhuli na kumtukana' ambayo tayari yameshatolewa etimolojia yake katika matukio yaliyotangulia. Aidha, maneno kama 'ghabeni, tufyate, fadhaa, aliikalifisha, kiburi, deko, unyarafu, usodawi na kujinyeta' yana uakisi na jamii hiyo. Maneno 'ghabeni, fadhaa, aliikalifisha na kiburi' yana chimbuko la lugha ya Kiarabu. 'Ghabeni' ni neno lenye maana ya mdanganyifu linalotokana na neno '*ghabana*', 'fadhaa' lina maana ya balaa ya mambo mazito au mshtuko kutokana na neno

'*fadhwa*' lenye maana anga, 'aliikalifisha' lina maana ya kufanya jambo kwa kujilazimisha, linalotokana na neno la Kiarabu '*yukallif*' na 'kiburi' lina maana ya hasira mbaya linalotokana na neno '*kibri*'. Ama 'ufidhuli na usodawi' yana chimbuko la lahaja ya Kipemba kwa maana ya 'ufidhuli' tabia ya kutothamini watu wengine na 'usodawi' kuringa kutokana na kipato. Aidha, maneno kama 'tufyate, mikogo na kujinyeta' yana chimbuko la lahaja ya Kiunguja mjini yenye maana ya 'tufyate' kunyamaza kimya kwa woga, 'mikogo' mbwembwe' na 'kujinyeta' kujiona mzuri na msafi. Na neno 'deko' lina chimbuko la lahaja mbili, Kimakunduchi na Kitumbatu linalomaanisha ringo au kutegemea kwa mtu mwengine. Maneno hayo mwandishi ameyatumia katika riwaya hiyo bila kubadili maana zake kulingana na jamii ya Wazanzibari na hilo linathibitisha usawiri wa nadharia ya uhalisia ndani ya kazi hiyo.

Kama ilivyojitokeza katika sehemu nyingi huko nyuma juu ya matumizi ya visawe vyenye usambamba katika kusesitiza jambo fulani, katika tukio hili pia hali hiyo imejitokeza tena kusesitiza suala la kukosa hadhi. Hali hiyo ilijitokeza baada ya kugundulika kuwa Kasim si mtoto halisi wa Bw. Hakimu Marjani, baada ya uchambuzi wa Bwana Msa juu ya warithi halali wa Bw. Hakimu. Mwandishi anaeleza yafuatayo:

Karibu wote pale hawakumuona Kasim alipoondoka kitini pake, na Speka Seif alipomzindua, Kasim alikuwa kaisha kufika mlangoni, anatoka. Kasim alisita kizingitini, akazunguka kuwatazama waliopo kwa unyenyenzi, unyanya wake umemtoka na nafasi yake sasa imekaliwa na unyonge. "Ah, Speka Seif, 'we,'" alijibu Kasim jawabu ya kukataa kwa sauti hafifu, dhaifu na dhalilifu... Nilikuwa nikidinda kwa dhati ya moyo wangu juu ya haki ya urithi wangu (uk. 96).

Mwandishi ametumia maneno kama 'hafifu', dhaifu na dhalilifu' kusesitiza namna alivyokuwa Kasim. Maneno hayo yana chimbuko la Kiarabu, yenye maana ya 'hafifu' nyepesi kutokana na neno '*khafif*', 'dhaifu' kutokuwa na uwezo katika

kufanya jambo kutokana na neno *'dhwaghiif'*, na *'dhalilifu'* unyonge kutokana na neno *'dhaliil'*. Hali hiyo ilimfanya Kasim ajutie kutokana na ufahari aliokuwa nao. Pia, mwandishi ametumia neno *'nikidinda na unyanya'* yenye chimbuko la lahaja ya Kiunguja mjini. Maneno hayo yana maana ya *'nikidinda'* kujigamba, na *'unyanya'* kuangukia pabaya baada ya ya kujifaharisha. Aidha, neno *'unyenzezi'* lina chimbuko la lahaja ya Kimakunduchi kumaanisha kutoona vizuri kutokana na mwanga hafifu au kuwa mbali na kitu chenyewe.

Katika tukio jingine lenye msamiati unaoakisi muktadha wa Kizanzibari ni hili ambalo linaonesha hali ya mapenzi aliyokuwa nayo Saleh juu ya mtoto wa Bw. Hakimu, Selume. Mwandishi anasema:

Saleh hakuweza kutambua: kuwa mapenzi yake yalikuwa ya kitabia ya binadamu, mtu mume kumpenda mwanamke, au kwa sababu Selume alikuwa na roho nzuri, Saleh hakuweza kuchanganua wala kupambanua (uk. 9).

Katika tukio hili kupitia nadharia ya uhalisia, utafiti umegundua kuwa mwandishi alikuwa mzalendo wa lugha ya jamii yake. Hakutaka kuibagua jamii yake kimaeneo. Msamiati kama *'mtu mume'* una uakisi na lahaja ya Kipemba, *'kuchanganua na kupambanua'* yana uakisi na lahaja ya Kiunguja mjini. Maana ya neno kama *'kuchanganua'* ni kufafanua sehemu za kitu zikaweza kutofautika na *'kupambanua'* ni kueleza tofauti ya vitu na vikaweza kufahamika. Ni maneno yenye kuleta mantiki moja ya kushadidia jambo lile lile linalomtanza Saleh juu ya mapenzi yake kwa Selume. Maneno hayo hayajabadilika maana wala matamshi. Aidha, chimbuko la neno *'mtu mume'* linathibitisha usawiri wa kazi yake na jamii yake kwa sababu neno hilo halikuwa na ulazima wa kulitumia wakati neno *'mwanamme'* linafahamika zaidi. Lakini kwa kuwa Muhammed Said Abdulla alitaka kuthibitisha dhamira yake ya

kuiakisi kazi hiyo na jamii yake, aliona ni vyema kulitumia neno 'mtu mume' kwa maana hiyo hiyo ya mwanamme.

Sambamba na hilo, ukurasa wa 32 ametumia neno 'ndume na nke' wakati Hakimu Marjani alipokuwa anawaomba dua Saleh na Selume baada ya kuwafungisha ndoa, kwa kusema:

"Lete mkono, baba," alisema Bw. Hakimu, huku akimtazama usoni. Wakapeana mikono, wakizuia hivyo hivyo kwa kitambo; kisha, "Mungu akubarikini nyote wawili, muishi kwa masikizano mema, 'mzae ndume na nke'. Amin.

Maneno hayo yanamaanisha 'mwanamme na mwanamke' kwa kuyafupisha huku yakiwa na chimbuko hilo hilo la lahaja ya Kipemba.

Tukio jingine ni hili ambalo mwandishi anaonesha masikitiko ya Bw. Hakimu juu ya mwanawe, Kasim, kwa kusema:

...lakini yote haya nimeyataka mwenyewe binafsi yangu; nilipokutunduwa hata sasa umekuwa mtundu; nikakuengaenga hata ukawa huwezi kutendekezeka; nikakutendea kila kitu, hata ukawa mpumbavu wa kutenda mwenyewe; nikakulisha tamu hata ukawa husubiri uchungu wa shubiri; nikakuendekeza hata ukawa hukinai; nikakudekeza hata ukawa hufai pesa mbili -a-ah, ama kweli, ajipigaye nafsi yake, asilie (uk. 5).

Hapa mwandishi ameteua msamiati wenye usambamba ili kuonesha utundu wake wa kucheza na lugha. Ni mbinu ambayo hupangilia maneno katika mgawiko wa mizani wenye kuchukua mapigo fulani katika uimarishaji wa mantiki inayotolewa. Pamoja na utundu huo, hakwenda kinyume na nadharia ya uhalisia inayosawiri kazi ya fasihi na jamii andikiwa. Usambamba wa msamiati wake aliyouonesha mtunzi ulisawiri na jamii andikiwa kupitia kipengele cha lahaja. Maneno yote yaliyopigiwa mstari yana chimbuko la lahaja ya Kiunguja Mjini. Etimolojia yake inasomeka kama 'nilipokutunduwa' lina maana ya kumfanya mtu akawa mtundu kwa asili ya neno

'utundu', 'nikakuengaenga' lina maana ya kumuangalia mtu katika hali ya uangalifu mkubwa kwa asili ya neno 'engaenga', 'kutendekezeka' lina maana ya kumkamilishia mtu kila kitu kwa asili ya neno 'tendekeza', 'mpumbavu' lina maana ya mtu mwenye uwezo mdogo wa akili, 'nikakuendekeza' lina maana ya kumridhisha mtu kwa kila analolitaka kwa asili ya neno 'endekeza', 'hukinai' lina maana ya mtu kutoridhika na chochote anachokipata kwa asili ya neno 'kinai' na 'nikakudekeza' lina maana ya kumfanyia mtu kila analolitaka kwa asili ya neno 'dekeza'. Maneno yote hayo yametumika bila ya kuongeza, kupunguza wala kubadilisha silabi.

Tukio jingine linaloonesha uakisi wa msamiati wa Kizanzibari limejitokeza katika ukurasa wa 11 wakati mwandishi anaonesha hali ya mchezo wa kamari na ushabiki wake kwa watalii. Mwandishi anasimulia haya:

Washabiki wa mchezo huo hufurahi sana wakifikiwa na washabiki watokao nchi za nje; kwani aghlabu ya watalii huwa ni watu wenye pesa za mwashege na kwa hivyo, wao hucheza kamari bila kimeme wala hawajutii kuliwa au kufutwa pesa zao... Lakini ashiki wa mchezo huo hayatii rohoni yote, anacheza kwa sababu bilisi kamzaini acheze tu. Pale barazani washabiki wamelaza miundi yao chini, wamekaa kama wanasali, taa ya kibatari iliyochochewa utambi imewekwa katikati yao. Wageni walikuwa wakicheza kwa uharara, moyo na ghera, wakikorokocha lugha ya kwao kama magolegole.

Hii ni hali mojawapo ya maudhui yenye mwelekeo wa kiuhalisia amabapo mwandishi wa kazi ya fasihi hakujienea fahari kukitumia Kiingereza eti kwa sababu kawatumia wahusika wazungu. Alikuwa anafahamu nini anakizungumza na kazi yake ni zao la jamii ipi na ndio maana akaweza kuyatumia maneno kulingana na usawiri wa jamii yake. Maneno yaliyopigiwa mstari kama 'mwashege, kimeme, kamzaini, wakikorokocha na magolegole' yana chimbuko la lahaja ya Kiunguja mjini, 'uharara' lina chimbuko la Kimakunduchi, 'wanasali na ghera' Kiarabu. Maana ya neno 'mwashege' ni kitu kisichoumiza, 'kimeme' tahadhari juu ya jambo,

'kamzaini' kamshawishi, 'wakikorokocha' kufanya kitu bila ya ujuzi nacho, na 'magolegole' ni aina ya ndege ambao huimba na kulia kuonesha hali ya kuhuzunika na kufurahisha kwa wakati mmoja. Aidha, neno 'uharara' lina maana ya uhakika wa jambo, 'wanasali' lina maana ya wamekaa kwa utulivu na unyenyekevu kama mtu anayefanya maombi kwa muumba wake likiwa na chimbuko la neno '*swalaat*' na 'ghera' lina maana ya moyo wa kuazimia kufanya jambo lenye chimbuko la neno '*ghazmu*'. Maneno hayo mwandishi ameyatumia bila ya kuyabadilisha silabi wala kuongeza.

Katika kuikamilisha kazi yake Bwana Msa juu ya kumkabidhi Speкта Seif mali ya Bw. Hakimu ni tukio jingine ambalo mwandishi ametumia msamiati unaoakisi mazingira ya Kizanzibari. Mwandishi anasimulia yafuatayo:

Kwa kila jiha, ni rahisi sana kukutuhumu, Bwana Msa, kwa wivi wa mali ya Hakimu Marjani, na kukufungisha kwa ushahidi wako mwenyewe. Wallahi, Bwana Msa, jambo moja tu linan'zuia nisikukamate sasa 'ivi n'kakupeleka stesheni. Lakini kwanza, hebu nihakikishe nini kilichomo katika madebe haya". "Uhakikishe nini, Speкта Seif," aliteta Bwana Msa, "na hakika yote iko kwangu? Hayo ndiyo mali ya Hakimu Marjani, hayageuki." Juu ya hayo, Speкта Seif alitoa kijembe madhubuti mfukoni mwake akatumia nguvu kidogo kuiambua risasi iliyolehemisha funiko la debe. Kubanduka risasi, funiko kwa ghafla lilitutumka kwa juu; na lilipofunuliwa, Speкта Seif na Najum walikodoa macho kushuhudia marobota kwa marobota ya manoti yameruhusiwa yakalaliana ndani ya debe. Speкта Seif hakuwa na haja ya kufungua debe la pili, alitosheka na lilile moja. Alitafuta ununu akaupuna, akalifunga lile debe lililotetereka... Waliondoka kimya kimya. Madebe hayakuwa mazito ya kumtopea mtu (uk. 73).

Tukio hili linakamilisha lile tukio la ukurasa wa 71 ambapo Bwana Msa alimpa uhuru Speкта Seif wa kumtukana, kumsubu na kumlaumu iwapo hakuikuta mali ya Bw. Hakimu katika pango. Katika kuhakikisha mali hiyo Speкта Seif, mwandishi ametumia msamiati kadhaa wenye uakisi na mazingira ya Kizanzibari kupitia lahaja zizungumzwazo Zanzibar na lugha za Kigeni. Maneno kama 'wivi, kuiambua,

iliyolehemisha, ununu, akaupuna, na kumtopea' yana chimbuko la lahaja za Zanzibar. Neno 'wivi' lina chimbuko la lahaja tatu, Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba kwa maana ya kuchukua kitu bila ya idhini ya mwenyewe. 'Akaupuna' lina chimbuko la lahaja mbili, Kimakunduchi na Kipemba kwa maana ya kupunguza maki ya unyunu ili uwe mlaini kwa matumizi na 'ununu' ni neno la Kipemba 'unyunu' lenye maana ya kamba inayotokana na ugubi wa kuti la mnazi. Maneno 'kuiambua, iliyolehemisha, na kumtopea' yana chimbuko la Kiunguja mjini. Maana zake ni 'kuiambua' kunyambua, 'iliyolehemisha' iliyogandisha kwa neno 'iliyolehenisha', na 'kumtopea' kukaa kwa mzigo mzito kichwani. Ama kwa upande wa maneno yenye chimbuko la lugha za Kigeni, tunakuta maneno kama 'jiha, kukutuhumu, wallahi, na marobota' yakiwa na chimbuko la Kiarabu na 'stesheni' Kiingereza. Maneno hayo yana maana ya 'jiha' upande maalum kwa neno la Kiarabu 'jihah', 'kukutuhumu' kukufanyia wasi wasi juu ya jambo kwa msingi wa neno 'tuhmat', 'wallahi' naapa na Mwenyezi Mungu kwa mantiki ya neno la Kiarabu 'wallahi', 'marobota' pesa zilizofungwa pamoja kwa neno la Kiarabu 'baalat', na 'stesheni' kituoni kwa chimbuko la neno la Kiingereza 'station'. Kulingana na utafiti juu ya mweka wa nadharia ya uhalisia ni kwamba kazi ya fasihi haimchoshi msomaji kutokana na ujenzi wa kazi hiyo kusawiri matukio halisi yaliyomo katika jamii kupitia wahusika na lugha wanayoitumia kama ambavyo matumizi ya lugha ya Muhammed Said Abdulla yalivyoisawiri jamii yake.

Katika ukurasa wa 87, mwandishi anaonesha mkanganyiko wa mawazo alioupata Spekta Seif katika uchambuzi wa Bwana Msa juu ya mali aliyoiacha Bw. Hakimu. Mwandishi anachambua haya:

Spekta Seif alitikisa kichwa “Bwana Msa” aliita Seif, nakuona umo kutafuta maneno yako, ukituzungusha huku ukitutolea kule, umekuwa

unatuendesha puta na myugwa wako mkononi husemi wewe ndiye nyakanga au mhenga, na mara nyingine ututolee kunga tusizoweza kuzifuata, na mara tena mizungu tusiyoweza kucheza. Kwa nini husemi kinaganaga?

Katika tukio hili mwandishi ametumia msamiati wenye chimbuko la lahaja ya Kiunguja mjini lakini ni msamiati ambao wakazi wa Zanzibar si mgeni katika mazungumzo yao ya kila siku. Katika kuonesha utajiri wa lugha ya jamii yake, Muhammed Said Abdulla ameyapanga maneno hayo katika mtiririko unaomvutia msomaji. Maneno kama 'puta' lina maana ya kuhangaika na kitu huku na huku, 'nyakanga' ni mtoa mafunzo katika ngoma za asili, 'mhenga' ni mzee wa zamani, 'kunga' ni mafunzo anayopewa mtu katika kumakinikia jambo fulani, 'mizungu' ni mbinu anazofunzwa mtu kwa siri katika kufanya jambo, na 'kinaganaga' ni kufafanua jambo wazi wazi. Maneno hayo ameyatumia mwandishi bila mabadiliko yoyote ya maana wala matamshi.

Jedwali 2: Muhtasari wa Msamiati Kutoka Katika *Duniani Kuna Watu* na Etimolojia Yake

Uk.	Neno	Asili Yake	Maana Yake	Chimbuko Lake	Maelezo
3	Machu-gachuga	Machu-gwachugwa	Hofu ya kufanya jambo	Kimakunduchi	Amepunguza silabi 'w'
3	Kujikisha	Osha	Kujiweka safi kwa maji	Kiunguja mjini	Halijabadilika
3	Masalheri	Masalheri	Habari za jioni	Kiarabu	Masaulkhair مساء الخير
3	Kujisafisha	Safisha	Kuondoa uchafu	Kiarabu	Swaafi صاف
3	Kujinadhifisha	Nadhifu	Kujiweka safi	Kiarabu	Nadhwiif نظيف

3	Kujito-harisha	Tohara	Kuondoa najisi au hadathi (kubwa na ndogo) katika mwili, nguo na pahala	Kiarabu	Twaharat طهارة
3	Sini	Sini	Miaka	Kiarabu	Sanat سنة
4	Aushi	Aushi	Maisha	Kiarabu	Aasha عاش
5	Nikaku-engaenga	Enga-enga	Kuangalia kitu au mtu kwa uangalifu mkubwa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
5	Kutende-kezeka	Tendekeza	Kamilisha kila kitu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
5	Nikaku-endekeza	Endekeza	Kumridhisha mtu kwa kila analolitaka	Kiunguja mjini	Halijabadilika
5	Hukinai	Kinai	Kuridhika na kitu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
5	Nikaku-dekeza	Dekeza	Kumfanyia mtu kila analopenda	Kiunguja mjini	Halijabadilika
5	Mpumba vu	Mpumba vu	Mtu mwenye uwezo mdogo wa akili	Kiunguja mjini	Halijabadilika
6	Faka	Faka au fwaka	Utulivu wa moyo	Kimakunduchi Kipemba	Halijabadilika au amepunguza silabi 'w'.
7	Bezo	Bezo	Dharau ya hali ya juu	Kitumbatu Kipemba	Halijabadilika
9	Kuchanganua	Changanua	kufafanua sehemu kwa	Kiunguja mjini	Halijabadilika

			kutofautisha		
9	Kupa- mbanua	Pamba- nua	Kueleza tofauti ya vitu na kufahamika	Kiunguja mjini	Halijabadilika
9	Mtu mume	Mtu mume	Mwanamme	Kipemba	Halijabadilika
10	Nibu	Nibu	Kipimo cha ulevi	Kiingereza	Nib
11	Wakako- rokocha	Koroko- cha	Kufanya kitu bila ya ujuzi unaosababisha uharibifu	Kiunguja mjini	Halijabdilika
11	Uharara	Harara	Uhakika wa kitu	Kimakunduchi	Halijabadilika
11	Magole- gole	Golegole	Jamii ya ndege wanaolia na kuhuzunika kwa wakati mmoja	Kiunguja mjini	Halijabadilika
11	Mwashe- ge	Mwashe- ge	Kitu kisichoumiza	Kiunguja mjini	Halijabadilika
11	Ghera	Ghera	Moyo wa kuazimia kufanya kitu	Kiarabu	Ghazmu عزم
11	Kimeme	Kimeme	Khofu ya kufanya jambo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
11	Kamzai- ni	Kuzaini	Kushawishi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
13	Siunga- mi	ungama	Kukubaliana na kitu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
14	Marisedi	Marisedi	Mahali pa kazi maalumu	Kiarabu	Makaanul mursal مكان المرسل
15	Zuhali	Zohali	Kuwa na usiri	Kipemba	Amebadilisha

			wa jambo		silabi 'o'
20	Akisafidi	Safidi	Kukamilisha kitu kwa manufaa	Kiarabu	Istifaada استفاد
21	Kumuanisi	Anisi	Kufariji	Kiarabu	Annasa أنس
32	Kumjuvya	Juvya	Kueleweshwa	Kimakunduchi Kitumbatu na Kipemba	Halijabadilika
32	Ndume, nke	Mwanamme na mwanamke	Jinsia mbili	Kipemba	Amefupisha
35	Kutunduwaa	Tunduwa au tunduwaa	Kubabaika na jambo kutokana na ubora wa jambo hilo	Kimakunduchi Kiunguja mjini	Ameongeza silabi 'a'.
36	Twezo	Twezo	Kutothamini	Kiunguja mjini	Halijabadilika
36	Sodawi	Sodai	Kuringa kutokana na maumbile au kipato	Kipemba	Ameongeza silabi 'w'
36	Izara	Izara	Fedheha	Kiunguja mjini	Halijabadilika
39	Sukumizo	Sukumizo	Laana	Kiunguja mjini	Halijabadilika
39	Afifilishwe	Fifilisha	Kufanya kitu kuwa hakipo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
39	Anyang'anywe	Nyang'anya	Kuchukua kitu kwa kutumia nguvu bila ya hiari ya mwenyewe	Kipemba	Halijabadilika

39	Adokole- we	Dokoa	Punguza	Kipemba	Halijabadilika
39	Wakim- karamkia	Kara- mbuka	Kuchangamka	Kiunguja mjini	Ampunguza silabi 'bu' na kuongeza 'i'
39	Kutaja- mali	Jamali	Kujipamba	Kiarabu	Jamiil جميل
39	Kamfa- dhili	Fadhili	Wema au hisani	Kiarabu	Fadhwala فضل
39	Nakama	Nakama	Maangamizo	Kiarabu	Naqamat نقمة
49	Bulibuli	Bulibuli	Kofia nyeupe yenye viua vya kufumwa kwa mkono	Kiunguja mjini	Halijabadilika
53	Mnoga	Mnoga	Tumbaku ya mgomba	Kiunguja mjini	Halijabadilika
56	Zili- chwea	Chwea	Kupita	Kimakunduchi	Halijabadilika
60	Vono	Vono	Kitanda cha siringi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
62	Anukulu	Nukulu	kunukuu	Kiarabu	Naklu نكال
63	Ghamu	Ghamu	Majonzi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
66	Kunisu- ta	Suta	Kumkadhibisha mtu mbele za watu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
66	Kunisu- suika	Susuika	Kutokubaliana na jambo	Kimakunduchi	Halijabadilika
66	Kunishu- tumu	Shutuma	Kutukana	Kiarabu	Shutmat شتمة
66	Mwivi	Mwivi	Mtu anayechukua kitu bila ya	Kimakunduchi Kitumbatu na Kipemba	Halijabadilika

			idhini ya mwenyewe		
66	Hutani-beua	Beua	Kutazama kwa dharau	Kiunguja mjini	Halijabadilika
67	Hakuka-siri	Kasirika	Kutopendeze-shwa na jambo	Kiunguja mjini	Ampunguza silabi 'ka'
67	Kuntajili	Tajili	Kutaja	Kitumbatu	Halijabadilika
68	Kupekenyua	Pekenyua	Chunguza	Kiunguja mjini	Halijabadilika
68	Uliobeta beta	Beta	Aina ya miale (beta)	Kiingeraza	Beta
69	Mapuuzza	puuzza	Kutojali katika kufanya jambo	Kitumbatu	Ameongeza silabi 'ma'
70	Ruya	Ru'uya	Ndoto	Kiarabu	Ru'uyat رؤية
71	Unitukane	Tukana	Kusema neno la kuudhi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
71	Nilamu	Laumu	Kumsuta mtu juu ya jambo fulani	Kiarabu	Lawwaamat لوامة
71	Nisubu	Nisubu	Kususuwa au kulaumu	Kiarabu	Sabakat سبكة
73	Ununu	Unyunu	Kamba inayotokana na ugubi wa kuti la mnazi	Kipemba	Ampunguza silabi 'y'
73	Akaupuna	Puna	Kupunguza maki ya unyunu ili uwe mlaini kwa matumizi	Kimakunduchi Kipemba	Halijabadilika
73	Kumtopea	Topea	Kukaa kwa mzigo mzito kichwani	Kiunguja mjini	Halijabadilika

73	Iliyolehemisha	Lehenisha	Gandisha	Kiunguja mjini	Amebadilisha silabi 'n' - 'm'
73	Wallahi	Allah	Naapana Mwenyezi Mungu	Kiarabu	Wallahi والله
73	Kuia-mbua	Nyambu-a	Kugandua	Kiunguja mjini	Ampunguza silabi 'ny'
73	Jiha	Jiha	Upande maalumu	Kiarabu	Jihat جهة
73	Marobota	Robota	Pesazilizofungwa pamoja	Kiarabu	Baalat بالة
73	Stesheni	Stesheni	Kituoni	Kiingereza	Station
73	Kukutuhumu	Tuhuma	Wasiwasi juu ya mtu	Kiarabu	Tuhmat تهمة
74	Aliyekwiba	Kuiba	Kuchukua bila ya idhini	Kiunguja mjini	Amebadilisha silabi 'u'
74	Jaha	Jaha	Bahati njema	Kiarabu	Majdu مجد
77	Kidogi	Kidogo	Kutokuwa kingi	Kiunguja mjini	Amebadilisha silabi 'o'
77	Mustahili	Astahili	Haki yake	Kiarabu	Mustahiil مستحيل
79	Porojo	Porojo	Maneno mengiyasioleta maana	Kiunguja mjini	Halijabadilika
79	Ufidhuli	Ufezuli	Tabia ya kutothamini watu wengine	Kipemba	Amebadilisha silabi 'e' na 'z' kuwa 'i' na 'dh'
80	Tufyate	Fyata	Kunyamaza kwa woga	Kiunguja mjini	Halijabadilika
80	Fadhaa	Fadhaa	Balaa ya mambo mazito au mshtuko	Kiarabu	Fadhawau فضاء

80	Ghabeni	Ghabeni	Mdanganyifu	Kiarabu	Ghabana غبن
81	Mikogo	Mikogo	Mbwembwe	Kiunguja mjini	Halijabadilika
81	Kujinyeta	Nyeta	Kujiona msafi na mzuri	Kiunguja mjini	Halijabadilika
81	Deko	Deko	Ringo au kutegemea kwa mtu	Kimakunduchi Kitumbatu	Halijabadilika
81	Kiburi	Kiburi	Hasira mbaya ambazo si tabia nzuri kuwa nazo mtu	Kiarabu	Kibri كبر
81	Aliikalifisha	Kalifisha	Kufanya jambo kwa kujilazimisha	Kiarabu	Yukallif يكلف
82	Manzili	Manzili	Nyumba	Kiarabu	Manzil منزل
84	Natija	Natija	Faida	Kiarabu	Natijjat نتيجة
87	Putu	Putu	Kuhangaika na kitu huku na huku	Kiunguja mjini	Halijabadilika
87	Kunga	Kunga	Mafunzo anayopewa mtu katika kumakinikia jambo fulani	Kiunguja mjini	Halijabadilika
87	Mizungu	Mizungu	Mbinu anazofunzwa mtu kwa siri katika kufanya jambo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
87	Nyaka-nga	Nyaka-nga	Mtoa mafunzo katika ngoma za kienyeji	Kiunguja mjini	Halijabadilika

87	Mhenga	Mhenga	Mzee wa zamani	Kiunguja mjini	Halijabadilika
87	Kinaganaga	Naganaga	Kufafanua jambo wazi wazi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
88	Zuti	Zuti	Zuzu au mpumbavu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
89	Nongwa	Nongwa	Kutosarifika	Kiunguja mjini	Halijabadilika
91	Mushkel	Mushkel	Wasiwasi wa kitu	Kiarabu	Mushkel مشكل
93	Humchaka	Hutaka	Kuhitaji kitu	Kimakunduchi	Halijabadilika
94	Akirendenda	Rendenda	Kusema bila kizuizi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
94	Kimeme	Kimeme	Woga au wasi wasi	Kipemba	Halijabadilika
94	Akiropoka	ropoka	Kusema bila kuulizwa	Kiunguja mjini	Halijabdilika
95	Kindaki-ndaki	Kindaki-ndaki	Halisi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
95	Adinasi	Nasi	Watu	Kiarabu	Nnasi الناس
96	Nikidi-nda	Dinda	kujigamba	Kiunguja mjini	Halijabadilika
96	Unye-nyezi	Unye-nyezi	Kutoona vizuri kutokana na mwanga hafifu au kuwa mbali	Kimakunduchi	Halijabadilika
96	Unyanya	Unyanya	Ubaya au kuangukia pabaya baada ya kujifaharisha	Kiunguja mjini	Halijabadilika
96	Hafifu	Hafifu	Nyepesi	Kiarabu	Khafiif خفيف

96	Dhaifu	Dhaifu	Kutokuwa na uwezo wa kufanya jambo	Kiarabu	Dhwaghiif ضعيف
96	Dhalilifu	Dhalili	Unyonge	Kiarabu	Dhaliil ذليل
97	Pumbao	Pumbao	Kujipumbaza	Kitumbatu	Halijabadilika
105	Taamuli	Taamuli	Kufanya kazi	Kiarabu	Ghamala عمل
105	Taib	Taib	Safi sana	Kiarabu	Twayyib طيب
110	Kazi-kweza	Kweza	Kusifia	Kiunguja mjini	Halijabadilika
111	Alimbi-bidia	Bibidia	Kuazima	Kiunguja mjini	Halijabadilika
112	Wame-barizi	Barizi	Pahala patulivu	Kiarabu	Baraz برز
113	Vilinge	Kilinge	Kikundi au pahala panapopungiwa mashetani	Kimakunduchi Kiunguja mjini	Halijabadilika
113	Tiara	Tiara	Kishada	Kiarabu	Twaairat طائرة
114	Kigeu-geu	Kigeu-geu	Kutokuwa na msimamo madhubuti	Kiunguja mjini	Halijabadilika
114	Kufidi	Kufidi	Kumjuilisha	Kiarabu	Afaada أفاد
115	Kiraru	Uraru	Hamu ya kitu	Kipemba	Halijabadilika
117	Madha-behi	Dhabehi	Nadhiri	Kiarabu	Tadhw-hiyat تضحية
117	Ilipota-mauka	Tamauka	Kukata tamaa	Kiarabu	Yaqnatwu يقنط

4.4.3 Matukio Yenye Msamiati Unaoakisi Mikdadha ya Kizanzibari na

Etimolojia Yake katika Riwaya ya Kosa la Bwana Msa

Tukio la kwanza limejitokeza katika kurasa 21 - 22 ambalo linaonesha hali iliyomtokezea Jamila baada ya Bwana Msa kutambua kuwa ameichana karatasi ya cheti cha ndoa yake. Mwandishi anasema:

Hiyo kazi imemfika Jamila! Kidogo alishangaa kama duwazi aliyeduwaa... Adhabu gani hii iliyomfika leo! Shamba kahiziwa, katukanwa, katishwa; mjini anatiwa soni na haya za uso. Mtu mmoja yeye - yote yamfike kwa siku moja! ..."Bi Jamila, nakuuliza. Nini maana ya kuichana karatasi ambayo ni nakala ya cheti cha ndoa, ndoa yako wewe na Bw. Ali bin Soud katika kijitabu chake kule ofisini kwa Shekhe Judi, kule Chwaka?" Jamila aliduwaa, akatunduwaa, akabumbuwaa, akashangaa, akapumbaa - yote kwa wakati mmoja. Kwa hakika, alikurubia kutaka kuzirai. Na mwisho, hana la kufanya, aliangua kilio akalia.

Hili ni tukio ambalo mwandishi, Muhammed Said Abdulla ametumia msamiati ambao maana zake zinakaribiana sana ili kuonesha usambamba wa msamiati hiyo. Kabla ya kuifafanua kwanza tuangalie maneno 'soni na duwazi' ambayo yana chimbuko la Kiunguja mjini. Maana ya 'soni' ni aibu inayompata mtu na kumsababishia kubabaika usoni, na 'duwazi' ni ugonjwa wa viungo vya mwili ambao husababisha kupoteza nguvu. Msamiati kama 'aliduwaa, akatunduwaa, akabumbuwaa, akashangaa na akapumbaa' yana maana zinazokaribiana. Msamiati hiyo ina chimbuko la lahaja za Zanzibar, ambapo maana inayotumika kwa neno moja katika lahaja moja inaweza kutumika maana hiyo hiyo kwa neno jingine katika lahaja nyingine. Mfano neno 'aliduwaa' lenye chimbuko la Kimakunduchi na 'akabumbuwaa' lenye chimbuko la Kiunguja mjini, yote yana maana ya kupigwa na mshangao au butwaa. Aidha, 'akashangaa' lina maana ya kustaajabu, 'akatunduwaa' kubabaika na jambo kwa chimbuko la Kiunguja mjini, na 'akapumbaa' kupungukiwa na akili kwa chimbuko la Kipemba. Maneno hayo yalitumika bila kubadilika maana zake wala matamshi.

Hali kama hiyo ya kutumia msamiati wenye maana zinazokaribiana, imejitokeza katika tukio ambalo linaonesha hali iliyomkuta Shekhe Judi baada ya Bwana Msa kumueleza kuwa amezesha ndoa ya kubuni kati ya Jamila na Bw. Ali bin Soud.

Mwandishi anaeleza haya:

Hebu fikiri mwenyewe. Wewe, kumwachia yeye kaingia afisini mwako, ndiko kutampa Jamila kichaa cha kuchana karatasi zako muhimu? Lakini, wewe mwenyewe, wewe binafsi yako, ndiye uliyempa kukichana cheti kile. Kilichompa kukichana cheti kile ni kukutoa wewe jiriwani!" "Audhubillah na majiriwa!" Sheha alitaka himaya kwa Mwenyezi Mungu. ...Sheha mzima hapo ulipo, mwenye dhamana kamili ya serikali, kwenda kukubali - kama fununu zinavyotangaza - kula mrungura kwa kumwoza mtu kwa jina la kubuni!..."Sawa maneno yako. Seyyid Ahmed bin Soud ndiye Bw. Ali bin Soud. Umewaozesha weye hapo ndoa ya kubuni, baina ya Ali bin Soud (ambalo ni jina la kubuni la Seyyid Ahmed bin Soud) na Jamila bint Farhan. Sheha aliduwaaa, akakaa tutwe, kahemewa, hana nafasi ya kutweta kwa mzigo mzito ulomlemea ukamlemeza (kur. 46 - 47).

Tukio hili mwandishi ameonesha msamiati kama 'jiriwani, majiriwa, audhubillah, na himaya' yenye chimbuko la lugha ya Kiarabu. Maana za maneno hayo ni 'jiriwani au majiriwa' uchukivu au chuki yenye chimbuko la neno '*jara-at*', 'audhubillah' najilinda na Mwenyezi Mungu kwa chimbuko la neno '*aghuudhubillah*', na 'himaya' mamlaka kwa chimbuko la neno '*himayat*'. Aidha, maneno kama 'fununu, mrungura, akakaa tutwe, kahemewa, kutweta, ulomlemea, na ukamlemeza' yana chimbuko la Kiunguja mjini. Maana ya maneno hayo ni 'fununu' habari zisizo za uhakika, 'mrungura' rushwa, 'akakaa tutwe' kukaa bila ya kusema chochote katika hali ya kuzubaa, 'kahemewa' kuzidiwa na mambo, 'kutweta' kuvuta pumzi kwa taabu, 'ulomlemea au ulomlemeza' kuzidi au kuzidisha uzito au nguvu upande mmoja wa kitu. Katika mustawa huo, Muhammed Said Abdulla hakuacha kucheza na msamiati kama ilivyo kawaida yake.

Tukio linaloonesha hali ya Bwana Ali baada ya kupewa maneno makali na Shekhe Judi limeundwa katika mtiririko wa visawe vyenye ukaribu wa maana kama linavyoonesha:

Ni vigumu kueleza hali aliyokuwa nayo Bwana Ali kwa kusikia maneno makali aliyopewa na sheha. Kusema alishangaa tu, hakutoshi; lakini aliduwaa, alitunduwaa, alipumbaa, alidumaa! Mradi hali zote hizo zilichanganyika pamoja katika kumchonga na kumduduka, zikamfanya yeye awe chochote kati ya dude na dufu na dudu... Bwana Ali alipoyakagua yote yaliyopita asubuhi ile, kutoka saa edashara mpaka thenashara, aliona kuwa yanatosha kumtia mtu wazimu. ...Mimi sipuuzi ubaya anaonitendea mtu; mimi nafuata mafunzo ya Kurani tukufu moja kwa moja - aliposema Mnyenzi Mungu 'Anayekutendeeni ubaya, mtendeeni ubaya kama alivyokutendeeni ubaya'. Sadakallahul Adhim." (uk. 66).

Msamiati 'aliduwaa, alitunduwaa, na alipumbaa' yameshaelezwa etimolojia yake katika tukio la ukurasa wa 22. Ama 'alidumaa' lina chimbuko la Kimakunduchi kutokana na neno 'dumaga' au Kipemba kutokana na neno 'dumaa' lenye maana ya kuwa mdogo. 'Kumchonga na kumduduka' ni maneno yenye maana ya kusawijika uso ukabadilisha hali na rangi ya asili ya mtu yenye chimbuko la Kiunguja mjini kwa asili ya maneno 'chonga na duduka'. 'Dude na dudu' yana chimbuko la Kipemba kwa maana ya jitu lisilo maana lisilofaa na 'dufu' mtu aliyezidiwa na mambo kwa chimbuko la Kiunguja mjini. Neno 'sipuuzi' linaonesha hali ya ukanushi kutokana na neno 'puuza' lenye chimbuko la Kitumbatu kwa maana ya kutojali katika kufanya jambo. 'Saa edashara, thenashara, na sadakallahul Adhim' yana chimbuko la lugha ya Kiarabu. Maana za maneno hayo ni 'saa edashara' saa kumi na moja linalotokana na neno '*Ithdaa ghashara saa*', 'thenashara' saa kumi na mbili '*Ithnaa ghashara saa*', na 'sadakallahul Adhim' amesema kweli Mwenyezi Mungu mtukufu kwa asili ya neno '*swadaqa llahul-ghadhwiim*'.

Mwandishi anatumia tena msamiati unaoakisi miktadha ya Kizanzibari katika kituo cha polisi cha Malindi wakati Spekta Seif anamuhoji Seyyid Ahmed juu ya kuvamiwa na Joka na Shoka na kumkosea kumuua wakati anaelekea Chwaka kumuona mkewe, Jamila. Mwandishi anaeleza yafuatayo:

Ulikuwa unakwenda wapi, hasa?" aliuliza Spekta Seif kwa mkazo. Seyyid Ahmed alisita, akapesapesa, akataataa, halafu akagoteza, "nilikuwa nakwe-nakwe-nda-nakwenda ch-Chwaka." "Usiku ule, Seyyid Ahmed?" Spekta Seif aliuliza, akimtizama mtu wake usoni. ...Seyyid Ahmed kimya. "Seyyid Ahmed," alimwonya Spekta Seif, "maswali yote niliyokuuliza hapa, wewe ama unayafifilisha au unayaviviza, huwezi au hutaki kuyajibu la kinaganaga, wala angalau sawa sawa tu. Sasa basi, utakuja kuyajibu maswali haya mbele ya korti tutakapokuchukua wewe kuwa ni shahidi wa polisi siku hiyo ya kesi ya wale watu wawili" (uk. 73).

Katika tukio hili mwandishi ametumia msamiati unaoashiria uzungumzaji usio wa kawaida kupitia neno 'akapesapesa, akataataa, na akagoteza'. 'Akapesapesa na akagoteza' yana chimbuko la lahaja ya Kiunguja mjini yenye maana ya kujitoa kimasomaso na kusema katika hali ya kukokoteza maneno. 'Akataataa na korti' ni maneno yenye chimbuko la lugha za Kigeni, Kiarabu 'akataataa' na Kiingereza 'korti'. 'Akataataa' lina maana ya kuangalia kitu kwa kuogopa linalotokana na neno '*qalika*', na 'korti' lina maana ya mahakama linalotokana na neno '*court*'. Ama 'unayafifilisha na unayaviviza' yana maana ya 'unayafifilisha' kufanya kitu kuwa hakipo kwa msingi wa lahaja ya Kiunguja mjini, na 'unayaviviza' kuyabadilisha mazungumzo kwa msingi wa neno la Kimakunduchi 'viviga' ambalo limebadilishwa silabi 'g' na kuwa 'z'.

Msamiati mwingine wenye usambamba wa visawe vya namna kama hiyo tunaupata katika kurasa 75 - 77 wakati mtunzi anaelezea hali ya Bi Shinuna baada ya kuwaajiri na kuwalipa kabisa Joka na Shoka katika kazi ya kumuua mumewe, Seyyid Ahmed. Pia, majibu ya Tunu kwa bibie juu ya hali aliyomkuta bwana wake

walipopishana njiani wakati anarudi kuwatafuta wauwaji kwa lengo la kuwauliza

kuwa kazi wameitekeleza. Mwandishi anaeleza hivi:

Tangu alipoondoka mumewe kwenda na safari yake, alfajiri giza giza, Bi Shinuna alikuwa na kiherehere, kukuru na kikaka. Mara ashike hiki aone sivyo, mara aende huku aone siko, Bi Shinuna alikuwa roho juu juu, hajui afanye nini. Kutwa siku ile alishinda na mashumshum ya fadhaa, akalala nayo... Tunu aliona kuwa mara tatu zinatoshwa, tafuta kutiliwa shaka bure, kuonekana ana maarubu fulani yanayompitisha pale... Lakini yeye alikuwa na akili yake hadhiri - siyo kama akili ya bwana wake iliyokuwa ikiranda na kupotea ughaibuni - na ukuta wa nyumba.. Nilipokuwa narudi - nafika Kiponda - nani bibie, nikakumbana naye kama si Bwana Mdogo?" "Aah? Huachi Tunu?" "Wallahi bibie," Tunu alishadidisha kwa kuapa. Tena tumekutana uso kwa uso, nusura tupigane vikumbo - kama mimi sikujibari nikajitenga. Lakini, hivyo tumekutana namna hiyo, yeye hakuniona; na kama kaniona, hakunitambua. Lakini kwa namna yenyewe, naweza kusema, hakuniona asili. Bwana Mdogo kabadilika, kafujika, kasawijika - kidogo kasoro, lakini Bwana Mdogo kawa kama Mshukunu Mafikira!

Hapa mwandishi anatuonesha hali iliyomtanza Bi Shinuna kwa kutumia msamiati 'kiherehere, kukuru, na kikaka' yenye chimbuko la Kiunguja mjini kuonesha udhaifu wa bibi huyo. Neno 'kiherehere' lina maana ya pupa na papara alizonazo mtu za kutaka kujua jambo, 'kukuru' ni neno lililofupishwa kutokana na neno 'kukuru kakara' lenye maana ya mvutano wa kutenda jambo, na 'kikaka' ni neno linalotokana na neno 'kikakaka' lenye maana ya kufanya jambo kwa kutumia nguvu. Hakuishia na maneno hayo tu aliongezea neno 'fadhaa' lenye chimbuko la Kiarabu kwa neno '*fadhawau*' likiwa na maana ya mzunguko wa mambo mazito yaliyomkaa mtu kichwanimwe. Maneno hayo yanasisitiza hali aliyokuwa nayo Bi Shinuna juu ya wahaka na wasiwasi kwa mumewe. Aidha, katika maelezo ya Tunu juu ya hali aliyomkuta bwana wake, mwandishi alitumia maneno kama 'maarubu, ughaibuni, wallahi, alishadidisha, nusura, sikujibari, na kabadilika' yenye chimbuko la Kiarabu, na 'kafujika na kasawijika' yenye chimbuko la Kiunguja mjini. Maana ya maneno hayo ni 'maarubu' kutafuta sababu kutokana na neno la Kiarabu '*mubarrir*',

'ughaibuni' ugenini kutokana na neno '*ghaib*', 'wallahi' kiapo juu ya muumba kutokana na neno '*wallahi*', 'alishadidisha' kukazia kitu ili kiaminike kutokana na neno '*ishtadda*', 'nusura' kupata msaada kutokana na neno '*nuswrat*', 'sikujibari' kujipa ukubwa kutokana na neno '*jabbar*', na 'kabadilika' kugeuka hali moja kuwa nyengine kutokana na neno '*baddil*'. Ama neno 'kusawijika' lina maana ya kuondoka kwa bashasha usoni na 'kafujika' lina maana ya kuchakaa kwa kitu au mtu, ni maneno yaliyotumika bila ya kubadilisha maana wala matamshi.

Tukio jingine lenye kuonesha mtindo wa maneno ya aina hiyo linapatikana pale Bi Shinuna anapombadilikia kwa ghafla mtumishi wake, Tunu baada ya kumueleza ukweli juu ya yaliotokezea wakati aliporudi kuwatafuta Joka na Shoka. Mwandishi anaeleza kuwa:

Nje huko umekwisha kunibazazi ukaniuza; na sijui umeniuza kwa kiasi gani, mwanamke weye! ...Tukirudi Chwaka, nataka uwe tayari wa kujitetea kwa kunitajia mtu mwingine, kama siye wewe, aliyenichongea polisi." Lakini bibie mimi sikukuchongea polisi," alikataa Tunu, akaonyesha kunywea kama siye yule. Bashasha yote ile aliyokuwa nayo kabla, iliyozalika kwa kujuana sana na bibi yake, na iliyokuwa juu ya mazoea makubwa baina yao - bashasha yote ile, kwa wakati mfupi tu, iliatilika, ikadhoofika, ikalika, ikatilifika (uk. 79).

Katika tukio hilo, msamiati kama 'iliatilika na ikadhoofika' yana chimbuko la Kiarabu, na 'ikalika na ikatilifika' yana chimbuko la Kiunguja mjini. Mwandishi alichanganya msamiati wenye chimbuko tofauti katika kuonesha hali ilivyombadilika Tunu mara moja tu baada ya kugeukwa na bibiye. Maana ya msamiati 'iliatilika' ni kuharibika kutokana na neno la Kiarabu '*ghatwlu*' na 'ikadhoofika' ni kuwa na unyonge kutokana na neno '*dhwaghiif*'. 'Ikalika' lina maana ya kumalizika kwa kitu baada ya kutumika sana na 'ikatilifika' lina maana ya kupata shida na kuishiwa na nguvu. Aidha, msamiati kama 'kunibazazi' una chimbuko la Kiarabu kutokana na neno '*bazza*' lenye maana ya kulaghai, na 'aliyenichongea au

sikukuchongea' yana chimbuko la Kiunguja mjini kwa maana ya kusema habari za mtu kwa mtu mwingine.

Katika ukurasa wa 107 mwandishi ametumia msamiati mwingine kabisa kuonesha hali ya furaha na majonzi kupitia Mwanatenga wakati anasoma barua kutoka kwa Jamila huku akigaragara kitandani. Mtunzi anaeleza:

Mwanatenga kaisoma barua ile na yeye kalala chali kitandani kwake. Alikuwa peke yake chumbani kule, lakini angalikuwapo mtu wa kumtazama, angalimwona namna uso wake ulivyokuwa ukipitiwa na migeuo ya dutu kufuata maendeleo yake katika kusoma barua ile - mara ulionyesha furaha; mara kicheko; mara ulisunza; mara ulisuta; mara ulipurukusha; mara ulisikitika, mambo kama hayo.

Msamiati unaoakisi mazingira ya Kizanzibari unaojitokeza katika tukio hilo ni 'migeuo, dutu, ulisuta, ulikurupusha, na ulisunza'. 'Migeuo' ni neno lenye chimbuko la Kipemba kupitia asili ya neno 'migeuzo' kwa kulipunguza silabi 'z' kwa maana ya kubadilisha. 'Dutu, ulisuta na ulipurukusha' ameyatumia bila ya kuyabadilisha, kuongeza wala kupunguza yakiwa na chimbuko la Kiunguja mjini. Maana zake ni 'dutu' uvimbe unaosababishwa na kufinga, 'ulisuta' kukemea kitu, na 'ulipurukusha' kusababisha matatizo. Ama 'ulisunza' ni neno linaloonesha hali ya faraja. Ni msamiati wenye chimbuko la Kipemba kwa maana ya kukinai au kuridhika.

Hali iliyomfika Seyyid Ahmed baada ya kupona maradhi ya wendawazimu aliyoyapata kutokana na masaibu ya kupotelewa na wake zake, ni tukio linalosimulia msamiati wenye kuakisi muktadha wa Kizanzibari. Mwandishi anaisimulia hali hiyo kama hivi:

Seyyid Ahmed bin Soud kabakia na jina tu kubwa kuliko yeye mwenyewe alivyo kwa hivi sasa, jina lenye haiba lakini kutwaza kwake - kama alivyo nako hivi sasa - na kwasi alizokuwa nazo zimetoweka, hanazo tena, kusalia yeye kula mwande na mkewe, Jamila kula mbwanda.

...japokuwa yeye, waonavyo wao, ni zuzu au dufu, au duba, au dudu, asiyefahamu kitu kinachokwenda pale. Lakini yeye, siku zote, yupo pale (kur. 121 - 122).

Tukio hilo limesimuliwa kupitia msamiati wenye chimbuko la Kiarabu kwa neno 'duba', Kiunguja mjini kupitia neno 'kutwaza, kwasi, mbwanda, na dufu', Kimakunduchi kwa neno 'mwande', na Kipemba kwa neno 'zuzu na dudu'. Maana zilizotumika juu ya maneno hayo ni 'duba' jitu lisilo akili kutokana na neno la Kiarabu '*dubu*', 'kutwaza' ukubwa au uongozi, 'kwasi' utajiri, 'mbwanda' chakula chenye lishe bora, 'dufu' mtu aliyezidiwa na mambo, 'mwande' uporo, 'zuzu' mtu mwenye uwezo mdogo wa kufahamu, na 'dudu' jitu lisilo maana lisilofaa. Hiyo ndiyo hali iliyomkuta Seyyid Ahmed baada ya kupona maradhi yake.

Katika ukurasa wa 48, mwandishi anatuonesha tukio kupitia tash-hisi kwa kuipa meza uwezo wa kulalama juu ya vyakula vitamu vilivyowekwa juu yake, vilivyoandalia siku ya kuitwa ugeni Aziz Akram nyumbani kwa Amanulla; anasimulia hivi:

Tena chakula chenyewe! Hicho hapo mezani! Hutapindukia mipaka kama utakisia kuwa hata ile meza nayo, nafasi ya meza, iliyoandikiwa juu yake chakula kile, ilikuwa ikikimezea mate na ikataasafu kimoyomoyo: "Laiti kama ningalikuwa na mdomo kama binadamu - kwa chakula hichi - kingenijia kijoyo kikanitia uchoyo na uroho, nikakila chote kabla wenyewe hawajaja kukila." Mabibi wa nyumbani, nakusudia Mwanatenga na Jamila, walikuwa kila mmoja chumbani kwake anajitengeneza na kujilabisi. ...ikazitoa dodo zake mbili Jamila zilizosimama zenyewe bila kutaka ule msaada wa ushaufu unaotolewa na kanchiri au sidiria;...

Malalamiko ya meza yalipambanua msamiati 'ikataasafu, uchoyo na uroho' yenye uakisi na mazingira ya Kizanzibari kupitia Kiarabu na lahaja ya Kiunguja mjini. Msamiati 'ikataasafu' lina maana ya masikitiko kutokana na neno la Kiarabu 'asafa'. 'Uchoyo na uroho' ni maneno yenye chimbuko la Kiunguja mjini yanayokaribiana sana maana zake lakini yanatofautika. Maana za maneno hayo ni 'uchoyo' tabia

mbaya ambayo mtu hutaka mwengine asipate au 'uroho' yeye apate kwa wingi kuliko mwengine. Aidha, kuna msamiati 'kujilabisi na kanchiri' uliopatikana wakati wa kuwaeleza Mwanatenga na Jamila wanavyojitayarisha wao binafsi katika ugeni wa Aziz Akram. Msamiati huo una chimbuko la Kiarabu kupitia maneno *'labisa na swidriyya'* yenye maana ya nguo na sidiria.

Msamiati mwingine umejitokeza katika tukio hili linalomuelezea Bi Shinuna alivyokuwa anafanya dharau wakati alipofika Chwaka nyumbani kwa Jamila na mapambano kati yake na Safinia kutokana na dharau hizo. Mwandishi anasimulia yafuatayo:

Gari la rangi ya kijani lilijimimina mpaka kizingitini pale walipo wao; akateremka; kwanza, bibi mmoja mweupe; na halafu akafuatiwa na mwingine hadharani. Bibi mweupe alisimama kuwakabili Safinia na Siajabu. Kwanza aliwatazama kwa urefu wa pua yake akiwaua. "Mimi sipigi hodi nyumba hii," alisema na uso kaubidia kuonyesha bera na twezo za udhilifu... "Huyo unayemwita kisononoko ni bibi wa kila 'mtamba na koko' kama wewe, wewe leo utaanana na mimi hapa, nikuweke sawa; maana weye si kifu yake yeye kuonana naye - weye, usiyejiwekea heshima, wala huijui heshima ni kitu gani ila kwa kwenda kwa watu wakakutukane. ...Wewe ungalikuwa mtu mkubwa katika dunia, lakini umejiharibia mwenyewe kwa kutakabari kwako. ...Wewe, kinyangaa, sasa hapo ulipo, ni duni kuliko paka wetu hapa nyumbani." Safinia aliyasema yale kwa ubaridi mkubwa ulioachana na uharara wa roho (kur. 82 - 83).

Hapa mwandishi ametumia msamiati unaoakisi miktadha ya lahaja za Zanzibar na lugha ya Kigeni. Maneno kama 'bera' lina chimbuko la Kitumbatu, 'twezo, wakitukane, na kinyangaa' yana chimbuko la Kiunguja mjini, na 'uharara' Kimakunduchi. Maana zake ni 'bera' upuuzi, 'twezo' ukubwa, 'wakitukane' kutoa maneno ya kuudhi mbele za watu, 'kinyangaa' mtu mwenye kudharauliwa kwa asili ya neno 'nyangau', na 'uharara' uhakika wa jambo. Ni maneno yaliyotumika bila ya kubadilika isipokuwa 'nyangaa' ambalo alibadilisha silibi 'a' badala ya 'u'. Pia, kuna maneno kama 'udhilifu, kifu, na kutakabari'. Maana ya maneno hayo ni 'udhilifu'

unyonge kutokana na neno 'dhaliil', 'kifu' kutosheleza kutokana na neno 'kaafi', na 'kutakabari' kutaka ukubwa au cheo kutokana na neno 'takabbar'. Maneno hayo yana chimbuko la Kiarabu ambayo kwa sasa yanatumika kama Kiswahili sanifu.

Tukio jingine lenye msamiati ni hili lililotoa taarifa kwa Mwanatenga na mumewe juu ya kuwasili Jamila Dar es Salaam na kijiandaa na mapokezi Zanzibar.

Mwandishi anaeleza haya:

Wakati ule ule alitokea Amanulla, amekwisha kuliweka gari lake bandani. "Manu, biashara yako uliyobashiri, hii hapa basi fetwa yake." Amanulla aliinamisha uso wake juu ya kikaratasi kile, akasoma: "*Nipo Dar. Kesho nakuja ndege ya saa nne. "Jamila"* (uk. 120).

Neno 'fetwa' linaakisi muktadha wa Kizanzibari kupitia neno lenye chimbuko la lugha ya Kiarabu 'fat-waa' lenye maana ya maamuzi. Katika tukio hilo, Mwanatenga anampa habari mumewe juu ya maandalizi ya mapokezi ya Jamila kuwasili Zanzibar.

Jedwali 3: Muhtasari wa Msamiati Kutoka katika Kosa la Bwana Msa na Etimolojia Yake

Uk.	Neno	Asili Yake	Maana Yake	Chimbuko Lake	Maelezo
1	Kujishaua	Shaua	Kujisifu mbele za watu ili wavutike nawe	Kiunguja mjini	Halijabadilika
1	Wajoli	Joli	Mtu asiyehuru	Kiingereza	Jail
2	Tao	Tao	Kufanya jambo katika muelekeo mzuri	Kimakunduchi Kipemba	Halijabadilika
8	Mbuya	Mbuya	Mwanamke wa mtu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
8	Ajinabi	Ajinabi	Mgeni	Kiarabu	Ajnabiyyi أجنبي

17	Akichu-zana	Chuku-zana	Kufuatana	Kiunguja mjini	Ampunguza silabi 'ku'
17	Kujidhili	Idhilali	Matatizo	Kiarabu	Idhlaal إدلال
19	Nitatawakkal	Tawakkal	Kujiegemeza	Kiarabu	Tawakkal توكل
20	Hoshi	Hoshi	Kitambaa chepesi chenye nakshi mchanganyiko	Kipemba	Halijabadilika
20	Dume	Dume	Kiumbe chenye jinsia ya kiume	Kimakunduchi	Halijabadilika
21	Soni	Soni	Aibu inayompata mtu na kubabaika usoni	Kiunguja mjini	Halijabadilika
21	Duwazi	Duwazi	Ugonjwa wa viungo vya mwili	Kiunguja mjini	Halijabadilika
22	Dia	Dia	Mpenzi	Kiingereza	Dear
22	Akashangaa	shangaa	Kustaajabu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
22	Akabumbuwaa	Bumbu waa	Mzubao au butwaa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
22	Akapumba	Pumbaa	Kupungukiwa na akili	Kipemba	Halijabadilika
25	Kiduhushi	Kiduhushi	Mbeya	Kipemba	Halijabadilika
26	Chechei	Chechei	Maamkizi ya watu waliokuwa hawajapitana sana kiumri	Kipemba	Halijabadilika
26	Kufu	Kufu	Ulinganifu	Kiunguja mjini	Halijabadilika

			katika hadhi za watu		
26	Mafamba	Mafamba	Kufanya jambo kwa kubahatisha	Kimakunduchi	Halijabadilika
27	Kidimu	Kidimu	Kuku mwenye mbawa zilizosimama	Kiunguja mjini	Halijabadilika
27	Kidiku	Diku	Jogoo kishingo	Kiarabu	Diiku ديك
36	Ikakufutini	futu	Kupita kutokana na muda	Kiunguja mjini	Amebadilisha silabi 'u'
36	Mkafaitika	Faitika	Kujisahau	Kiunguja mjini	Halijabadilika
37	Alimlaki	Laki	Alikutana naye	Kiarabu	Laqaa لقي
41	Yaya	Yaya	Mwanamke anayetunza watoto kwa malipo	Kipemba	Halijabadilika
44	Kukoro-weza	Koroweza	Kumharibia mtu jambo lake	Kipemba	Halijabadilika
45	Maganjo	Maganjo	Sehemu iliyohamwa ambayo ilikuwa ni makazi ya watu	Kiunguja mjini Kipemba	Halijabadilika
46	Fununu	Fununu	Habari zisizo za uhakika	Kiunguja mjini	Halijabadilika
46	Himaya	Himaya	Mamlaka	Kiarabu	Himayat حماية
46	Audhubillah	Aghudhubillah	Najilinda kwa Mwenyezi Mungu	Kiarabu	Aghuudhubillah أعوذ بالله
46	Mrungura	Mrungura	Rushwa	Kiunguja mjini	Halijabadilika

46	Jiriwani	jiriwa	Uchukivu	Kiarabu	Jara-at جراءة
47	Kaheme-wa	Emewa	kuzidiwa	Kiunguja mjini	Ameongeza silabi 'h'
47	Akakaatutwe	Tutwe	Kukaa bila ya kusema chochote katika hali ya kuzubaa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
47	Kutweta	Tweta	Kuvuta pumvi kwa taabu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
47	Ulomlemea	Elemea	Kuzidi uzito kwa kitu upande mmoja kuliko mwingine	Kiunguja mjini	Ampunguza silabi 'ue' baina ya 'm' na 'l'
47	Ukamlemeza	Elemeza	Kuzidisha uzito au nguvu upande mmoja	Kiunguja mjini	Ampunguza silabi 'ue' baina ya 'm' na 'l'
48	Ikataasafu	Asafa	Kusikitishwa	Kiarabu	Asafa أسف
48	Uchoyo	Choyo	Tabia ya kutaka mwingine asipate	Kiunguja mjini	Halijabadilika
48	Uroho	Uroho	Tabia ya kutaka mtu apate kwa wingi kuliko mwingine	Kiunguja mjini	Halijabadilika
48	Kujilabisi	Labisa	Nguo	Kiarabu	Labsu لبس
48	Kanchiri	Kanchiri	Sidiria	Kiarabu	Swidriyyat صدرية
49	Kujitongoa	Tononoka	Kuingia mwili au kunenepa	Kimakunduchi	Amebadilisha neno 'noka'
50	Mbeja	Mbeja	Mwanamke maridadi	Kiunguja mjini	Halijabadilika

50	Mzumbao	Zubaa	Kustaajabia kitu na kuduwaa	Kiunguja mjini	Ameongeza silabi 'm'
51	Nakisi	Nakisi	Pungufu	Kiarabu	Naaqisw ناقص
53	Kutuzuga	Zuga	Kumfanyia ubaya mtu	Kimakunduchi	Halijabadilika
54	Kalili	Kalili	Kudogosheka kwa kitu au mtu	Kiarabu	Qaliil قليل
59	Joko	Joko	Balaa	Kilatini	Jock
65	Jaka	Jakamo yo	wasiwasi	Kipemba	Ampunguza neno 'moyo'
66	Alidumaa	Dumaa au duma-ga	Kuwa mdogo	Kipemba Kimakunduchi	Halijabadilika au amepunguza silabi 'g'
66	Dudu, dude	Dudu	Jitu lisilo maana, lisilofaa	Kipemba	Amebadilisha silabi 'u' katika dude
66	Dufu	Dufu	Mtu aliyezidiwa na mambo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
66	Thenasha-ra	Ithnaa-ghasha-ra	Saa kumi na mbili	Kiarabu	Ithnaa-ghashara saa إثنا عشرة ساعة
66	Sadakallahul Adhim	Swada-qallahul-ghadhwiim	Amesema kweli Mwenyezi Mungu mtukufu	Kiarabu	Swadaqalla hul-ghadhwiim صدق الله العظيم
67	Hariji	Hariji	Kutumia pesa kwa matumizi ya nyumbani	Kiunguja mjini	Halijabadilika
68	Kustaladhi	Staladhi	kupendezewa	Kiarabu	Istaladha استلذ

72	Mang'a-mung'amu	Mang'a mung'amu	Machofu yaliyotokana na kazi nyingi au usingizi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
73	Akapesa-pesa	Pwesa-pwesa	Kujitoa kimasomaso	Kiunguja mjini	Amepunguza silabi 'w'
73	Akagoteza	Goteza	Kusema kwa kukokoteza maneno	Kiunguja mjini	Halijabadilika
73	Unayavi-viza	Viviga	Kubadilisha	Kimakunduchi	Amebadilisha silabi 'g'
73	Akataataa	Taataa	Kuangalia kwa kuogopa	Kiarabu	Qaliqa قلقى
73	Korti	Korti	Mahakama	Kiingereza	Court
75	Kiherehere	Kiherehere	Pupa na papara za mtu kutaka kujua jambo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
75	Kukuru	Kukuru kakara	Mvutano katika kutenda jambo	Kiunguja mjini	Amepunguza neno 'kakara'
75	Kikaka	Kikaka ka	Kufanya jambo kwa nguvu	Kiunguja mjini	Amepunguza silabi 'ka'
75	Maarubu	Maaru bu	Sababu	Kiarabu	Mubarrir مبرر
75	Ughaibuni	Ghaibu	Ugenini	Kiarabu	Ghaaib غائب
77	Nusura	Nusura	Kupata msaada	Kiarabu	Nuswrat نصره
77	Sikujibari	Jabari	Kujipa ukubwa	Kiarabu	Jabbar جبار
77	Alishadishia	Shadi-dia	Kukazia kitu ili kifanyike	Kiarabu	Ishtadda اشتد
77	Kasawijika	Sawijika	Kuondoka bashasha usoni	Kiunguja mjini	Halijabadilika
77	Kafujika	Fujika	Kuchakaa	Kiunguja mjini	Halijabadilika
77	Kabadili-	Badili	Kugeuka kwa	Kiarabu	Baddil بدل

	ka		maumbile		
79	Sikukuch ongea	Cho- ngea	Semea	Kiunguja mjini	Halijabadilika
79	Ikalika	Lika	Kumalizika kwa kitu mfano jembe au kiatu kutokana na kutumika sana	Kiunguja mjini	Halijabadilika
79	Ikatilifika	Tilifika	Kupata shida na kuishiwa na nguvu	Kiunguja mjini	Halijabadilika
79	Iiatilika	Atilika	Kuharibika	Kiarabu	Ghatwlu عطل
79	Kunibaza- zi	Bazazi	Kulaghai	Kiarabu	Bazza بز
82	Bera	Bera	Upuuzi	Kitumbatu	Halijabadilika
82	Udhilifu	Dhalili	Unyonge	Kiarabu	Dhaliil ذليل
82	Kifu	Kifu	Kinatosheleza	Kiarabu	Kaafi كاف
83	Kinya- ngaa	Nya- ngau	Mtu mwenye kudharauliwa	Kiunguja mjini	Amebadilisha silabi 'a'
83	Kutakaba- ri	Takaba ri	Kutaka ukubwa	Kiarabu	Takabbar تكبر
84	Ewala	Ewala	Mambo yamekuwa sawa	Kiarabu	Huwallah هو الله
84	Ghairi	Ghairi	Isiyokuwa hiyo	Kiarabu	Ghairi غير
95	Kutaarafu	Arafu	Kujua	Kiarabu	Gharrif عرف
105	Payo	Payo	Mahali hapo	Kitumbatu	Halijabadilika
105	Mumiani	Mumia ni	Mganga wa dawa za kienyeji	Kijerumani	Medizinmann
107	Migeuo	Geuza	Badilisha	Kipemba	Amepunguza silabi 'z'
107	Dutu	Dutu	Uvimbe ufanyikao usoni	Kiunguja mjini	Halijabadilika

			kwa sababu ya kufinga		
107	Ulipuru-kusha	Puruku-sha	Kusababisha matatizo	Kiunguja mjini	Halijabadilika
107	Ulisunza	Sunza	Kinai, ridhika	Kipemba	Halijabadilika
109	Rakadha	Rakadha	Kujitutumua	Kiarabu	Raqadha رقص
110	Alighilibika	Ghilibu	Kuhadaika	Kiarabu	Ghalab غلب
118	Alimnabihisha	Tanabahi	Kujua	Kiarabu	Tanbiih تنبيه
120	Fetwa	Fat-wa	Maamuzi	Kiarabu	Fat-waa فتوى
121	Kwasi	Kwasi	Mali au utajiri	Kiunguja mjini	Halijabadilika
121	Mwande	Mwande	Uporo	Kimakunduchi	Halijabadilika
122	Mbwanda	Mbwanda	Chakula kizuri chenye lishe	Kiunguja mjini	Halijabadilika
122	Zuzu	Zuzu	Mtu mwenye uwezo mdogo wa kufahamu	Kipemba	Halijabadilika
122	Ima faima	Ama	Kusemea kitu kwa kuweka suluhisho mbili au zaidi	Kiarabu	Imma faimma إماما
122	Duba	Duba	Jitu lisilo akili	Kiarabu	Dubu د ب
124	Kusowera	Sowera	Kucheza ngoma kwa kunegua	Kiunguja mjini	Halijabadilika
127	Kutanza	Tanza	Kutofahamika kwa urahisi	Kiunguja mjini	Halijabadilika
128	Maghafira Ghafuru	Ghafara	Kusamehe	Kiarabu	Ghafara غفر
128	Rahimu	Rahimu	Mwenye	Kiarabu	Arrahiim

			kurehemu		الرحيم
129	Anighufi- rie	Ghafara	Kusamehe	Kiarabu	Ghafara غفر

Kwa ujumla, utafiti huu umegundua kuwa matumizi ya msamiati unaoakisi mazingira ya Kizanzibari katika riwaya hizo tatu teule haukutofautiana chimbuko lake. Riwaya zote zimechanganya maneno kutoka katika lahaja na lugha za Kigeni kama historia ya jamii yenyewe inavyobainika. Aidha, tunaporudi katika mihutasari ya orodha yenye msamiati unaoakisi mazingira ya Kizanzibari, utafiti umegundua matumizi ya msamiati wenye chimbuko la Kiarabu ni mwingi mno kuliko lugha nyengine za Kigeni. Pia, takribani asilimia za maneno yenye chimbuko la lahaja za Zanzibar na yenye chimbuko la lugha ya Kiarabu yanakaribiana. Hii inatokana na kuwa, Waarabu na utamaduni wenye silka ya dini ya Kiislamu umeathiri sana Wazanzibari na kwa hivyo, hata katika hali ya kawaida ni nadra kumuona Mzanzibari ameweza kukwepa maneno yenye chimbuko la Kiarabu.

Hata hivyo, utafiti umegundua kuwa, matukio mengi ambayo mwandishi anaonesha hali ya kughumiwa, hasira, masikitiko, dharau, masaibu, ugomvi na wasiwasi hutumia msamiati wenye chimbuko la lahaja zilizopo Zanzibar. Kwa mfano, msamiati kupitia matukio yanayoonesha hali ya kughumiwa katika *Kosa la Bwana Msa* ni (akashangaa, akabumbuwaa na akapumbaa) kwa Jamila katika ukurasa wa 22, (kahemewa, akakaa tutwe, kutweta, ulomlemea na ukamlemeza) kwa Shekha Judi katika ukurasa wa 47, na (alidumaa, dudu, dude na dufu) kwa Bwana Ali katika ukurasa wa 66. Pia, hali inayoonesha masikitiko katika *Duniani Kuna Watu* ni (nikakuengaenga, kutendekezeka, nikakuendekeza, hakinai, nikakudekeza, na mpumbavu) kwa Hakimu Marjani katika ukurasa wa 5, na hali ya hasira ni (twezo,

sodawi na izaru) kwa Selume katika ukurasa wa 36. Aidha, mara nyingi mwandishi amependelea kutumia msamiati wenye chimbuko la Kiarabu kuonesha hali ya udhaifu na unyonge. Kwa mfano, msamiati kupitia matukio yanayoonesha hali ya udhalili katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* ni (nakama na sukumizo) kwa Kasim katika ukurasa wa 39, (kiburi, ufidhuli, deko, unyarafu na usodawi) katika ukurasa wa 81 na (hafifu, dhaifu na dhalilifu) katika ukurasa wa 96. Vile vile, katika masuala yanayoambatana na dini, Muhammed Said Abdulla alitumia msamiati unaoenda sambamba na tendo lenyewe. Kwa mfano, katika *Duniani Kuna Watu* ukurasa wa 3, mwandishi alitumia maneno kama (kujisafisha, kujinadhifisha na kujitoharisha) wakati anaeleza matayarisho ya Hakimu Marjani ya kutekeleza ibada ya swala. Pia, katika masuala yanayoambatana na mila na desturi za wakazi wa Zanzibar kama vile masuala ya mashetani na kuchagawa, mwandishi ameonesha uakisi kupitia lugha zao za kijadi. Kwa mfano, katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* kurasa 11 - 12 anamuonesha mama Kipwerere jinsi alivyoshughulika kumuuguza mwanawe. Katika kumuuguza huko, mwandishi anaeleza kuwa alikuwa akitamka maneno ama yenye asili ya Kipemba cha ndani au Kimakunduchi ambayo mtu hawezi kuyafahamu. Tendo hili linatilia msisitizo uakisi wa msamiati na mazingira ya Kizanzibari kwani linaonesha uhalisia ulivyo juu ya wakazi hao.

Jambo jingine ambalo limegundulika katika utafiti huu ni umahiri wa matumizi ya visawe vyenye kuonesha usambamba wa maana zake. Hili linamaanisha kwamba Muhammed Said Abdulla alikuwa ni mtundu katika uundaji wa lugha na mweledi sana wa lugha yake. Katika upande wa kubadilisha maneno ama kwa kupunguza au kuongeza silabi, mwandishi ameonesha umahiri mkubwa. Utafiti huu umegundua kuwa, hali hiyo imetokana na kuitaka hadhira ipate urahisi wa kusoma kwa

kukatisha baadhi ya maneno, kupunguza au kuongeza silabi. Mfano wa maneno ambayo mwandishi ameyakata katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* ni kukuru badala ya kukuru kakara (ukurasa wa 75), kikaka badala ya kikakaka (ukurasa wa 75), na jaka badala ya jakamoyo (ukurasa wa 65). Aidha, katika kupunguza silabi, mwandishi amepunguza maneno kama akapesapesa badala ya akapwesapwesa (ukurasa wa 73), akichuzana badala ya akichukuzana (ukurasa wa 17) katika *Kosa la Bwana Msa*. Pia, katika *Duniani Kuna Watu* maneno kama ununu badala ya unyunu (ukurasa wa 73), hakukasiri badala ya hakukasirika (ukurasa wa 67), wakimkaramkia badala ya wakimkarambukia (ukurasa wa 39), na machugachuga badala ya machugwachugwa (ukurasa wa 3). Pia, katika *Mzimu wa Watu wa Kale* maneno ametafarika badala ya ametafranika (ukurasa wa 36), na baraste badala ya barasite (ukurasa wa 6).

Zaidi ya hayo, kuna jambo jingine la kipekee kuhusu usawiri wa msamiati kupitia mhusika. Utafiti umegundua kuwa mtunzi alikuwa anapendelea sana kuchanganya msamiati wenye chimbuko tofauti. Hii inaakisi uhalisia wake katika kumjenga mhusika Bwana Msa, dhamira anazofikisha na uhusika wake wa kuchunguza na kudadisi masuala yote yanayojiri ndani ya riwaya hizo. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* (ukurasa wa 66) alipokuwa akitoa majibu juu ya sifa alizopewa na Spekta Seif anasema:

Spekta Seif! Sijui kama hivyo ndiyo katika jumla ya kunisifu au ndiyo namna yako ya kunisusuika, kunishutumu na kunisuta.

Pia katika ukurasa wa 71 alipokuwa anasisitiza kuhusu mali iliyomo katika pango anasema:

Wewe ingia katika pango na utoke hukupata kitu, halafu nilaumu, nisubu, unitukane utakavyo - bali nenda kwanza.

Hayo ni matukio yenye msamiati wenye chimbuko la Kiarabu na kidogo lahaja.

4.5 Athari za Msamiati Unaoakisi Miktadha ya Kizanzibari Katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla kwa Wasomaji

Muhammed Said Abdulla ni mtunzi wa zamani lakini hadhi yake inayotokana na uzuri wa kazi zake inamfanya kutambulika na kuenziwa kila leo. Inaonekana kama ni mtunzi wa kisasa kwa jinsi ambavyo anatajwa na kutumika vyema kwa vitabu vyake katika ngazi mbalimbali za elimu hapa nchini na Afrika Mashariki kwa ujumla. Utajiri wa kazi zake upo katika umbo na muundo mzima wa kazi hizo kuanzia lugha, wahusika na uhusika wao, mandhari, na maudhui ya kazi zenyewe. Ni kazi zilizotungwa kwa ubunifu mkubwa wenye kila aina ya uhalisia wa jamii andikiwa.

Utafiti huu umegundua kuwa mtunzi huyu hatajiki kwa elimu kubwa lakini ni ya ghali kwa watu wengi. Akipenda sana kusoma vitabu vya hadithi vya lugha tofauti kama vile Kiswahili, Kiingereza na Kiarabu. Hili lilimfanya awe ni mjuzi wa lugha zaidi ya moja na kuathirika na kile anachokisoma. Kwa maoni ya mtafiti, katika usomaji wa vitabu vya hadithi vya Kiswahili, Muhammed Said Abdulla aliathiriwa na uandishi wa Shaaban Robert kupitia falsafa ya maneno yake. Maneno ya Shaaban Robert ni yenye hekima, busara na ubunifu mkubwa wa kuweza kuyapatia maana zake. Jambo hilo lilimuathiri sana Muhammed Said Abdulla. Kwa mfano katika riwaya yake ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, anasema:

Shibe kamwamini Njaa, na kwa hiyo kampa chakula amwekee. Lakini Njaa alipomwona Shibe kaondoka, alikiangamiza chakula chote tumboni mwake (uk. 2).

Maneno hayo yanaleta tafsiri ya kisa chenyewe. Kisa cha riwaya hiyo kinatafsirika kuwa Shibe ni mzee wa Ahmed (Bwana Yunus) na Njaa ni Bwana Ali. Sasa ufafanuzi unakuja hivi, Bwana Yunus alimpata Ali na kumlea kwa kumfanya mtoto wa nyumbani na kumuamini kwa kila kitu wakati wakiishi Kongo. Baada ya

kushikwa na ugonjwa Bwana Yunus, mali yake yote alimkabidhi Ali. Ali aliuza mali yote na akafunga safari ya kuja Unguja kwa ajili ya matibabu ya mzee wake. Mzee huyo alifurahi sana na alimkamilishia mali yote Ali, na akamtaka pindi akifariki, amlee mwanawe Ahmed hadi awe mkubwa kisha amkabidhi mali yake. Lakini la ajabu, baada ya kufariki Bwana Yunus, Bwana Ali kamgeuka Ahmed. Mali ameifanya kuwa ni yake na kuiyonea uchungu kiasi ambacho hakumtambulisha Ahmed kuwa ni mali aliyorithishwa kutoka kwa baba yake, Bwana Yunus. Hapo ndipo fasiri ya Shibe kumwamini Njaa na kumpa chakula amwekee ilipotokea. Lakini, uaminifu ulikwisha pale alipokiingamiza chakula chote yaani Bwana Ali kujimilikisha mali yote ambayo si yake. Katika kuyakamilisha maneno yake yenye hekima, Muhammed Said Abdulla alisema:

Nadhani waandikaji magazeti walikosea kukiita kisa hicho cha Bwana Ali *Mzimu wa Watu wa Kale* - wangelipiga ndipo kama wangelikiita Njaa iliyoshibishwa! (uk. 5).

Yaani, uchu wa Bwana Ali wa kuivizia mali ya Bwana Yunus na hatimaye kuipata.

Athari ya utumiaji wa maneno ya namna kama hiyo kwa mwandishi huyo inatokana na utunzi wa Shaaban Robert. Kwa mfano, katika riwaya ya *Kusadikika*, Shaaban Robert anasema:

Tone moja la maji haliwezi kuleta gharika katika nchi. Tone dogo la maji, lile nililolidhania kuwa litakauka wenyewe mara moja, limekuwa mlizamu wa kuwafariji kwa siri wanafunzi wa mshtakiwa! (uk. 2). Maisha huwaficha watu wake bora mpaka tukio kubwa litokee (uk. 12).

Uchanganuzi wa maneno hayo unatokana na mantiki ya kisa kilichomo ndani ya riwaya ya *Kusadikika* juu ya mhusika wake mkuu, Karama. Karama alikuwa ni mhusika mshtakiwa wa serikali ya Kusadikika ambaye alishtakiwa kwa kosa la kufundisha raia elimu ya Uanasheria. Hivyo, mtunzi ameyatumia maneno hayo katika muktadha wa kuonesha dharau kwa viongozi wa nchi hiyo juu ya

kutofanikiwa kwa mpango aliyouanzisha Karama kutokana na hadhi duni aliyonayo. Ghafla mambo yalibadilika. Dhana ya viongozi wa Kusadikika ya kumshinda mshtakiwa imewageukia wenyewe. Hatimaye, Karama kufichua siri zote za Kusadikika. Siri hizo, zilisababisha kuokoa maisha ya wajumbe sita ambao walikuwa tayari ni mahabusu na Karama kuibukia kuwa mtu muhimu wa nchi hiyo.

Pia, suala la uumbaji wa wahusika ni athari nyingine ya Muhammed Said Abdulla aliyoiipata kutoka kwa Shaaban Robert. Muhammed Said Abdulla ametumia wahusika vielelezo kwa kuwapa majina kulingana na uhusika wao. Fasiri ya majina ya wahusika hao kwa Kiarabu yana maana ya yale matendo yao. Kwa mfano, mhusika kama Ahmed katika *Mzimu wa Watu wa Kale*; Jamila na Aziz Akram katika *Kosa la Bwana Msa*; na Saleh, Hakimu, Selume na Kasim katika *Duniani Kuna Watu*. Majina hayo yamejiegemeza katika muktadha wa kidini kama inavyofafanuliwa hapo chini:

Ahmed ni jina lenye asili ya neno حمد (*hamida*) lenye maana ya sifa njema. Na katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, Ahmed amepewa wasifu wa mtoto mzuri au mwema. Jamila ni jina lenye asili ya neno جميل (*jamiil*) lenye maana ya kujipamba. Katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*, Jamila ni mhusika aliyepewa uzuri wa sura na tabia. Aziz ni jina lenye asili ya neno عزيز (*ghaziiz*) lenye maana ya tukufu. Katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*, mhusika huyu alipewa sifa ya utukufu sana. Hakimu ni jina lenye asili ya neno la Kiarabu حكيم (*hakiim*) lenye maana ya mwenye kutoa hukmu. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, mhusika huyu amebeshwa wasifu wa kutoa hukmu inayofaa juu ya warithi wake halali wenye haki ya kumrithi. Saleh ni jina lenye asili ya neno صالح (*swaalihu*) yaani mwema. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, mhusika Saleh amewakilisha kijana mwema, mwenye huruma, upendo

na ukweli. Kasim ni jina lenye asili ya neno قسم (*qismu*) lenye maana ya kigawanyo. Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, mhusika huyu amebeba sifa ya kupigania agawiwe mali ambayo ilikuwa haimuhusu.

Majina hayo yana usambamba na majina ya wahusika wa Shaaban Robert kama vile Karama, Buruhani, na Fadhili katika *Kusadikika*, Adili katika *Adili na Nduguze* na Radhia katika *Utubora Mkulima*. Karama ni jina lenye asili ya neno la Kiarabu كريم (*kariim*) lenye maana ya tukufu. Katika riwaya ya *Kusadikika*, mhusika huyu ni mkarimu na mwenye mambo mengi mazuri kama vile kauli nzuri na roho nzuri. Buruhani ni jina lenye asili ya neno برهان (*burhaan*) lenye maana ya ishara au alama. Katika riwaya ya *Kusadikika*, Buruhani ni mhusika mwenye kila alama nzuri ambazo zilitakiwa wakati wa kutafuta mjumbe wa kusafiri kwa ajili ya maendeleo ya nchi ya Kusadikika. Fadhili ni jina lenye asili ya neno فضيلة (*fadhwiilat*) lenye maana ya kutaka fadhila kutoka kwa muumba kwa kufanya jambo bila ya malipo. Katika riwaya ya *Kusadikika*, mhusika huyu amejitolea muhanga kimaendeleo kwa ajili ya nchi yake ya Kusadikika. Adili ni jina lenye asili ya neno عادل (*ghaadil*) lenye maana ya uadilifu. Katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, Adili ni mhusika muadilifu katika utoaji wa hukmu. Radhia ni jina lenye asili ya neno رضي (*radhwaa*) lenye maana ya kuridhika. Katika riwaya ya *Utubora Mkulima*, mhusika huyu ni maridhia kwa kila jambo na asiye matatizo. Kwa mnasaba huo, tunaweza kusema usomaji wa Muhammed Said Abdulla ulikuwa ni wa malengo na manufaa makubwa.

Aidha, kwa maoni ya mtafiti, Muhammed Said Abdulla alikuwa ni mtu mwenye hekima na busara sana. Hii ilitokana na tabia yake ya kuchanganyika na watu hasa wazee wa Kizanzibari katika kuchambua mambo mbalimbali. Upekuzi wake wa mambo aliokuwa nao uliweza kuisoma jamii yake vilivyo, kisha kuiweka kitabuni

kama ilivyo. Mnasaba na hilo, utafiti huu umegundua manufaa mengi ya kazi zake kwa jamii husika na Waswahili kwa ujumla. Mfano mmojawapo ni kipengele cha mandhari. Muhammed Said Abdulla ameitumia mandhari halisi ya Zanzibar yenye kila vielelezo vitambulikavyo kama vile lugha alizowapa wahusika, majina yao na maudhui waliyoyafikisha. Lugha hiyo ni yenye mchanganyiko wa msamiati wenye chimbuko la sehemu tofauti kama wanajamii wenyewe walivyokuwa wakiitumia huko nyuma na mpaka sasa. Pia, dhamira za riwaya hizo ni kama vile vifo, mapenzi, ndoa, talaka, eda, maradhi, malezi, utumikishwaji na biashara ambazo zina uakisi na jamii hiyo.

Baada ya ufafanuzi huo, sehemu inayofuata inaeleza tija na madhara ambayo wasomaji hupata kutokana na matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla.

4.5.1 Tija Zilizopatikana

4.5.1.1 Kuvutika na Uandishi Wake

Matumizi ya lugha yenye mnato na mvuto katika riwaya za Muhammed Said Abdulla humfanya msomaji kuwa na hamu ya kuendelea mbele ili kuona hatma ya utunzi huo. Hii hutokana na msomaji kutotosheka na kutochoka kuendelea kusoma riwaya hizo kutokana na raha na ladha ya utunzi huo. Katika kulitilia mkazo suala hilo, Sengo (2011) ametoa mifano ya maneno hayo kupitia riwaya za Muhammed Said Abdulla, yanayoonesha hekima, ladha ya uandishi na raha kwa msomaji. Maneno yenyewe ni kama vile 'Ukitaka kujua asili ya mwangaza ingia kizani', 'Sasa, mtu akichagawa, shetani hukaa wapi hasa, mwilini au rohoni mwake?', 'mwiba uchomeako ndiko utokeako', 'Shibe kamwamini njaa, Njaa alikiangamiza chakula chote tumboni mwake', 'kuzinduwa ni kuzingua', 'kusitua ni kuroga na kuroga kuna kutengeza na kuangamiza'.

Aidha, matumizi ya taharuki katika usimuliaji wa kisa ni mbinu nyingine ya kushawishi na kutia hamu ya kuendelea mbele pamoja na kutochosha. Muhammed Said Abdulla huwadhhibiti na kuwatawala wasomaji wake kwa usimulizi wa namna hiyo kwa kuwanyima habari inayowazuia wasomaji wasifikie haraka upeo wa tukio. Katika unyimaji huo hudokeza kidogo kidogo hatua za kufikia upeo wa kisa. Kwa mfano katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, alianza mwisho wa kisa ambao unaonesha jawabu la maswali mengi ambayo yalikuwa yakimtanza Najum juu ya umahiri wa Bwana Msa. Kwa msomaji wa riwaya hiyo, huweza kujiuliza imekuwaje kutokana na kutoelewa nini kinakusudiwa? Hali hiyo humtia hamu msomaji ya kutaka kufahamu nini kilijiri. Hapo ndipo mwandishi alipoanza na kutiririka na kisa kidogo kidogo kueleza chanzo cha yote.

Katika kipengele cha kuwavuta wasomaji ili wawe karibu na mtunzi, Muhammed Said Abdulla amejenga taswira ijengekayo katika akili ya msomaji wakati wa kusoma riwaya hizo. Taswira hizo hutokana na maneno yaliyotumika katika kukieleza kitu kama kilivyo kinaganaga hata ikafikia kukiona katika macho ya msomaji. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* katika sehemu za maonesho ya sinema za Kihindi na Kizungu, nyumbani kwa Hakimu Marjani, ukumbi wa Spekta Seif na sehemu yenye kila aina ya ghurubiko la maisha kama kutafuta kijio, ulevi, ngoma, kamari na mengineyo. Haya ni maeneo ambayo mwandishi ameyazungumza kiuhalisia kabisa kiasi ambacho unaweza kupata picha sahihi ya maeneo hayo kutokana na maisha yaliyozunguka ukweli huo. Mfano kama sehemu yenye ghurubiko la maisha ni eneo maarufu Zanzibar lililojulikana kwa jina la Kundemba. Eneo hili lililokuwepo nyuma ya nyumba ya mtunzi huyo na lilikuwa linasifika kwa masuala maovu kama kamari, ulevi na ngoma. Masuala hayo pia

yamedhihirika katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* kupitia matendo ya wahusika kama Kasim na rafiki zake kwa ulevi na kamari. Katika hali hiyo, msomaji wa riwaya ya *Duniani Kuna Watu* hujenga taswira kamili ya 'Kundemba' katika akili wakati wa kusoma riwaya hiyo.

4.5.1.2 Kubainisha Historia na Athari ya Wakoloni kwa Wenyeji wa Zanzibar

Athari hiyo imeibuka kutokana na utumiaji wa lugha ama kwa utohoaji wa maneno kutoka lugha za Kigeni; Kiarabu na Kiingereza kama tulivyoona katika lengo la kwanza na la pili. Pia, imebainika kupitia matumizi ya Kiswahili chenye athari ya lugha za asili kupitia wahusika Seti B. Sumatra na Mmanga Muuza Duka pamoja na uigaji wa matamshi kimakosa kama alivyokuwa akifanya Inspekta Sefu kuwaiga Wamanga na Mabaniani. Hili limedhihirika katika riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale*, ukurasa wa 51, wakati Mmanga Muuza Duka anaeleza haya:

Kafanya kher, Sbakta Seif, mafanya kher makugya kwangu. Mimi mwenyewe nataka nakugya huku huku steeshin nariboti kwako. Yule Mwarabu mgyeni bu nafika kwangu gyuzi, gyana maondoka haba wakati ya Imaghribi, sinarudi tena hata l'aan. Leo natazama naona ufanga yangu hayuko mahl yake, la shaka mashkuwa yeye tu.

Pia, katika ukurasa wa 62, Inspekta Sefu anamuiga Baniani kwa kusema:

Inspekta Sefu alianza, "Sikiliza Seti; mimi makuja nataka uliza we' kidogo. Jana wakati wa magharibi Bwana Ali, jirani yako, maonekana makuja hapa kwako. Hebu eleza kidogo, Bwana Ali makuja hapa fanya nini?" alistusha kichwa chake kama desturi yake.

Matumizi ya namna hii humfanya msomaji mwenye ukuraba au unasaba na jamii za watu wanaozungumza hivyo kujihisi yupo karibu sana na mtunzi na hata mhusika wenyewe. Aidha, kupitia riwaya hiyo hiyo ukurasa wa 3, mwandishi anaeleza ujenzi wa majumba ya Zanzibar yalivyokuwapo kipindi cha uandishi wake. Dai hili linatiliwa mkazo na Fundi Mvita¹⁰ wakati anafanya mahojiano na Mjawiri katika

¹⁰ Ni rafiki wa mtunzi Muhammed Said Abdulla ambaye alikuwa naye karibu kipindi chote cha uhai wake.

Makala ya Semina ya Kumuenzi Mwandishi (2012). Fundi Mvita anaeleza kuwa, alimsikia Muhammed Said Abdulla akisema kwamba, kabla ya kuendeleza kisa chake katika maandishi, alikuwa akifanya safari za kutembelea sehemu mbalimbali za Zanzibar. Alikuwa akifanya hivyo kwa sababu isije ikawa kinyume na uhalisia ulivyo na ndio maana utayakuta mandhari halisi ya Zanzibar na maeneo yake kama yalivyo.

4.5.1.3 Kubainishwa kwa Historia na Silika ya Mtunzi

Katika utunzi wake, Muhammed Said Abdulla alimtumia mhusika mkuu Bwana Msa. Mhusika huyu jinsi ambavyo aliumbwa ni sawa na mtunzi mwenyewe alivyokuwa. Katika mahojiano kati ya mtafiti na mwalimu Ali Mwalim juu ya tabia za Muhammed Said Abdulla, ameeleza mtafitiwa huyo kuwa, Muhammed Said Abdulla ni mvutaji mwenye kutumia toza, mpekuzi na mchunguzi, hataki kushindwa, anajifanya kuwa anajua kila kitu, anapenda kuchanganya lugha, anapasua nywele upande namna yake, mkimya kama bubu na akitembea anaweka shingo upande. Tunaporejea katika riwaya zake, sifa za mtunzi huyo zinawiana na sifa za mhusika wake, Bwana Msa. Uwiano huo unapatikana katika ujenzi wa lugha juu ya wahusika wake kupitia riwaya zake zote. Riwaya hizo zinathibitisha kuwa, Muhammed Said Abdulla ni mvutaji na mpekuzi na mchunguzi wa hali ya juu. Kwani ameweza kuichunguza lugha na akaitumia kwa ustadi wa hali ya juu. Akishadidia hoja hiyo Mjawiri (2011) anaelezea kuwa, inasemekana kuwa uchunguzi wa mambo mengi wa Muhammed Said Abdulla ulitokana na utayarishaji wa kipindi cha redio kilichoitwa 'Sadiki Ukipenda'. Kipindi hiki kilimlazimu mtunzi huyo kufanya tafiti za kadhia nyingi katika jamii yake ili kupata vipindi vya kuwasisimua wasikilizaji wake na kukuza hadhira yake. Matendo ya uchunguzi

kama hayo ni kama aliyahaulisha kutoka kwake binafsi na kumvisha mhusika wake mkuu Bwana Msa katika riwaya zake zote.

Aidha, usanii alioutumia Muhammed Said Abdulla katika kuibuni mandhari ya riwaya zake umebainisha uasili wake. Maeneo kama Mambomsiige, Vuga, Chwaka, Kazole, Kituo cha polisi - Malindi na Mbaleni ni sehemu zinazotambulika Zanzibar. Pia, wasifu wa majengo uliomo katika riwaya zake ni jambo la uhalisi wa majumba ya zamani yalivyokuwa. Utafiti huu umegundua ukweli wa uhalisia wa Zanzibar kwa kulinganisha maelezo ya Muhammed Said Abdulla anayosifia majengo hayo na matumizi ya vijilugha vinavyoiakisi Zanzibar. Ugunduzi huo, umeifanya tasnifu hii kubaini historia yake na ya jamii yake.

Hata hivyo, historia na silika ya mtunzi imebainika kupitia usawiri wa matumizi ya lugha. Usawiri huo ni ushahidi tosha juu ya visiwa vya Zanzibar kuwa ina lahaja zake na ni chachu na chimbuko la Kiswahili sanifu. Jambo hili huleta tafsiri ya kwamba mtunzi huyo ni mzalendo wa nchi yake. Hakutaka kujiweka mbali na jamii yake hata kidogo na ndio maana akaamua kubainisha kila kipengele cha uhalisi wa jamii yake, katika riwaya zake. Aidha, katika kuonesha msisitizo wa uzalendo juu ya nchi yake, Fundi Mvita anafafanua wasia wa mtunzi huyo kupitia mahojiano kati yake na Mjawiri (2011). Fundi Mvita alisema kuwa, Muhammed Said Abdulla aliacha wasia wa kuitunza Zanzibar. Alieleza kuwa Zanzibar ni nchi pekee duniani ambayo hailingani na nchi nyingine yoyote. Wasia huo umemfanya mtunzi huyo kuonekana ni miongoni mwa wazalendo wa Zanzibar. Ingawa uzalendo wake haukuonekana kipindi cha uhai wake, lakini kufanyika kwa mkutano wa maadhimisho ya kumuenzi mtunzi huyo ni dalili tosha. Katika maadhimisho hayo kumefanyika uchambuzi wa kazi zake kupitia vipengele mbalimbali kama lugha,

mandhari, wahusika, ujumbe, falsafa na nafasi ya mwanamke. Na leo hii kuna makala mzima inayomzungumza Muhammed Said Abdulla na utunzi wake.

4.5.1.4 Kutambulisha Lahaja Mbalimbali na Kuzitofautisha Kimatumizi

Athari hii hupatikana pale Muhammed Said Abdulla alipolitumia neno moja ambalo lina maana zaidi ya moja. Lakini kwa kuwa huwezi kupata maana mbili au zaidi wakati neno hilo linapotumika sehemu moja, utaikuta maana ya neno hilo imekengeuka maana ya lahaja moja na kukubali lahaja nyingine. Kwa mfano, neno 'biwi'; katika lahaja ya Kipemba lina maana ya mkusanyiko wa takataka. Lakini Kimakunduchi na Kitumbatu, neno hilo sio lazima iwe takataka tu, bali hata mkusanyiko wa vitu vyengine hutumika hivyo hivyo. Na hiyo ndiyo maana sahihi aliyoitumia mtunzi katika riwaya zake.

Pia neno 'uharara'; katika lahaja ya Kipemba lina maana ya maradhi ya ngozi. Lakini Muhammed Said Abdulla hakulitumia neno hilo kwa maana ya maradhi, bali amelitumia kwa maana ya kusema kitu ambacho kina uhakika bila ya kuwa na wasi wasi wowote. Matumizi hayo ya visawe sambamba na maana zilizokusudiwa huweza kulikuta neno linatumika katika lahaja zote lakini linatofautika baina ya lahaja moja na nyingine.

4.5.1.5 Kurahisisha Kueleweka kwa Maudhui

Muhammed Said Abdulla ametumia lugha ambayo ipo wazi wala haina matusi ambayo husababisha kuficha au kubadili maana zake wakati wa kutafsiri kazi hizo. Dhana hii haipingani na ile hoja inayosemekana kuwa Muhammed Said Abdulla ametumia lugha isiyoieleweka. Kwani, ukubalifu wa hoja hiyo ni pale ambapo msomaji wa riwaya ni miongoni mwa wanaokisoma Kiswahili tu sio kukizungumza. Kwa sababu kukizungumza Kiswahili na kukisoma ni vitu viwili vinavyotofautiana. Mtu anapokizungumza Kiswahili basi atakuwa yupo tayari kucheza nacho kwa

kukifinyanga namna awezavyo. Na hii si kwa Kiswahili tu bali ni miongoni mwa sifa ya lugha yoyote. Kwa maana ya kwamba, kadri unavyoitumia lugha ndivyo unavyozidi kuifahamu. Kwa mtu ambaye si mpekuzi wa kukisarifu Kiswahili, yumkini, matumizi ya lugha katika riwaya za Muhammed Said Abdulla yatakuwa na ugumu kwake. Na kwa ambaye ni mtumizi wa lugha ya Kiswahili, riwaya za mtunzi huyu atazifahamu mara moja.

Riwaya za Muhammed Said Abdulla zina uakisi mkubwa wa uhalisia wa Zanzibar katika vipengele vya wahusika, mandhari na dhamira. Vitu vyote hivyo vimeelezwa bila ya kificho kupitia matumizi mazuri ya lugha na muwala wa matukio. Hili humsababisha msomaji kuhisi kama anakisoma kitu ambacho tayari ameshakiona. Na kwa hivyo, ule ujumbe unaowasilishwa ndani ya riwaya hizo huweza kufika kwa urahisi.

4.5.1.6 Kushajiisha Matumizi ya Msamiati Uliopo Hatarini Kupotea

Kuna baadhi ya msamiati ambao ni nadra kuukuta katika matumizi yetu ya lugha ya kila siku ingawa msamiati huo upo katika makamusi. Mfano wa msamiati huo ni mwande, maarubu, mafamba, kihanshe, bera, rubaa, maganjo, rakadha, kijoyo, mbuya, ghera, ghamu na kimeme. Maneno hayo ni nadra kumkuta mtu anayatumia hata kama anayafahamu. Hii ni kwa sababu anaweza kukosa mahitaji yake kwa kutofahamika anachokizungumza. Hatimaye, tunajisahau wapi tulikotoka na kuipuuza asili yetu. Hivyo, shime jamii kuachana na mila potofu. Tuzitumie lugha zetu ili zisipotee.

4.5.1.7 Kubainisha Umahiri wa Mtunzi Katika Matumizi ya Visawe

Utunzi wa Muhammed Said Abdulla umeibua mambo mengi. Kupitia lugha ya utunzi huo kuna matumizi ya visawe ambavyo msomaji anaweza kuvibaini. Visawe hivyo ni vile vinavyokaribiana sana kimaana vikiwa na lengo la kutimiza dhana

moja. Mfano wa visawe hivyo kutoka katika *Duniani Kuna Watu* ni kujikosha, kujitoharisha, kujisafisha na kujinadhifisha katika ukurasa wa 3; kunishutumu, kunisuta na kunisusuika katika ukurasa wa 66; nilaumu, nisubu, unitukane katika ukurasa wa 81; na hafifu, dhaifu, dhalilifu katika ukurasa wa 96. Pia katika riwaya ya *Kosa la Bwana Msa* maneno kama iliailika, ikalika, ikadhoofika, ikatilifika katika ukurasa wa 79; na zuzu, dufu, duba au dudu katika ukurasa wa 122.

Hata hivyo, matumizi ya maneno na usambamba wake ni umahiri mwingine aliouonesha Muhammed Said Abdulla katika utumiaji wake wa lugha. Mbinu hii huiathiri jamii ya wasomaji kwenda sambamba na utunzi huo. Mfano katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* wakati Hakimu Marjani akiilaumu nafsi yake juu ya mwanawe Kasim, mtunzi anasema:

Nilipokutunduwa hata sasa umekuwa mtundu; nikakuengaenga hata ukawa huwezi kutendekezeka, nikakutendea kila kitu, hata ukawa mpumbavu wa kutenda mwenyewe; nikakulisha tamu hata ukawa husubiri uchungu wa shubiri; nikakuendekeza hata ukawa huginai, nikakudekeza hata ukawa hufai pesa mbili - a - ah, ama kweli, ajiipigaye nafsi yake, asilie (uk. 5).

Hili huonesha namna mtunzi alivyokuwa ni mzalendo na mtumizi mzuri wa lugha yetu ya Kiswahili.

4.5.1.8 Kuathiri Watunzi Wengine wa Zanzibar Waliomfuatia

Athari hii imejitokeza kupitia watunzi waliofuata wa Zanzibar kama ambavyo yeye aliathiriwa na Shaaban Robert. Mfano wa watunzi hao ni Said Ahmed Mohamed na Mohamed Suleiman Mohamed. Kwa mujibu wa Said Ahmed Mohamed mwenyewe katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi* (2012: 1-21) anaeleza ualimu wa mtunzi huyo kwa watunzi wa Zanzibar. Katika kutoa athari ya kazi za mtunzi huyo, amejitolea mfano yeye mwenyewe kupitia riwaya ya kwanza ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambayo ilimuathiri toka angali bado ni mwanafunzi. Aliathirika kupitia lugha,

muundo, wahusika, mandhari, usimulizi wa hadithi katika mchukuo na mabadiliko ya nafsi na wakati kuelekea upeo wake. Katika upande wa lugha, Said Ahmed Mohamed alijikita katika msamiati wa lahaja ya Kipemba. Pia, alieleza msamiati wa riwaya za Muhammed Said Abdulla kuwa umekamilika kimatumizi. Anasema kuwa, mtunzi huyo hakulitumia neno kwa ajili ya kutumika, bali linaburudisha, linamulika, linaongoza, linaamsha, linashitua, linatikisa, lina kunini na kukunini huku likikusogeza mbele mpaka ufikie mwisho wa hadithi. Maneno yake sharti yawe na kinyume ambapo ukitizama utaona kama ni upuuzi lakini ukizingatia utaona yana ukweli ndani yake.

Pia, mandhari ya *Mzimu wa Watu wa Kale* yameathiri sana riwaya yake ya *Asali Chungu*. Hili lilisababishwa na mazingira aliyokulia na kuishi Muhammed Said Abdulla na yeye kutobadilika. Walikuwa wakiishi pua na mdomo ingawa Muhammed Said Abdulla alishakuwa mtu mzima na Said Ahmed Mohamed angali bado mtoto. Hali hiyo ilimfanya Said Ahmed Mohamed kupenda sana kusoma kazi za Muhammed Said Abdulla kutokana na kuyapatia uhalisia matukio yaliyomo katika riwaya zake. Kwa hivyo, Said Ahmed Mohamed alitamani kuvisoma vitabu vingi vya Muhammed Said Abdulla ili awe mtunzi mzuri mfano wake.

Mwingine ni Mohamed Suleiman Mohamed ambaye ameathiriwa na Muhammed Said Abdulla kupitia kipengele cha lugha katika mtindo wa kuwatolea wasifu wahusika. Watunzi hawa hutoa wasifu wa wahusika kwa lugha ambayo msomaji anaweza kujenga picha katika akili namna alivyo mhusika huyo. Mara nyingi wasifu za wahusika wao hulandana na uhusika wao. Mfano wa wahusika hao ni Rehema na Sulubu katika *Nyota ya Rehema*, Mzee Mwinyi na Bahati katika *Kiu*. Majina hayo ya wahusika huwa na maana kulingana na matendo yao kama yalivyo majina ya

wahusika wa Muhammed Said Abdulla. Yaani, Sulubu - kutumikishwa; Bahati - kuwa na bahati nzuri; Mwinyi - kupenda ubwanyenye au umwinyi; na Rehema - mwenye kupata rehema za Mungu.

4.5.2 Madhara Yaliyopatikana

Matumizi ya lugha ambayo ameyatumia Muhammed Said Abdulla katika riwaya zake yanaweza kuwatenga baadhi ya wasomaji na hata kukosa wasomaji wa siku za baadaye. Utengaji wa baadhi ya wasomaji huweza kutokea pale ambapo, msomaji wa riwaya amekosa umahiri wa lugha ya Kiswahili. Hili linasababishwa na mtunzi huyo kuifinyanga lugha kwa msamiati ambao unalenga kwa hadhira husika. Riwaya zake zinahitaji umakini mkubwa wa kucheza na lugha kadri inavyotakikana; kwani, lengo lake siku zote halikuwa nyuma katika kuienzi Zanzibar na kila kinachotokana na nchi hiyo.

Aidha, utandawazi na maendeleo ya Sayansi na Teknolojia vinachangia sana ama kuikuza, kuiharibu au kuidumaza lugha. Tunapoiangalia lugha aliyoitumia Muhammed Said Abdulla katika riwaya zake tunakuta kuwa ina asili ya mchanganyiko wa lahaja na lugha za kigeni. Hivyo, lugha hiyo inaweza kuwepo hatarini kupotea kadiri siku zinavyoendelea. Katika kuchunguza msamiati wa kilahaja visiwani humo, imebainika kuwa kuna maneno mengi yameshapotea na mengine yanaendelea kupotea kutokana na watumiaji wake kujikita katika Kiswahili sanifu. Maneno kama vile faka, bulibuli, unyanya, duba, mbeja, kufu, mwande, sowera, mbuya, faitika na kinyangaa. Maneno hayo yanaweza kumletea ugumu wa kuyafahamu kwa mzaliwa yoyote wa Zanzibar wa miaka ya 1980. Sasa je, tujiulize kwa mtoto atakayezaliwa miaka ya 2020 na kuendelea anaweza kweli kuyapatia maana zake?

4.6 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imekusanya vipengele vinavyotoa majibu ya malengo ya utafiti huu. Majibu hayo yalijibika kupitia riwaya tatu teule za Muhammed Said Abdulla. Riwaya hizo zilichunguzwa kupitia kipengele cha lugha na athari yake kwa wasomaji. Utafiti uliegemea mweka mkuu wa nadharia ya uhalisia ambayo inaichunguza lugha katika muundo na muwala, hali halisi ya wahusika na lugha wanayotumia, na vielelezo vya kihistoria kupitia lugha, ambavyo vinasababisha mabadiliko makubwa ya kijamii. Kwa ujumla, miktadha hiyo imebainika. Sura hii imeeleza miktadha ya maisha ya Wazanzibari ambayo imeakisi mandhari ya riwaya teule, matumizi ya lugha ya jamii lengwa yenye usambamba na matumizi ya lugha ya riwaya hizo kupitia vielelezo vya kihistoria vya jamii yenyewe. Ushahidi wa hilo ni matumizi ya lugha kupitia riwaya ya *Mzimu wa Watu wa Kale* ambayo imebainisha uharibifu wa lugha uliokuwa ukifanywa na Wamanga na Mabaniani. Hii ilitokana na athari ya lugha zao mama ambazo ziliwafanya washindwe kukitamka Kiswahili vizuri. Lakini kadiri siku zilivyosonga na watu hao kuchanganyika na wenyeji, matamshi yalibadilika. Hata Muhammed Said Abdulla alipotunga riwaya nyingine ya *Duniani Kuna Watu* na *Kosa la Bwana Msa*, athari hiyo ilikwishatoweka. Hivyo, katika utunzi wake hakuonesha tena matamshi kama yale kwa sababu wakazi wote walikitamka Kiswahili sawa sawa. Hii inamaanisha kuwa nadharia ya uhalisia imefana katika uchunguzi wa lugha uliofanyika katika riwaya za Muhammed Said Abdulla kwa kuonesha mabadiliko hayo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Sura hii inaitamatisha tasnifu hii. Sura inaunda sehemu zinazofafanua muhtasari wa tasnifu, hitimisho la utafiti, utoshelevu wa nadharia ambayo ilitumika kama mwega wa kutolea matokeo ya utafiti, mapendekezo kwa tafiti zijazo na muhtasari wa sura.

5.2 Muhtasari wa Tasnifu

Utafiti huu una sura tano zinazojitosheleza. Sura ya Kwanza inahusu utangulizi wa kazi mzima ya utafiti kwa kubainisha istilahi muhimu, usuli, tamko la tatizo la utafiti, malengo yake, umuhimu wake, historia ya mtunzi teule, nadharia, mipaka pamoja na vikwazo na utatuzi wake. Sura ya Pili inahusu mapitio ya kazi tangulizi zilizohusiana na mada ya utafiti na mapengo yaliyopaswa kuzibwa. Sura ya Tatu ni usanifu wa mbinu za utafiti zikiwa ni taarifa za watafitiwa, eneo, njia na vifaa vilivyotumika katika kukusanyia data, uchanganuzi wa data, itikeli za utafiti pamoja na uhalali na uthabiti wa data. Sura ya Nne inahusu mjadala wa matokeo ya utafiti. Mjadala huo ulihusu historia ya maisha ya Wazanzibari, maelezo mafupi ya riwaya teule, matukio yenye msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari na etimolojia ya msamiati huo, muhtasari wa msamiati uliotumika na etimolojia yake pamoja na athari yake kwa wasomaji. Sura ya Tano inatoa majumuisho ya kazi nzima kwa kuweka wazi hitimisho, muhtasari na mapendekezo ya mtafiti juu ya tafiti zijazo. Mwisho kabisa kuna marejeleo na viambatisho ambavyo ni njia zilizotumika kukusanyia data za uwandani, udurusu wa kimaktaba, ratiba, makadirio ya bajeti ya utafiti na picha ya mtunzi wa riwaya teule.

5.3 Hitimisho

Utafiti huu unahusu taaluma na jamii kwa sababu unazungumzia fasihi na fasihi ni mali ya jamii. Kama mada ya utafiti huu inavyojieleza kuwa ilijielekeza katika kuchunguza matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari kupitia riwaya za Muhammed Said Abdulla, ni dhahiri kuwa ni fasihi inayotazamiwa katika jamii ya Wazanzibari. Utafiti huu uliibua changamoto kutokana na mada yenyewe kwani kuna wengi waliodai kuwa, kuna usawiri wa aina gani juu ya msamiati. Wengine walidai sio matumizi ya msamiati wenye kusawiri mazingira ya Kizanzibari bali ni lahaja. Pia, wengine walisema, hakuna matumizi ya lahaja ni Kiswahili sanifu alichokitumia mtunzi. Pamoja na changamoto hizo, mtafiti hakurudi nyuma bali, aliendelea kuandaa mikakati ya kuboresha na kufanikisha malengo lake ipasavyo. Hii ilitokana na kuitambua mada ya utafiti wake kuwa bado ni ngeni katika masikio ya wanajamii. Baada ya purukushani hizo, jibu limeibuka na limetoa wasi wasi kwa wale wengi wenye madai haya na yale. Jibu ambalo limeweza kubainisha matukio yenye msamiati na kutoa asili ya msamiati huo. Kisha, kuonesha ukweli wa uakisi wa msamiati huo na mazingira ya Kizanzibari. Uakisi huo umeingia katika kipengele cha lahaja ambazo zipo na zinazungumzwa Zanzibar. Hii huwaondolea mashaka wale waliodai kuwa hakuna matumizi ya lahaja katika riwaya za mtunzi huyo. Aidha, uakisi wa msamiati huo na lugha za Kigeni, Kiarabu na Kiingereza kutokana na historia ya Zanzibar ya kutawaliwa na koloni hizo. Pia, kigezo kingine kinatokana na utamaduni wa dini ya Kiislamu uliokuwepo na uliopo Zanzibar.

Aidha, suala la ugumu wa lugha katika kazi za Muhammed Said Abdulla linaweza kutokea iwapo msomaji atakuwa na upungufu wa kuelewa msamiati wa Kiswahili vizuri au kuwa msomaji wa lugha ya Kiswahili lakini si mzungumzaji. Tatizo hilo

linaweza kupungua kupitia uorodheshwaji wa msamiati na maana zake mwishoni mwa riwaya zenyewe. Aidha, utafiti huu ni chachu ya kuliondoa tatizo hilo kwa kuweka bayana msamiati na maana zake katika kila riwaya iliyotumika.

Hata hivyo, suala la muktadha katika kazi ya fasihi kama ni zao la jamii lenye kuleta uhalisia wa jamii na kazi yenyewe ni suala nyeti la kuzingatiwa. Suala hili haliwezi kukamilika katika uegemezi wa kipengele cha lugha wanayobebeshwa wahusika peke yake bali ni maisha ya watu hao kwa ujumla. Maisha hayo yanaweza kuchunguzwa katika muktadha wa jiografia, uchumi, siasa, utamaduni, sanaa na isimu. Hii ni kwa sababu fani na maudhui ya kazi yoyote ya fasihi kama ni zao la jamii haiwezi kwenda kinyume na uhalisia wa jamii hiyo. Sababu hiyo inaambatana na mtunzi binafsi wa kazi ya fasihi ni mwanajamii, naye hujibidiisha kuonesha ukweli ulivyo katika jamii yake. Kama hilo halitoshi, fani na maudhui anazowasilisha mtunzi katika kazi yake haziwezi kukwepa kipengele kimoja wapo cha maisha ya jamii yake. Kwa kulihitimisha hilo, utafiti huu umegundua asili ya Muhammed Said Abdulla, uhalisia wa kazi zake na jamii ya Wazanzibari kwa kuchunguza muktadha wa maisha wa wanajamii hao na yale yaliyomo ndani ya riwaya za mtunzi huyo. Kwa kuwa uchunguzi ulipitia kipengele cha lugha katika riwaya za mtunzi huyo, uhalisia wake umejibainisha kupitia muktadha wa maisha ya Wazanzibari kijiografia, kiutamaduni na kiisimu.

5.4 Utoشهlevu wa Nadharia

Uchunguzi wa utafiti huu uliegemea nadharia ya Uhalisia ambayo hutathmini uhalisia wa maisha na kuusawiri uhalisia huo katika kazi za fasihi. Msomaji au mhakiki wa kazi ya kifasihi anaweza kupata mambo mengi ambayo katika maisha yana uya kinifu. Uya kinifu huo huweza kujitokeza ama kupitia lugha, wahusika na kile wanachokiwasilisha pamoja na mandhari ya kazi yenyewe. Vipengele hivyo

vinaweza kupelekea kubainika kwa kazi ya fasihi ni ya muda gani kutokana na vielelezo vya kihistoria vinavyosababisha mabadiliko ya jamii husika.

Nadharia hiyo imetosheleza katika utafiti huu kwa kuichunguza lugha katika riwaya za Muhammed Said Abdulla na kubaini matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari. Msamiati huo umebainika kupitia vigezo vya kihistoria ambavyo ni usawiri wa wahusika na matumizi ya lugha zao unaolandana na usawiri wa jamii hiyo ya Kizanzibari. Ni ukweli usiopingika kwamba, jamii ya watu wa Zanzibar wanatumia lugha ya Kiswahili yenye kuchanganyika msamiati wake na lahaja zilizopo Zanzibar. Lugha hiyo imepatikana kutokana na kusanifiwa lahaja ya Kiunguja mjini. Lahaja hii ilikuwa inatumika sambamba na Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba. Pia uchunguzi ulibainisha matumizi ya msamiati wenye asili ya lugha ya Kiarabu. Hili halina shaka kabisa kwa kuiangalia historia ya Zanzibar. Hivyo utumiaji wa msamiati huo ni uhalisia wa jamii andikiwa, jamii ya Wazanzibari. Mnasaba na dondoo hizo, nadharia ya uhalisia imetosheleza katika uchunguzi huo.

5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Kuna tafiti nyingi zilizofanyika juu ya riwaya za Muhammed Said Abdulla. Utafiti huu ambao umechunguza matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari ni nyongeza nyingine muhimu. Hii ni kwa sababu, kwa maoni na fikra za mtafiti, anaamini kuwa ni kitu kipya kabisa ambacho kimeleta ubainifu wa asili ya msamiati wenye kusawiri mazingira hayo pamoja na athari ya matumizi ya msamiati huo kwa wasomaji. Pamoja na kuziba pengo hilo kupitia riwaya za mtunzi huyo bado kumeibua maeneo mengine yanayopaswa kuchunguzwa zaidi. Maeneo hayo ni pamoja na:

- a) Matumizi ya msamiati yanayosawiri mazingira ya Kizanzibari au sehemu nyingine kupitia riwaya za mtunzi yoyote wa kazi za fasihi.
- b) Matumizi ya semi na falsafa juu ya matumizi hayo katika riwaya za Muhammed Said Abdulla.
- c) Ujitokezaji wa kipengele cha dini ya Kiislamu na utamaduni katika riwaya za Muhammed Said Abdulla.
- d) Suala la ukombozi linavyojitokeza katika riwaya za mtunzi huyo.

5.6 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura hii imeeleza muhtasari wa mchakato wote wa utafiti kwa kuonesha mihutasari ya kila sura, hitimisho lilipatikana baada ya purukushani za uchunguzi huo, namna ilivyojitokeza nadharia ya uhalisia katika mjadala wa matokeo ya utafiti na ilivyoweza kutosheleza pamoja na kutoa mapendekezo kwa tafiti zitakazofuatia ndani ya riwaya za Muhammed Said Abdulla au watunzi wengine. Sura imejitosheleza kwa kuyamakinikia masuala hayo kwa ufupi sana na kwa uwazi bila ya kuchosha. Hivyo, imeweza kuifunga kazi hii kwa mtindo bayana wenye kufahamika.

MAREJELEO

- Abdulla, M. S. (1976), *Duniani Kuna Watu*, Afro Press Ltd, Nairobi.
- (1982), *Mzimu wa Watu wa Kale*, Eastern African Publication Ltd, Arusha.
- (1984), *Kosa la Bwana Msa*, Africana Publisher Ltd, Nairobi.
- Ahrenberg, L. (1984), *Kisima cha Giningi na Hadithi Nyingine za M. S. Abdulla*, Ilihaririwa na Abdul- Aziz Lodhi, The Department of Afro- Asia Language, UPPSALA, Urusi.
- Amin, M. E. (2005), *Social Science Research Conception, Methodology and Analysis*, Makerere University printery, Kampala.
- BAKIZA (2010), *Kamusi la Kiswahili Fasaha*, Oxford University Press, Nairobi.
- (2012), *Kamusi la Lahaja ya Kitumbatu*, Jamana Printers Ltd, Dar es Salaam.
- (2012), *Kamusi la Lahaja ya Kipemba*, Oxford University Press, Nairobi.
- (2012), *Kamusi la Lahaja ya Kimakunduchi*, Jamana Printers Ltd, Dar es Salaam.
- Baydoun, A. A. (2004), *Students' Dictionary: English- Arabic Bilingual Arabic- English*, Dar Al-Kotob Al-Ilmiyah, Beirut, Lebanon.
- BBC SWAHILI (2012), "Msamiati sio Mawasiliano," (3 Octoba, 2012- Saa 10:17 GMT) Iliyosomwa tarehe 20/7/2014, Saa 6: 15 AM katika http://www.bbc.co.uk/swahili/mobile/kwa_kina/2012/10/121003kiswahililil_ugha.shtm
- Gibbe, A. G. (1990), "Ufumbaji katika Ushairi wa Kiswahili," *Kiswahili*, Juzuu ya 1, Kur. 17.
- Haji, H. G. (2006), *Kamusi ya Kitumbatu*, Express Printing Services, Zanzibar.
- Hamad A. K. (2011), "Matumizi ya Lugha katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdullah (Bwana MSA)* (eds), University College Education of Zanzibar, Zanzibar. Kur. 95 - 108.
- Idd, A. Z. (2010), "Phonological Process in Kimakunduchi Dialects," *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Sarufi*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).

- Ingrams, W. H. (1931), *Zanzibar: Its History and Its People*, Stacey International, London.
- (1924), "The Dialects Zanzibar Sultanate," *The school oriental of and African studies: Part Three*, Vol. III, Pg. 18.
- Issa A. A. (2011), "Taswira ya Mwanamke katika Kazi za Muhammed Said Abdulla," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdulla (M. S. Abdulla)* (eds) University College Education of Zanzibar, Zanzibar. Kur. 83 - 93.
- Juma, M. A. (2011), "Ulinganifu wa Kimakunduchi, Kimtende, Kibwejuu na Kikizimkazi," *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Sarufi*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Kantangayo, K. (2011), "Matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika Kazi za Sanaa," Iliyosomwa tarehe 19/7/2014, Saa 6:10 AM katika <http://khadilkantangayo.blogspot.com/2011/04/matumizi-ya-lugha-ya-kiswahili-katika.html>
- Khamis, A. O. (2012), "Wazanzibari ni Jamii Yenye Asili na Ustaarabu Mseto (Cosmopolitan Society) na Sio Jamii ya Kibantu (Kiafrika)," *katika Majadiliano kwenye Jamii Forums, Jukwaa la Siasa*, 4 Agosti, 2012, Saa 19:46 GTM, Iliyosomwa tarehe 29/02/2015, Saa 04:30 PM katika <http://www.jamiiforums.com/jukwaa-la-siasa/303067print.html>
- Khamis, M. (2012), "Athari za Matamshi ya Msamiati ya Kiswahili Sanifu katika Kimakunduchi," *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Sarufi*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Khatib, M. S. (1983), "Historia ya Maendeleo ya Kiswahili Zanzibar," katika *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili: Lugha ya Kiswahili 1* (eds), Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Toleo la 1, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Uk. 23.
- Kiango, J. G. (2004), "Uundaji wa Msamiati Mpya katika Kiswahili: Zoezi Lenye Njia Mbalimbali," *katika Mradi wa Kuswahilisha Programu Huria, Warsha ya Arusha*, 11-22 Novemba, 2004, Iliyosomwa tarehe 18/7/2014, Saa 6:15 AM katika <http://www.kilinux.udsm.ac.tz/kiblog/documents/training/kiango.htm>
- Kothari, C. R. (2004), *Research Methodology Methods & Techniques*, New Age International (P) Ltd Publishers, New Delhi.

- Krain, E. (1998), "Cooparative Development in Zanzibar," *The Agrarian Constitution of Zanzibar and its Impact on Agricultural Development*.
- Madumulla, J. S (2009), *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*, Sitima Printers and Stationery Ltd, Nairobi.
- Maganga, C. (1991), "A study of Morphology of Kiswahili Kiunguja, Kitumbatu and Kimakunduchi," *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Sarufi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* (Haijachapishwa).
- Makuthuria, M. (2013), "Uislamu na Maendeleo ya Kiswahili," *Katika Uchambuzi wa Makala*, 24 Agusti, 2013, Iliyosomwa Tarehe 23/03/2015, Saa 2:45 PM Katika
<http://chomboz.blogspot.com/2013/08/uchambuzi-wa-makala.html#uds-searchresults>
- Mdowe A. R. (2011), "Falsafa ya Muhammed Said Abdulla Katika Kazi zake," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdullah (Bwana MSA)* (eds.), University College Education of Zanzibar, Zanzibar. Kur. 57 - 70.
- Mgeni, A. (1983), "The Element of Mystery in the Novel of Muhammed Said Abdulla ," *Kiswahili* 50/2, Pg. 48 - 57.
- Mjawiri, M. M. (2011), "Muhammed Said Abdulla, Jamii, Maisha yake na Utajiri wa Kazi zake," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdulla (Bwana MSA)* (eds), University College Education of Zanzibar, Zanzibar. Kur. 109 - 116.
- Mkawe, D. F. (2011), "Sayansi katika Riwaya ya Upelelezi ya Kiswahili," *Ripoti ya Utafiti Mdogo*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- Mohamed, A. A. (1994), *Zanzibar Facts, Figures and Fiction*, Colour Separated and Printed, Alkhayria Press Ltd, Zanzibar.
- Mohamed, M. S. (1972), *Kiu*, Educational Books Publishers Ltd, Dar es salaam.
- (1976), *Nyota ya Rehema*, Educational Books Publishers Ltd, Dar es Salaam.
- Mohamed, S. A. (2011), "Muhammed Said Abdulla: Mwalimu wa Waandishi wa Zanzibar," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdullah (Bwana MSA)* (eds.), University College of Education, Zanzibar. Kur. 1 - 21.
- Mugenda, O. M. & Mugenda, A. G. (2003), *Research Methods Qualitative and Quantitative Approaches*, ACTS Press, Nairobi.

- Mushengyezi, A. (2003), *Twentieth Century Literary Theory*, Mukono Bookshop Printing & Publishing Company Ltd, Kampala.
- Njogu, K na Wafula, R (2007), *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*, Sai Industries Ltd, Nairobi.
- Ntarangwi, N. (2004), *Nadharia za Fasihi*, Foundation, Nairobi.
- Oxford Advanced Learners* (2009), Oxford University Press, Oxford
- Rashid, A. M. (2011), "Undaji wa Wahusika katika Kazi za Muhammed Said Abdulla," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdullah (Bwana MSA)* (eds.), University College of Education, Zanzibar. Kur. 38 - 56.
- Robert, S. (1952), *Adili na Nduguze*, Macmillan, London.
- (1991), *Kusadikika*, Mkuki na Nyota Publishers, Dar es Salaam.
- Rweyemamu, U. (2013), "Kulinganisha Ufundi wa Muhammed Said Abdulla na Faraji Katalambula," *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Salim A. A. (2011), "Mafunzo na Ujumbe katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdulla (M. S. Abdulla)* (eds.) University College Education of Zanzibar, Zanzibar. Kur. 71 - 82.
- Sanga, A. N. (2012), "Ujumi katika Riwaya Pendwa ya Kiswahili: Mifano Kutoka kwa Muhammed Said Abdulla na Aristabulus Elvis Musiba," *Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Sengo, T. S. (2011), "Ubunifu wa Mandhari katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla," katika *Makala za Semina ya Kumuenzi Mwandishi Muhammed Said Abdullah (Bwana MSA)* (eds.) University College Education of Zanzibar, Zanzibar. Kur. 22 - 37.
- Senkoro, F. E. (1982), *Fasihi*, Dar es Salaam Press and Publicity Centre, Dar es Salaam.
- Sulaiman, M. S. & Onkalo, P. J. (2011), "Zanzibar: Sustaining the Environment at the Confluence of Cultures," Vol. 3, No. 2, Pg. 12 - 24, Iliyosomwa tarehe 19/7/2014, Saa 5:55 AM katika http://www.fig.net/pub/fig2011/papers/ts06c/ts06c_onkalo_sulaiman_5051.pdf.

- Suleiman, R. (2015), "Kupaa kwa Watalii na Changamoto za Maadili, Utamaduni, Zanzibar," katika *Nipashe*, 3 February, 2015, Iliyosomwa tarehe 26/02/2015, Saa 10:06 PM.
- Sumary, J. J. (2013), "Riwaya ya Upelelezi na Mabadiliko ya Kijamii: Mifano kutoka katika Kazi Teule za Muhammed Said Abdulla na Aristabulus Elvis Musiba," Tasnifu ya Shahada ya Uzamili ya Fasihi ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dodoma (Haijachapishwa).
- Temu, C. (1980), "Lahaja za Kiswahili," Tasnifu ya Shahada ya Uzamili katika Sarufi, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa).
- The History of Taarab in Zanzibar, Iliyosomwa tarehe 25/02/2015, Saa 3:13 PM katika http://www.zanzibarmusic.org/traditional_taarab_history.php.
- TUKI (2001), *Kamusi ya Kiswahili- Kiingereza*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- (2006), *Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Warner, A. (1916), "The Wahadimu of Zanzibar," *Journals of African Society*, Vol. XV, Pg. 24 - 26.
- Wellek, R. na Warren, A. (1984), *Theory of Literature*, New York: Harcourt Brace & Company.
- Whitely, W. H. (1960), "An Introduction of Rural Dialects of Zanzibar," *Swahili Journal*, Part one, Vol. 31, Pg. 2.
- Zanzibar Economic Bulletin (2004), Vol. 2, No. 2, April-June, Pg. 27.
- Zanzibar Investment Policy (2006), Pg. 4.

VIAMBATISHO

A: Dodoso kwa Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza wa Kiswahili (SUZA)

Maelekezo:

- Dodoso hili ni kwa ajili ya kukusanya data za utafiti wa kukamilisha Shahada ya Uzamili Katika Fasihi ya Kiswahili, Chuo kikuu Cha Dodoma (UDOM)
- Mada ya utafiti ni Matumizi ya Msamiati Unaosawiri Mazingira ya Kizanzibari katika Riwaya za Muhammed Said Abdulla.
- Unaombwa kutoa ushirikiano kwa kadri ya uwezo wako ili kufanikisha kazi hii.

SEHEMU A: Taarifa za Mtafitiwa

Jina (sio lazima): Umri:

Uko mwaka wa ngapi:..... Masomo ya kufundisha: Kiswahili na

Nambari ya Simu (sio lazima):

SEHEMU B

1(a) Muhammed Said Abdulla anatajwa kama ni miongoni mwa watunzi mashuhuri wa nathari za Kiswahili wa Zanzibar. Tutajie nathari zake ulizowahi kusoma, kuchambua au kuzisikia.

- a)
- b)
- c)
- d)

b (i) Je, kuna ugumu wowote unaotokana na kazi zake kupitia kipengele cha lugha aliyoitumia?

(a) Ndiyo (b) Hapana

ii) Kama jibu ni ndiyo, ni upi? Ueleze

.....
.....
.....

2(a) Mtunzi wa kazi za fasihi anapoandika kazi yake hulenga jamii ndogo tu ingawa kazi hiyo husawiri eneo kubwa na pana. Je, kwa maoni yako Muhammed Said Abdulla aliandika kwa kuulenga jamii gani?

- i. Jamii ya Wazanzibari na Watanzania kwa ujumla
- ii. Jamii ya watu wasiokuwa Watanzania

(b) Ukirejelea kazi zake unamuonaje kuhusu matumizi ya lugha? Je, ameitumia lugha ipasavyo kulingana na jamii yake au alikwenda kinyume na jamii yake?

.....

(c) Katika kuisana lugha, oneshwa vipengele vya kisanaa vilivyokithiri katika kazi zake.

- (i) Tamathali za semi (ii) Taswira (iii) Lahaja
- (vi) Mafumbo (v) Methali (vi) Msamiati unaosawiri Zanzibar

3(a) Tutajie kazi za Muhammed Said Abdulla zenye msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari.

- i.
- ii.
- iii.

b (i) Taja msamiati wowote unaoufahamu unaotoka katika riwaya ulizotaja katika (3a) ambao unasawiri mazingira ya Kizanzibari?

.....

.....

.....

ii) Bainisha msamiati huo, jamii na mahali unapozungumzwa ndani ya Zanzibar (Pemba na Unguja) katika kila riwaya uliyoitaja katika (3a) hapo juu.

Na	Riwaya	Msamiati	Jamii Inayoutumia	Mahali
i				
ii				
iii				

4(a) Chagua matukio matatu katika riwaya zake zozote ambazo zimetumia msamiati wa Zanzibar na utaje msamiati huo.

Na.	Tukio	Msamiati
i		
ii		
iii		

(b) Je, kwa maoni yako, msamiati huo uliotumika umeibua dhamira au ujumbe gani?

.....

(c) Eleza sababu zilizomsukuma Muhammed Said Abdulla kutumia msamiati ambao ulisawiri mazingira ya Kizanzibari katika utunzi wake

.....

5 (a) Kwa maoni yako, matumizi ya msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya za Muhammed Said Abdulla yametoa athari gani kwa wasomaji?

.....

(b) Toa maoni yako ya jumla kuhusu uzuri au ubaya wa kutumia msamiati unaolandana na jamii lengwa ya kazi za fasihi

.....

*******Tunakushukuru kwa ushirikiano wako*******

B: Mwongozo wa Usaili kwa Wahadhiri wa Fasihi katika Vyuu Vikuu

1. Kitabia, unaweza kumuelezeaje Muhammed Said Abdulla?
2. Miongoni mwa watunzi mashuhuri wa riwaya za Kiswahili anatajwa Muhammed Said Abdulla. Tutajie kazi zake na ufundi (usanii) unaobainika ndani ya kazi zake.
3. Muhammed Said Abdulla, katika uandishi wake, ameathiriwa na mazingira alimokulia na kuishi. Thibitisha dai hili kwa kuchunguza namna mwandishi huyu alivyotumia lugha ya hadhira wake katika uandishi wake. Je, ameathiriwa na hali halisi ilivyokuwa jamii yake?
4. Ni tukio au matukio gani unayoyakumbuka katika kazi zake, yaliyotumika msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari kwa wingi?
5. Fikiria na utueleze etimolojia ya msamiati huo.
6. Kwa vile utunzi wake ulianza kabla ya Mapinduzi ya mwaka (1964); na kwa kuwa Zanzibar kabla ya kupatikana kwa Kiswahili kulikuwapo lahaja ambazo watu wake wakizitumia katika mawasiliano yao. Je, una maoni gani kuhusiana na msamiati uliomo katika riwaya zake?
7. Je, unadhani kuna sababu yoyote iliyomuongoza au kumsababisha Muhammed Said Abdulla kutumia msamiati wa Zanzibar katika uandishi wake? Eleza.
8. Toa tathmini yako juu ya kutumika kwa msamiati wa Zanzibar katika riwaya za Muhammed Said Abdulla na kuathiri kwake wasomaji.

*******Tunakushukuru kwa ushirikiano wako*******

C: Mwongozo wa Usaili kwa Jamaa wa Mwandishi Muhammed Said Abdulla

1. Unamfahamu vipi Muhammed Said Abdulla? (uzao, kuishi hadi kufa kwake, wazazi wake, kazi zake ndani ya fasihi na nje ya fasihi)
1. Kabla ya kupatikana lugha moja (Kiswahili) ambayo ilitumika kwa Zanzibar, Tanganyika, Kenya na Uganda, Zanzibar kulikuwepo vijilugha mbalimbali ambavyo wenyeji wake wakivitumia katika mazungumzo yao. Je, Muhammed Said Abdulla alikuwa ni mtumiaji wa vijilugha vipi?
2. Je, wewe binafsi umewahi kuzisoma kazi zake? Ni kazi gani ulizosoma?
3. Kama alitunga kwa ajili ya jamii yake, aliyoyakusudia ndani ya utunzi wake yaliwafikia hadhira aliyoilenga? Kwa nini?
4. Unazionaje kazi zake kuhusiana na lugha aliyoitumia? Je, imesawiri mazingira ya Kizanzibari? Kwa nini?
5. Kwa maoni yako, unadhani Muhammed Said Abdulla alipokuwa akitumia msamiati wa Zanzibar ndani ya kazi zake alikuwa akimaanisha kitu gani? Ni athari gani iliyopatikana juu ya msamiati huo?
6. Kwa mtu ambaye si mmahiri wa vijilugha au msamiati wa Zanzibar, anaweza kupata ugumu gani wakati anaposoma riwaya za Muhammed Said Abdulla?
7. Unadhani tunapoweka bayana msamiati unaosawiri mazingira ya Kizanzibari katika riwaya zake na kutoa asili ya msamiati huo inaweza kusaidia kuondoa ugumu wa lugha hiyo? Kwa nini?

*******Tunakushukuru kwa ushirikiano wako*******

D: Mwongozo wa Usaili kwa Wakazi wa Zanzibar

1. Naomba utueleze historia ya maisha yako kwa ufupi (mahali ulipozaliwa na kuishi n.k)
2. Ifuatayo ni baadhi ya misamiati aliyoitumia Muhammed Said Abdulla katika riwaya zake. Tunaomba utueleze asili na historia ya msamiati unaoufahamu:

Mapuza	Udhilifu	Kinyangaa
Tweza	Maarubu	Kihunzi
Rakadha	Mwande	Iliatilika
Masalheri	Beuo	Kusowera
Ukichuzana	Alidumaa	Kumduduka
Unayafilisha	Unyenyezi	Mkuukuu
Unayaviviza	Taalaki	Soni
Alidunduwaa	Kustaladhi	Kihanshe
Natija	Jiriwani	Fununu
Kujikaili	Mbeja	Kutakabari
Kortini	Zuhali	Ujuvi
Joko	Kusibika	Buhuri
Siungami	Kanchiri	Kujitonogoa
Mwashege	Zuti	Pogoka
Wajoli	Deko	Jaha
Kihunzi	Hariji	Kikaka
Zuzu	Biwi	Heba
Mtu mume	Kujikweza	Fetwa
Wivi	Marisedi	Machugachuga
Mafamba	Vono	Kidiku
Jiha	Pakanga/ pachori	Ruya
Wakibobokwa	Tutwe	Kibuhuti
Bilashi	Tao	Kujilabisi
Hoshi	Alivyogubika	Iliyoshii
Kukoroweza	Kigoron'gondwa	Mkanganyo
Ikakufutuni	Mumiani	Kiduhushi
Mbuya	Ufidhuli	Duba
Dufu	Dudu	Dude
Unyarafu	Afilishwe	Adokolewe
Shabuka	Vilinge	Madhabehi
Kigeugeu	Kubeza	Alimbibidia
Shaufu	Nikidinda	Akamjuvya
Akirendenda	Kwasi	Nyakanga
Kimeme	Marobota	Kunisusuika
Izara	Kumnukulu	Tuo

Faka	Uharara	Magolegole
Bezo	Ghera	Kufu
Mbwanda	Bera	Kunibazazi
Mzumbao	Alitaasafu	Shabuka
Kukuru	Kifu	Mnoga
Mrungura	Payo	Duwazi
Nakisi	Rubaa	Usodawi
Alimlaki	Maganjo	Alitaasafu
Alikuzaini	Akarengwa	Manzili
Zilichwea	Mang'amung'amu	Nibu
Hakukasiri	Kutazwa	Kukorwa
Barakoa	Alitunduwaa	Yaya
Tolatola	Ghabeni	Mhenga

*******Tunakushukuru kwa ushirikiano wako*******

E: Mwongozo wa Udurusu wa Kimaktaba

Katika udurusu huo, mtafiti ilimlazimu kupitia maandiko mbalimbali ili kukamilisha malengo ya utafiti. Maandiko yaliyolazimu kuyadurusu ni kama:

1. Kuzidurusu kwa makini riwaya teule za Muhammed Said Abdulla ambazo ni *Mzimu wa Watu wa Kale, Duniani Kuna Watu na Kosa la Bwana Msa.*
2. Kudurusu makamusi ya lugha ya Kiswahili, Kiarabu na Kiingereza pamoja na ya lahaja za Zanzibar, Kimakunduchi, Kitumbatu na Kipemba.
3. Kudurusu maandiko yanayomuhusu Muhammed Said Abdulla. Maandiko hayo yalijumuisha tasnifu za wataalamu mbalimbali, majarida, vitabu na makala. Udurusu huo ulizingatia vipengele kama uzao wake, familia yake, maisha yake, kifo chake na uandishi wake wa kazi za fasihi na zisizokuwa za fasihi.
4. Kudurusu maandiko yaliyohusu Zanzibar na Wazanzibari ili kuchunguza vipengele kama hali ya hewa, ardhi, makazi, idadi, lugha, utamaduni, utawala, uchumi, na sanaa. Maandiko hayo yalijumuisha tovuti, makala, majarida, tasnifu na vitabu mbalimbali.
5. Kudurusu maandiko yanayohusu lugha kwa ujumla. Hii ni kwa sababu utafiti huu ulifanyika katika kipengele cha matumizi ya msamiati. Maandiko hayo yalijumuisha tovuti, majarida na vitabu.
6. Kudurusu maandiko yanayoelezea nadharia mbalimbali za fasihi. Maandiko haya yalijumuisha vitabu kadhaa ili kuangalia ni nadharia ipi inayofaa katika utafiti huu.
7. Kudurusu tasnifu za wataalamu waliopita wa ngazi hii na ya juu ili kupata mwelekeo katika mchakato mzima wa utafiti.

F: Makadirio ya Bajeti ya Utafiti

Na.	Matumizi	Gharama	Jumla
1.	Gharama za vifaa vya kiofisi: <ul style="list-style-type: none"> • Kalamu za wino na wino wa kufutia. 5,000/= • Mabunda 3 ya karatasi za A4 kwa ajili ya kunukulia maandiko maktabani na kuandikia nakala kwa hatua za uandishi, usomaji na uhariri @ 10,000/= 30,000/= • Vitabu vitatu vilivyoteuliwa vya Muhammed Said Abdulla @ 6,500/= 19,500/= • Vidaftari 5 vya kuchukulia nukuu wakati wa ukusanyaji wa data @ 1,000/= 5,000/= 		59,500/=
2.	Gharama za nauli za kufuata huduma kwa msimamizi (Dodoma), kukusanya data, chakula na malazi: <ul style="list-style-type: none"> • Nauli ya Zanzibar - Dodoma kwenda na kurudi (safari 10 x 86,000/=) 860,000/= • Gharama za kujikimu (chakula na malazi) Dodoma kwa siku 40 kutokana na safari 10 (40 x 9,000/=) 360,000/= • Usafiri wa ndani (SUZA, BAKIZA na Malindi kwa ukusanyaji wa data mbalimbali (45 x 7,000/=) 315,000/= 		1,535,000/=
3.	Gharama za mawasiliano na zana za utafiti: <ul style="list-style-type: none"> • Gharama za mawasiliano ya simu 200,000/= • Kompyuta na vifaa vyote katika shughuli za utafutaji wa data mtandaoni, uchapaji na uhifadhi 700,000/= 		900,000/=
4.	Gharama za kupiga chapa muswada na utengenezaji wa tasnifu: <ul style="list-style-type: none"> • Kutoa nakala kwa awamu mbalimbali za usomaji na uhariri 200,000/= • Kutengeneza nakala nne za tasnifu ya mwisho ya utafiti 400,000/= 		600,000/=
Jumla Kuu			3,094,500/=

G: Ratiba ya Mchakato wa Utafiti

Na.	Shughuli	Muda wa Utekelezaji												
		Mwaka 2014						Mwaka 2015						
		J	J	A	S	O	N	D	J	F	M	A	M	J
1.	Kuandaa wazo la utafiti na kuwasilisha	■	■											
2.	Kuandaa pendekezo la utafiti, dodoso na hojaji na kuwasilisha			■	■									
3.	Kuirekebisha pendekezo la utafiti kulingana na maoni ya msimamizi					■								
4.	Kukusanya data na kuzichanganua						■							
5.	Kuandika tasnifu ya utafiti mara ya kwanza							■	■					
6.	Kuirekebisha tasnifu kwa mara ya kwanza									■				
7.	Kuiwasilisha tasnifu kwa mara ya pili										■			
8.	Kuirekebisha tasnifu kulingana na maoni ya msimamizi											■		
9.	Kuiwasilisha tasnifu kwa mara ya pili na ya mwisho												■	■

H: Picha ya Mtunzi wa Riwaya Teule, Muhammed Said Abdulla

